# Nipashe

Jumatatu Septemba 2, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 05780012

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Tisa mbaroni tuhuma za kubadilisha fedha za kigeni

UKURASA 3




UKURASA 13

# Korti kumaliza ubishi ubunge wa Lissu leo

UKURASA 2


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**VIFO AJALI YA LORI LA MAFUTA VYAFIKIA 104**

IDADI ya watu waliopoteza maisha kutokana na ajali ya lori la mafuta iliyotokea mkoani Morogoro Agosti 10, mwaka huu, imefika 104 baada ya majeruhi wengine wawili kupoteza maisha kati ya...

UKURASA WA 5

**BUGANDO MBIONI KUANZISHA TAASISI MAGONJWA YA MOYO**

HOSPITALI ya Rufani ya Bugando, inatarajia kuanzisha kituo cha taasisi ya kutoa huduma za magonjwa ya moyo, kitachogharimu kiasi cha Sh. bilioni 59...




Wasanii kutoka Jimbo la Yunnan nchini China, wakigawa chai kwa washiriki wa semina kuhusu utamaduni wa chai ya kichina katika Kituo cha Utamaduni wa China, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Vikwazo vinavyoua viwanda vyatajwa

UKURASA 3

## Ruwa'ichi: Nitaendeleza alikoishia Kardinali Pengo

**AWEKA** wazi mambo atakayoyapa kipaumbele...*Endelea ukurasa wa 2*


## TAIFA STARS vs BURUNDI

SEPTEMBA 8, 2019 • UWANJA WA TAIFA




215393302

HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

# Mahakama kuamua leo kuhusu jimbo la Lissu

**Na Enock Charles**

HATIMA ya kuapishwa kwa mbunge mteule wa Jimbo la Singida Mashariki, Miraji Mtaturu (CCM), itajulikana leo baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kuamua iwapo itatoa zuio la kuapishwa kwa mbunge huyo ama la.

Katika maombi yaliyowasilishwa mahakamani hapo na kaka wa aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Tundu Lissu, Alute Mungwai Lissu, pamoja na mambo mengine, ameiomba Mahakama hiyo itoe zuio la kuapishwa kwa mbunge huyo mpya na ruhusa ya kumshtaki Spika wa Bunge, Job Ndugai, kwa kumvua ubunge pasipo sababu za msingi.

Awali Mahakama hiyo ilitupilia mbali mapingamizi yaliyowekwa na upande wa Jamhuri uliotaka kesi hiyo isisikilizwe mahakamani hapo, kutokana na walichodai ni mapungufu ya kisheria ya maombi hayo, hivyo kutaka yasisikilizwe.

Jaji wa Mahakama Kuu, Sirilius Matupa, aliyatupa mapingamizi hayo baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili kwa maelezo kwamba upande wa Jamhuri haukuwa na hoja za msingi za kuizuia kesi hiyo isisikilizwe mahakamani hapo, hivyo kukubaliana na hoja za Wakili wa Lissu, Peter Kibatala.

Kwa mujibu wa maombi namba 18 ya mwaka 2019, Tundu Lissu anaiomba Mahakama impe kibali cha kufungua kesi dhidi ya Spika Ndugai na ili mahakama hiyo itoe amri ya kumtaka Spika ampe taarifa ya kumvua ubunge.

Katika hati ya dharura Lissu anaiomba mahakama isikilize na kutoa uamuzi haraka kabla ya kuapishwa kwa mbunge mteule Mtaturu aliyerithi kiti hicho, baada ya kutangazwa mshindi kwa kupita bila kupingwa.

Juni 28, mwaka huu wakati akiahirisha mkutano wa 15 wa Bunge, Spika Ndugai alitangaza uamuzi wa kumvua ubunge Tundu Lissu kwa maelezo kuwa alishindwa kuhudhuria vikao kwa muda mrefu bila kumjulisha pamoja na kutokujaza taarifa za mali na madeni kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.



Rais John Magufuli akiwa na mkewe Janeth Magufuli, mke wa Waziri Mkuu, Mama Marry Majaliwa, pamoja na waumini wengine wa Kanisa Katoliki wakishiriki Misa Takatifu Dominika ya 22 ya Mwaka "C", iliyofanyika katika Kanisa la Mtakatifu Petro, Parokia ya Oysterbay, jijini Dar es Salaam jana. Ibada iliyoongozwa na Paroko Msaidizi, Padre Dk. Alista Makubi. **PICHA: IKULU**

# Ruwa'ichi: Nitaendeleza alikoishia Kardinali Pengo

**Na Agnes Shayo, TUDARCO**

ASKOFU Mkuu mpya wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Jude Thaddaeus Ruwa'ichi, amesema ataendelea kutoa huduma za kiroho na kijamii kwa Watanzania pale alipoishia mtangulizi wake, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo.

Kardinali Pengo aling'atuka katika nafasi hiyo Agosti 15, mwaka huu, kwa ruhusa ya ya Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, baada ya kutimiza umri wa kuzaliwa wa miaka 75.

Askofu Mkuu Ruwa'ichi, alisema katika mahojiano Jiji la Dar es Salaam, kanisa linaendelea kuwavuta watu wengi kutoka mikoa na majimbo yote Katoliki Tanzania, na wanapofika wengi wao hawakai katikati ya mji bali wanatawanyika katika maeneo mbalimbali, ambako huenda kuanzisha maisha na familia zao, hivyo moja kwa moja wanajikuta wakihitaji huduma za kanisa zikiwamo zote muhimu za kijamii.

"Kikubwa ni kuhakikisha huduma zinasogezwa karibu na watu, mtangulizi wangu Baba Mwadhama alipoingia, alikuta hili jimbo likiwa na parokia 20 tu... leo hii ameondoka ameliacha lina parokia 118, hiyo ni kazi kubwa sana ila hutuwezi kusema kuwa kazi imeisha, maana hili jiji, linakua kila uchao na linazidi kutanuka," alisema Askofu Mkuu Ruwa'ichi.

Kuhusu vipaumbele vyake, alisema kwa kuwa kanisa la Dar es Salaam halipishani na kanisa la ulimwengu wote, ambalo lina utajiri mkubwa wa vijana na watoto wenye ari na nguvu, ambao ndio wamebeba sura ya Taifa na ya ulimwengu mzima, hivyo kazi kubwa anayoiona mbele ni kuwaandaa vijana hao na watoto vizuri maana wao ndio wanaotarajiwa kuwa watendaji wakubwa katika jamii inayotuzunguka.

Aidha, Askofu Mkuu Ruwa'ichi aliyataja masuala makubwa katika jamii ambayo alisema hayakwepeki kufanyiwa kazi na kanisa ni kusimamia vyema suala la kazi, fursa na changamoto zake.

Alisema kuwa katika uongozi wake anatamani kuona kila mwanajamii anakuwa sehemu ya maendeleo na kila mmoja ajenge tabia ya kujihoji kuwa: "Mimi kama mtoto wa Mungu mchango wangu katika maendeleo ya kijamii ni upi?"

Kuhusu elimu, ni muhimu kutambua aina ya elimu inayotolewa iwe ni ile inayoendana na malengo yatayokayomsaidia yule anayeelimishwa.

Kuhusu changamoto mbalimbali ambazo amekuwa akiziona katika utumishi wake ambayo si nzuri sana kwa sasa ni vijana wengi kutokuwa wakarimu kwa kujizuia kuzaa idadi kubwa ya watoto ilhali walio wengi wanazo fursa nyingi ukilinganisha na miaka waliyozaliwa wao.

"Kama kijana wa leo ukimwambia awe na watoto watatu au wanne, atakwambia watakula nini, nitawaleaje, watasomaje nk, na huyu anayekwambia hivi ni yule mwenye mshahara mzuri au kipato cha uhakika," alisema na kuongeza:

"Ukilinganisha na wazazi wangu walivyokuwa na maisha ya chini sana, lakini bado waliweza kutuhudumia sisi wote tisa na kutupatia kila tulichokihitaji ikiwamo elimu, japo sio wote tulifika vyuo vikuu."

Alitoa wito kwa vijana wa leo kujitafakari upya ili waweze kushiriki kwa makini zaidi kazi ya Mungu ya uumbaji, huku akiwataka washiriki pia kazi ya malezi kikamilifu, hasa kwa kutenga muda wa ziada kwa ajili ya watoto na familia zao, kuzungumza nao kujibu maswali yao sambamba na kutazama kazi zao za ziada wanazopewa shuleni, badala ya kuamini kuwa kwa kuwapatia karo, usafiri mzuri, nguo chakula, malazi, huduma za afya na vifaa vya kuchezea wamemaliza majukumu yao.

"Unaweza kukuta wamezaliwa watoto, wanapatiwa kila kitu wanachokihitaji vikiwamo vyombo vya kuchezea, vifaa vya masomo, lakini utakuta wazazi wao hawawekezi muda wao kwa ajili ya watoto, ambapo unaweza kukuta wapo watoto wanawaona wazazi wao labda mara moja tu kwa wiki, hii haitoshi kabisa, yafaa wazazi wapate muda wa kutosha kukaa na watoto wao."

Aliwaomba waumini wa kanisa hilo, wakiwamo watawa, wakleri, walei na kila mmoja, ushirikiano wao kama familia ya Mungu, huku akiwasihi waendeleze umoja na mshikamano na kuwa kitu kimoja na kuwakumbusha kuyaelewa vyema mazingira wanayoishi.

Askofu Mkuu Ruwa'ichi aliyekuwa Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Mwanza, aliteuliwa na Papa Francis kuwa Askofu Mkuu Mwandamizi wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar Es Salaam Juni 2018, na aliwasili jimboni humo Septemba 7, 2018, na Agosti 15, 2019, alithibitishwa rasmi na Papa Francis kuwa Askofu Mkuu wa jimbo hilo, baada ya Kardinali Pengo kustaafu rasmi.

# Walarushwa mizani kukiona

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU Mkuu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), Mhandisi Elius Mwakalinga, amesema mfanyakazi yeyote anayesimamia mizani atakayebainika anachukua rushwa atachukuliwa sheria kali.

Taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilieleza kuwa Mhandisi Mwakalinga alitoa onyo hilo akiwa jijini Dodoma wakati akikagua miundombinu ya barabara, madaraja, mizani, magari na mitambo ya serikali.

Mhandisi Mwakalinga aliwaonya watendaji wa mizani nchini kuacha kucheza na mizani, kupokea rushwa na kuzembea kazini.

"Serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwani barabara nyingi zinaharibika kutokana na kubeba mizigo mizito na nyie watu wa mizani hamfanyi kazi yenu kikamilifu," alisema Mhandisi Mwakalinga.

Alisema elimu elekezi itatolewa kwa wafanyakazi wa ngazi zote hata maaskari wanaolinda katika mizani ili kuepusha vitendo vya rushwa na kuingizia gharama kubwa serikali.

Wakati huo huo, Mhandisi Mwakalinga alikagua mzani wa Njuki uliopo mkoani Singida, ujenzi wa daraja jipya la Msingi lenye urefu wa mita 75 na barabara za maingilio zenye urefu wa kilometa moja kwa kiwango cha lami, kwa gharama ya Sh. bilioni tisa.

Naye Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), Mkoa wa Singida, Injinia Matari Masige, alimweleza Mhandisi Mwakalinga kuwa ujenzi wa daraja hilo utakamilika kwa muda wa miezi 24.

alisema kuwa daraja hilo likikamilika litaunganisha Wilaya ya Mkalama Mkoa wa Singida na Wilaya ya Meatu Mkoa wa Simiyu na hivyo kuendelea kufungua mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami nchini.

Alisema ujenzi wa Daraja la Sibiti umekamilika na magari yameanza kupita juu, wananchi walioathiriwa na mradi wameshalipwa fidia.

**"Serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwani barabara nyingi zinaharibika kutokana na kubeba mizigo mizito na nyie watu wa mizani hamfanyi kazi yenu kikamilifu," alisema Mhandisi Mwakalinga.**

HABARI KITAIFA

# Vikwazo vinne viwanda kufa nchini vyatajwa

**Na Gwamaka Alipipi**

WAMILIKI wa viwanda nchini wamemtajia Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa vikwazo vinne ambavyo vinawakwamisha na kusababisha viwanda vingi kufa mojawapo ikiwa ni uingizwaji wa bidhaa nyingi za magendo.

Vingine ni uwapo wa bidhaa feki sokoni, wafanyabiashara wadogo kutembeza bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi, pamoja na ukaguzi wa mizigo wa mara kwa mara kwenye vituo.

Wakizungumza kwenye mkutano uliojumuisha Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI) na Waziri Bashungwa jijini Dar es Salaam, wamiliki hao walieleza kuwa wanakabiliwa na changamoto hizo ambazo baadhi zimekuwa chanzo cha viwanda kufa.

Makamu Mwenyekiti wa pili wa CTI, Shabir Zavery alisema: "Machinga wengi siku hizi wanatembeza bidhaa ambazo hazizalishwi hapa nchini, zinatoka nje ya nchi, tunakuomba Waziri uliangalie hili suala hili."

Hussein Kamote kutoka Umoja wa wazalishaji mafuta na sabuni alisema kuna bidhaa nyingi za magendo zinazoingizwa kwa njia zisizo za halali.

Akitolea mfano, Kamote alisema hivi karibuni meli kubwa ya mafuta ya kula ilishusha tani 22,000 visiwani Zanzibar, na matumizi ya mafuta visiwani Zanzibar ni tani 1,000 pekee.

Alieleza kuwa tani 1,000 za mafuta ya kula zilisafirishwa kuja Tanzania Bara kwa njia halali, lakini tani 20,000 hazijajulikana zilikwenda wapi.

"Mheshimiwa Waziri kwa taarifa nilizozipata hizo tani 20,000 za mafuta ya kula zilisafirishwa kuja Tanzania bara kwa njia ya magendo kupitia bandari bubu za Bagamoyo, Mtwara, Pwani," alisema Kamote.

Isaak Lupokela kutoka kiwanda cha Saruji Tanga, alisema wamekuwa wakipata tabu wakati wa kusafirisha mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda mkoani kutokana na ukaguzi wa mara kwa mara wa risiti unaofanywa na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Mwakilishi kutoka kiwanda cha Sigara, alimweleza Waziri Bashungwa kuwa kumekuwapo na ucheleweshaji wa ukaguzi wa mizigo inayotoka nje kutoka kwa maofisa wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

"Vitu vinavyoingia nchini vinachelewa kukaguliwa, mzigo unakaa bandarini mwezi, tunaomba kama kuna bidhaa zinatoka nje kwenye nchi zenye ukaguzi mzuri tunaomba zisikaguliwe tena zinapoingia nchini," alisema.

Wakijibu hoja hizo, Mkurugenzi wa TBS, Dk. Athuman Ngenya, alisema wanalazimika kufanya ukaguzi kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi kwa sababu bandarini kumeimarishwa kwa kuwekwa mifumo ya elektroniki. Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo alisema: "Tumeanzisha vituo vya ukaguzi eneo la nane nane Morogoro, Iringa na Msata lengo ni kukaagua thamani ya mzigo kama unaendana na risiti, baadhi ya magari yanabeba mzigo tofauti na kilichoandikwa kwenye risiti."

Kayombo alisema kuwa wamiliki wengine wanatumia risiti moja kusafirisha mizigo zaidi ya mitatu.

"Utakuta gari limepeleka mzigo Mbeya, risiti iliyotumika kusafirisha mzigo huo inarudishwa Dar es Salaam na kutumika kusafirishia mzigo mwingine," alisema Kayombo.

Waziri Bashungwa alisema serikali ipo katika mchakato wa kuunda kikosi kazi kitakachokuwa na jukumu la kupambana na bidhaa za magendo na bidhaa feki.

Alisema taasisi zote za serikali zinazojihusisha na biashara zitatoa mjumbe mmoja atakayeingia katika kikosi kazi hicho.

Alisema lengo kuu la serikali ni kuona bidhaa kutoka Tanzania zinatamba katika masoko ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi Kusini mwa Afrika (SADC).

Vilevile, aliwataka CTI kuhakikisha wanaongeza wanachama wengi kutoka 400 wa sasa na kufikia zaidi ya 500, hususani mikoani.

Makamu wa Rais wa kwanza CTI, Paul Makanza alisema sekya ya viwanda nchini inakua kwa asilimia 8.3, inachangia pato la taifa kwa asilimia 8.1, inachangia asilimia 25 katika ajira.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto), akizungumza na Spika wa Bunge la Kenya, Justin Muturi, walipokutana katika hoteli ya Madinat Al Bahr Business and Spa mjini Zanzibar jana, kabla ya kuanza kwa kikao cha Kamati ya Utendaji ya Chama cha Mabunge Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika. **PICHA: BUNGE**

## Tisa waswekwa ndani sakata ubadilishaji fedha za kigeni

**Na Rose Jacob, MWANZA**

JESHI la Polisi mkoani Mwanza kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, limewakamata watu tisa wanaotuhumiwa kujihusisha na ubadilishanaji wa fedha za kigeni bila kuwa na leseni ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Watu hao ambao Jeshi la Polisi halijawataja majina yao, wanadaiwa kukutwa na kiasi kikubwa cha fedha za nchi mbalimbali duniani.

Operesheni hiyo maalum ya kusaka, kupekua na kukamata maduka, kampuni na watu binafsi wanaojihusisha na biashara haramu ya kubadilisha fedha za kigeni bila kuwa na leseni iliyotolewa na BoT kinyume cha Kanuni ya 4 ya Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni ya Mwaka 2019 pamoja na Sheria ya Fedha za Kigeni ya Mwaka 1992, pia imewezesha kukamata vifaa maalum vya kutunzia matukio ya CCTV- DVR mbili na kompyuta mpakato nne.

Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Muliro Jumanne, alisema watuhumiwa hao ambao wamekuwa akifanya biashara hiyo ambayo ina athari kubwa katika uchumi wa Taifa, walikamatwa Ijumaa katika operesheni hiyo ya kushtukiza.

Kamanda Muliro ametaja kiasi cha fedha kilichokamatwa zikiwamo dola za Kimarekani 14,084, EURO 200, zaidi ya Sh. milioni tatu za kitanzania, na risasi moja, magazini na bastola.

"Mahojiano na watuhumiwa waliokamatwa yanaendelea kufanywa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa dhidi ya vitendo hivyo vya uvunjaji wa sheria na kanuni husika," alisema Muliro.

Muliro alisema operesheni hiyo ilimalizika salama bila kuathiri wananchi wasiohusika, kwamba Jeshi la Polisi linawashukuru wa-

## Vifo ajali ya lori la mafuta vyafikia 104

**Na Mary Geofrey**

IDADI ya watu waliopoteza maisha kutokana na ajali ya lori la mafuta iliyotokea mkoani Morogoro Agosti 10, mwaka huu, imefika 104 baada ya majeruhi wengine wawili kupoteza maisha kati ya majeruhi 13 waliokuwa wamelazwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Majeruhi watano hali zao ni mbaya na wanaendelea kupatiwa matibabu katika chumba cha uangalizi maalum (ICU), huku wengine sita wakiwa katika wodi namba 22 ya Sewahaji.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa MNH, Aminiel Aligaesha, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, aliwataja waliopoteza maisha kuwa ni Asha Seleman (28) na Avelina Aman (30), aliyefariki dunia juzi.

"Majeruhi wa ajali ya moto iliyotokea huko Morogoro ambao walikuwa wanapatiwa matibabu hospitalini hapa wamebaki 11 baada ya wawili kupoteza maisha," Aligaesha alisema.

Alisema majeruhi 11 waliobaki wanaendelea kutibiwa na hali zao zinaendelea kuimarika.

Alisema mwili mmoja wa Avelina Aman (30), upo chumba cha kuhifadhia maiti ukisubiri taratibu za kusafirishwa kwenda mkoani Morogoro.

Kati ya majeruhi 47 walifikishwa hospitalini hapo kuanzia Agosti 11, mwaka huu, 36 wamefariki dunia.

Aligaesha alisema juzi walipokea miili ya watu watano waliopoteza maisha kwa ajali iliyotokea Kibiti mkoani Pwani.

Alisema walipokea miili hiyo juzi saa tano asubuhi na tayari imehifadhiwa chumba cha kuhifadhia maiti.

Aligaesha alisema miili hiyo ni ya watu wazima wanne na mtoto mmoja ambayo iliungua na kwamba utambuzi wake ni mgumu.

"Tayari hospitali yetu imefanya uchunguzi (postmortem) na kuchukua sampuli kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kitengo cha Forensic Pathology pamoja na Mkemia Mkuu wa Serikali ili kufanya uchunguzi zaidi," Aligaesha alisema. Aliwataka ndugu wa karibu wa marehemu kati ya baba, mama na mtoto kujitokeza kuanzia leo saa mbili asubuhi kwa ajili ya utambuzi.

"Tunaomba ndugu wa karibu hususani baba, mama au mtoto waje kesho (leo) kwa ajili ya kuchukuliwa sampuli na Mkemia Mkuu wa Serikali ili kusaidia kufanya uchunguzi wa kulinganisha vinasaba kati ya ndugu na marehemu na ili waweze kupewa miili hiyo kwa ajili ya mazishi baada ya uchunguzi kukamilika," alisema.

# Wafanyabiashara 80 wa China waja kusaka fursa na malighafi

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA 80 kutoka China wanatarajiwa kuwasili nchini keshokutwa kusaka fursa za uwekezaji na malighafi nchini.

Imeelezwa kuwa timu hiyo ambayo pia itafuatana na wawakilishi wa viwanda vinavyomilikiwa na Serikali ya China na vya watu binafsi nchini huko, itakuwa Dar es Salaam kwa siku mbili na baadaye itakwenda Zanzibar Septemba 6, mwaka huu kwa lengo hilo hilo la kusaka fursa za uwekezaji.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu ujio wa wafanyabiashara hao, Meneja wa Kituo cha Afrika Mashariki cha Biashara (East Africa's Commercial & Logistics Center Chamber of Commerce), Cathy Wang, alisema baada ya kuwasili jijini, timu hiyo itakuwa na mkutano na Wizara ya Viwanda na Biashara Jumatano.

"Kampuni nyingi ambazo wawakilishi wake wanakuja zinajishughulisha na sekta za kilimo na usafirishaji. Wanakuja kwa lengo la kuangalia soko la Tanzania na malighafi zilizopo kwa ajili ya viwanda ili kuimarisha zaidi uhusiano wa kimaendeleo uliopo kati ya mataifa hata mawili," alisema.

Wang alisema mkutano wa Jumatano utaikutanisha timu hiyo na wataalamu kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, EPZA, TPSF, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TCI) na kituo chake.

Wang pia alizungumzia mradi wa kujenga kituo cha biashara iliko stendi ya mabasi Ubungo utakaoanza mara tu baada ya stendi hiyo kuhamishiwa Mbezi jijini.

Alisema kituo kitakachojengwa kitakuwa na maduka milioni 2.6 ya bidhaa mbalimbali na kwamba mradi huo utakamilika ndani ya miezi 15, ukitarajiwa kugharimu Dola za Marekani milioni 114.



Wananchi wakitoa msaada wa kulitoa gari lililomshinda dereva na kutumbukia kwenye mtaro katika eneo la Goba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Utafiti wabaini sababu mazao 40% kupotea baada mavuno

**Na Enock Charles**

IMEELEZWA kwamba asilimia 40 ya mazao ya mkulima hupotea baada ya kuvuna kutoka na hifadhi na usimamizi hafifu na matumizi ya teknolojia duni.

Teknolojia duni inahusu uzalishaji, uvunaji, usafirishaji, uhifadhi na usindikaji hali inayoathiri kipato, maisha na uzalishaji wa mkulima.

Akizungumza katika mkutano na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na nafaka, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema kutokana na upotevu huo, na wakulima wengi wamekuwa wakipoteza mapato mengi yanayotokana na mazao yao.

"Ukisoma utafiti asilimia 40 ya mazao ya mkulima yanavyopotea unaweza ukaona ni kwa namna gani wakulima wetu wanavyoishi maisha duni ilhali wanapoteza kiwango kikubwa cha utajiri wao," Hasunga alisema.

Kwa mujibu wa utafiti wa Shirika la Kimataifa la Chakula na Kilimo (FAO), wakulima wa Tanzania hupoteza hadi asilimia 40 ya mazao baada ya kuvuna kutokana na changamoto za kiufundi zinazosababishwa na mtaji mdogo, ujuzi mdogo wa ubebaji mazao pamoja na matatizo ya masoko na sera.

Katika utafiti huo, nchi zinazoendelea makadirio ya upotevu wa mazao unaonyesha viwango tofauti vya upotevu katika mazao kama ya nyanya ambayo ni kati ya asilimia 20 na 50, viazi vikuu kati ya asilimia 10 na 60, ndizi kati ya asilimia 20 na 80 na mapapai kati ya asilimia 10 na 40.

Aidha, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na FAO mwaka 2011 kuhusu nafaka, umeonyesha makadirio ya upotevu katika nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika ni asilimia 13.5 matokeo yanayofanana na utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) mwaka 2012 ambayo yanaonyesha upotevu wa mazao makuu ya nafaka kama mahindi kwa asilimia 15.5, mpunga asilimia 10.7 na mtama asilimia 12.5.

Utafiti huo unaeleza zaidi kuwa pamoja na ongezeko la uzalishaji katika ngazi ya kitaifa linalokadiriwa wastani wa tani 9,445,000 kwa mwaka, teknolojia zinazotumika kabla, wakati na baada ya kuvuna husababisha upotevu wa wastani wa tani 3,782,000 kwa mwaka sawa na asilimia 40.

## Manara aomba mahakama kutupa madai dhidi yake

**Na Hellen Mwango**

MSEMAJI na Ofisa Habari wa Klabu ya Simba, Haji Manara, ameiomba mahakama kutupilia mbali madai ya fidia ya Sh. milioni 83 ya Kampuni ya Oman Dela Boss inayotengeneza manukato dhidi yake kwa madai kuwa anaidai kampuni hiyo Sh. milioni 31.

Manara aliwasilisha majibu na wenzake wawili dhidi ya kesi iliyofunguliwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam na Kampuni ya Abu Masoud Al Jahdhamy LLC, wakidaiwa fidia ya Sh. milioni 83 kwa kukiuka mkataba na kampuni hiyo.

Katika majibu yake ya utetezi Manara alidai kampuni hiyo anaidai Sh. milioni 31 sawa na asilimia 30 ya faida kutokana na matangazo ya manukato hayo ya Dela Boss.

Manara na wenzake wanapinga madai ya mdai ya kwamba waliingia mkataba wa ubia na wanamtaka mlalamikaji athibitishe hilo.

Kwa mujibu wa hati ya majibu, walalamikaji wanadai Manara alikuwa balozi na mwanahisa, alitangaza bidhaa hiyo katika mitandao ya kijamii, Twitter, Facebook, Instagram, YouTube, Snapchat and WhatsApp.

Manara alidai walikubaliana na mdai watagawana faida ya mauzo ya manukato hayo. Mapema mahakamani hapo, Manara na wenzake watatu wamefunguliwa kesi ya madai wakidaiwa deni na fidia ya Sh. milioni 83.3 baada ya kupokea bidhaa zenye nembo ya Dela Boss Perfume bila kuzilipia.

Mbali na fedha hizo, mlalamikaji Abu Masoud Al Jahdhamy LLC, ameiomba mahakama kuwaamuru walalamikiwa, Manara, Beatrice Ndungu na Palm General Supply, kumlipa fidia nyingine itayoona zinafaa na gharama za mawakili.

Kesi hiyo ya madai namba 128/2019 ilitajwa mwishoni mwa wiki iliyopita mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega, baada ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Wanjah Hamza, aliyepangiwa kuisikiliza kuwa na udhuru.

Katika madai ya msingi, mlalanikaji amefungua kesi hiyo akiwadai walalamikiwa fedha hizo baada ya kuwasambazia bidhaa yenye nembo ya Dela Boss Perfume 'Tanzania' zilizotengezwa Dubai. Ilidaiwa kuwa mlalamikaji aliingia mkataba na Manara Desemba 19, 2018 kwa kuchapa bidhaa zenye maneno hayo.

Katika mkataba huo, mlalamikaji alitakiwa kupata asilimia 70 na Manara asilimia 30 na kwamba faida itakayopatikana angemrudishia mlalamikaji gharama za uwekezaji wa kufikisha bidhaa jijini Dar es Salaam.

Januari 21, 2019 mlalamikaji kupitia kampuni ya AMA Trading LLC ilituma bidhaa jijini Dar es Salaam ambazo zina thamani ya Sh. milioni 46 na zilipokelewa na mlalamikiwa wa pili, Ndungu na wa tatu kama mawakala.

Januari 21, 2019 mlalamikaji alituma risiti ya madai (invoice) ya Sh. 83,300,000 kwa mlalamikiwa wa pili na wa tatu akitaka kulipwa faida ya uwekezaji na kiasi kilichotumika kununulia bidhaa hizo pamoja na faida.

Walalamikiwa walipokea bidhaa hizo na kwamba mpaka sasa hawajalipa chochote pamoja na kudaiwa kwa maneno na maandishi kutoka kwa mlalamikaji.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi (kulia), akisoma kipeperushi cha Benki ya NMB, alipotembelea mabanda mbalimbali kwenye Uwanja wa Sokoine, mjini Nachingwea juzi, kabla ya kufunga kampeni ya wiki moja ya "Elimu ya Mlipakodi na Tozo za Serikali". Wa pili kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango na (kushoto), ni Ofisa Mahusiano wa NMB wilayani humo, Ambokile Mwanjoka. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Taasisi kuipa Hospitali ya Mkapa basi hospitali

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Association of African Economy and Development in Japan (AFRECO), imeahidi kuipatia Hospitali ya Benjamin Mkapa ya Chuo Kikuu cha Dodoma basi ambalo ni hospitali kamili litakalotoa huduma za matibabu kwa Manispaa ya Dodoma, mikoa na wilaya zinazozunguka Mkoa wa Dodoma.

Basi hilo litakapowasili nchini kutoka Japan linatarajiwa kuwa ni mkombozi kwa wananchi waishio vijijini na katika maeneo ambayo hayana hospitali kwani kila litakakokwenda kutoa huduma litakuwa na madaktari waliobobea katika utaalamu wa tiba mbalimbali, vifaa tiba, maabara pamoja na dawa.

Hayo yamebainishwa jana na Rais wa AFRECO, Tetsuro Yano katika mazungumzo yake na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, nchini Japan.

Yano alisema wameamua kuanza kutoa misaada na huduma zao nchini Tanzania baada ya kufurahishwa na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano za kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Aliongeza kuwa anaamini siku moja Tanzania itakuwa nchi ya mfano kwa Afrika Mashariki na Afrika yote kwa kutoa huduma bora za tiba kwani itakuwa na vituo vingi vya afya na hospitali zenye uwezo wa kutibu magonjwa kama vile ya moyo na figo. Hata hivyo, wagonjwa toka nchi jirani wameanza kuja kutibiwa nchini.

Kwa upande wake, Waziri Mkuu alisema mbali na kutoa basi ambalo litakuwa linatoa huduma za matibabu, pia taasisi hiyo ya AFRECO itasaidia katika kupandisha hadhi Hospitali ya Benjamin Mkapa ya Chuo Kikuu cha Dodoma kuwa shule kamili ya tiba.

Amesema hospitali hiyo ya Benjamin Mkapa ya Chuo Kikuu cha Dodoma itapatiwa vifaa mbalimbali vya tiba ambavyo vitaifanya hospitali hiyo kuwa ni shule bobezi kwa utoaji wa tiba mbalimbali nchini Tanzania na Barani Afrika.

Kadhalika, Waziri Mkuu amesema kuwa wamekubaliana na AFRECO kuanzisha kitivo maalum cha uhandisi wa vifaa tiba ambacho kitafundisha uhandisi wa vifaa tiba ili nchi yetu iwe na wataalamu wa kukarabati vifaa tiba pindi vinapoharibika badala ya kuvipeleka nje ya nchi au kuagiza wahandisi na wataalamu kutoka nje ya nchi kuja kuvitengeneza.

"Hivi sasa yanafanyika makubaliano ya kuanzisha kiwanda cha kutengeneza vifaa tiba na kwa kuanzia wataanza kutengeneza maji ya drip ambayo huongezwa kwa wagonjwa kwa maelekezo ya madaktari na baadaye watengeneza dawa mbalimbali."

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Mipango, Utawala na Fedha, Prof. Donald Mpanduji, alisema wametia saini hati ya makubaliano kati ya AFRECO na Chuo Kikuu cha Dodoma ambayo yanalenga kuboresha Hospitali ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Awali, Dk. Omary Ubuguyu kutoka Wizara ya Afya, alisema maboresho yaliyofanywa na serikali katika huduma za tiba yameiwezesha Tanzania kupunguza wagonjwa wanaopelekwa nchi za nje kwa matibabu kutoka 800 hadi 42 ambalo ni punguzo la asilimia inayotajwa kuwa 200.

Alisema hatua hiyo imeongeza nafasi kwa wataalamu wetu wa tiba kujifunza zaidi pamoja na kuwapunguzia wananchi gharama za kusafiri kwenda nje ya nchi kutafuta tiba na pia imeipunguzia serikali gharama ya fedha za kigeni ambazo zingetumika kuwatibu wagonjwa nje ya nchi.

# Bugando mbioni kuanzisha matibabu magonjwa ya moyo

> **"Bugando tunatarajia kuanzisha kituo cha taasisi ya Moyo kwa ajili ya kutoa huduma za upasuaji magonjwa ya moyo na mafunzo, ambacho kitajengwa kwa ushirikiano wa Wizara ya Afya, wadau wa Mwanza, wafadhili wa nje na Kanisa Katoliki, alisema Prof. Makubi.**

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda Bugando mkoani Mwanza, inatarajia kuanzisha kituo cha taasisi ya kutoa huduma za magonjwa ya moyo, kitachogharimu kiasi cha Sh. bilioni 59.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi Mkuu wa hospitali hiyo, Prof. Abely Makubi, katika hafla fupi ya uzinduzi wa wodi vyumba 18 vya watu mashuhuri (VIP) na wodi vyumba vinane vya binafsi pamoja na vitanda 38.

"Bugando tunatarajia kuanzisha kituo cha taasisi ya Moyo kwa ajili ya kutoa huduma za upasuaji magonjwa ya moyo na mafunzo, ambacho kitajengwa kwa ushirikiano wa Wizara ya Afya, wadau wa Mwanza, wafadhili wa nje na Kanisa Katoliki, alisema Prof. Makubi.

Katika uzinduzi huo Prof. Makubi alisema Sh. milioni 230 zimetumika kujenga vyumba hivyo 18 vya wodi za VIP na Sh. milioni 132 zimetumika kujenga vyumba vya wodi binafsi vinane na huduma ya vitanda 38.

Hospitali hiyo imekuwa mtoaji mkubwa wa misaada kwa wagonjwa wasiojiweza, ambayo kila baada ya miezi mitatu hutumia Sh. milioni 420 sawa na Sh. milioni 140 kila mwezi kuhudumia bure wagonjwa wasiojiweza.

"Kila baada ya miezi mitatu tunatumia fedha nyingi kuhudumia wagonjwa maskini wasiojiweza ambao ni wajawazito, watoto chini ya umri wa miaka mitano na wazee kuanzia miaka 60 na kuendelea," alisema Prof. Makubi.

Alisema kuwa sambamba na kuboreshwa kwa mazingira ya hospitali hiyo na vifaa tiba, pia imeongeza madaktari bingwa na waliobobea katika magonjwa mbalimbali wakiwamo wazalendo na madaktari bingwa kutoka Nepali na Cuba.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, ambaye alikuwa mgeni rasmi, aliwataka wananchi wa mkoa huo kujiandikisha katika huduma ya bima ya afya.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars malizieni kazi Burundi

**TIMU** ya Tanzania, 'Taifa Stars' keshokutwa itashuka dimbani nchini Burundi kumenyana na wenyeji wao hao kwenye mechi ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar 2022.

Taifa Stars itashuka dimbani ikiwa na morali wa kuendelea kufanya vizuri kutokana na mwezi uliopita kuitoa timu ya Taifa ya Kenya, 'Harambee Stars' kwenye kinyang'anyiro cha kuwania kufuzu fainali za Wachezaji wa Ndani, CHAN.

Sasa Stars inasubiri kuvaana na Sudan na kama itaitoa itafuzu moja kwa moja kushiriki fainali hizo za CHAN zitakazofanyika mapema mwakani nchini Sudan. Na kama Stars itafuzu huu utakuwa mwaka wa mafanikio kwa Tanzania baada ya Juni mwaka huu kushiriki kwa mara ya kwanza fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) nchini Misri tangu 1980.

Hata hivyo, kwa michuano ya CHAN kama Stars itafuzu hii itakuwa mara ya pili kushiriki fainali hizo kwani ilishiriki kinyang'anyiro hicho mara ya kwanza ilipoanzishwa mwaka 2009.

Hivyo, wakati huu Stars ikielekea kuivaa Burundi, inapaswa kupigana kufa au kupona ili kumaliza kazi kwenye mechi hiyo ya kwanza ugenini na isisubiri kukutana na presha ya mchezo wa marudiano kama ilivyokuwa dhidi ya Harambee Stars kuwania kufuzu CHAN.

Tunasema hivyo kutokana na mechi ya kwanza Uwanja wa Taifa dhidi ya Harambee Stars, Taifa Stars ililazimishwa sare kabla na yenyewe kwenda kulazimisha sare ugenini nchini kwao na kuwatoa Wakenya hao kwa changamoto ya mikwaju ya penalti.

Hivyo, Taifa Stars haina budi kutambua biashara ni asubuhi na inapaswa kumaliza kazi mapema na kutosubiri kutegemea kushinda nyumbani wakati wa mechi ya marudiano Septemba 8, mwaka huu Uwanja wa Taifa.

Ushindi katika mechi hiyo ya ugenini itaifanya Stars kucheza kwa kujiamini zaidi katika mechi ya marudiano nyumbani huku presha ikiwa kwa Burundi ambayo itakuwa ikihitaji kupindua matokeo.

Tunatambua kikosi kilichoitoa Harambee Stars CHAN kitakuwa kimeongezewa nguvu kubwa kutoka kwa wachezaji wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi akiwamo nahodha wa timu hiyo, Mbwana Samatta, anayekipiga KRC Genk ya Ubelgiji.

Kwa mantiki hiyo Kaimu Kocha Mkuu, Mrundi Etienne Ndayiragije keshokutwa, Jumatano atakuwa na uwanja mpana zaidi wa kupanga kikosi kitakachompa matokeo chanya kwa kuwa silaha zake zimeongezeka.

Aidha, uwapo wa Ndayiragije unatupa matumaini zaidi ya kufanya vizuri katika mechi hiyo kwani atakuwa anayaelewa vema mazingira na falsafa za soka la kwao Burundi.

Lakini pia Ndayiragije atataka kushinda mchezo huo ili kulionyesha Shirikisho la Soka la Burundi, kuwa limefanya makosa kwa kutompa nafasi ya kukinoa kikosi hicho cha timu yao ya Taifa, hivyo ushindi si faida tu kwa Stars bali pia kwa kuongeza wasifu wa kocha huyo.

Kwetu sisi Nipashe tunaungana na Watanzania wengine kuiombea Stars ipate matokeo chanya ugenini kabla ya kurejea nyumbani kukamilisha tu ratiba katika mechi ya marudiano Jumapili ijayo.

Tunaitakia kila la heri katika mechi hiyo, lakini pia tukiwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kusafiri kuelekea Burundi kuishangilia Taifa Stars katika mchezo huo unaotarajiwa kuwa na ushindani mkali kwa pande zote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kocha wa makipa Simba ajitazame kwenye kioo

**NAKUMBUKA** baada ya Ligi Kuu kumalizika nilisoma mahali jinsi Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems alivyokuwa akitoa tathmini yake kwenye kikosi chake, benchi la ufundi, pamoja na ushauri jinsi gani ya kuboresha kwa ajili ya msimu huu.

Moja ya yale aliyosema ni kwamba alikuwa akichukizwa na makipa wake Aishi Manula na Deogratius Munishi 'Dida' kufungwa mabao ya aina moja.

Akiwa na maana kuwa makipa wake wanafungwa mabao yanayofanana. Aliyokuwa akifungwa Manula, siku akiwekwa Dida naye anafungwa kwa staili ile ile kama ya mwenzake.

Hilo lilionekana kumkera na kuahidi kulitafutia dawa ya kutafuta kocha wa makipa na aliyekuwapo aende kuongeza ujuzi.

Hata hivyo, msimu umeanza kocha wa makipa ni yule yule Muharami Mohamed, kipa mahiri wa zamani wa Simba, Pan Africa, Taifa Stars na pia amecheza soka la kulipwa nchini Msumbiji.

Ukiangalia mechi nyingi za msimu uliopita za Ligi Kuu, makipa wa Simba walikuwa wakifungwa mabao ya mbali na krosi.

Mastraika wanaopiga mipira kuanzia mita 20 kurudi nyuma wakiwa na asilimia kubwa ya kuwafunga kama mpira hiyo italenga goli. Hii iliwaweka roho juu wanachama na mashabiki wa Simba wanapoangalia mechi zao.

Lakini hata wachezaji waliokuwa wakicheza na Simba walionekana mkazo wao zaidi ni kupiga mashuti ya mbali. Na kuna wakati walifanikiwa.

Wanachama na mashabiki walipiga kelele sana juu ya makipa wa Simba kufungwa mabao ya aina hiyo. Msimu huu Simba imemsajili mmoja wa makipa wazuri kabisa nchini, Beno Kakolanya.

Hakuna shabiki yeyote yule nchini ambaye hajui umahiri wa Kakolanya. Kwenye mechi dhidi ya Azam katika namna ya kushangaza, naye alifungwa mabao mawili ya mbali kama yale yale ambayo Manula amekuwa akifungwa.

Alhamisi iliyopita, Manula alifungwa bao la takriban mita 24 kwenye mechi dhidi ya JKT Tanzania. Licha ya kushinda mabao 3-1, lakini bao hilo lilizua mjadala mkubwa mitaani na kwenye mitandao ya kijamii.

Sidhani kama inahitaji mjadala, badala yake imeshazoeleka kuwa makipa wa Simba wamekuwa na tatizo hilo.

Hata kama akitoka kwenye timu nyingine akiwa hafungwi mabao ya mbali, lakini anapoingia kwenye klabu hiyo naye anakuwa kama ameambukizwa tatizo hilo hilo.

Klabu ya Simba inaonekana kusajili makipa ikitegemea kutibu baadhi ya mapungufu walionayo makipa wao, lakini kipa anayesajiliwa naye anakuja kuwa na mapungufu yale yale ya wenzake.

Kwa maana hiyo tatizo halitokuwa la makipa hao. Lipo kwenye benchi la ufundi na hasa kocha wa makipa. Ilitegemewa baada ya ligi kumalizika, msimu huu kocha wa makipa angekuwa na mbinu mbadala, au kuwa ameshapata mwarobaini wa hilo, lakini kwenye mechi za awali tu imeonekana kuwa tatizo hilo bado liko pale pale.

Manula na Kakolanya ni makipa wakubwa na tegemeo kwa nchi yetu kwa sasa. Kufungwa mabao ya mashuti ya mbali si aibu kwao tu, bali pia hata kwa kocha wao anayewafundisha.

Ni kwa sababu makipa hawa wote huko walikotoka, Yanga na Azam hawakuwa na matatizo hayo. Muharami anatakiwa aliangalie hili kwa sasa kwani bado wanachama na mashabiki wengi wanaona safu yao ya ulinzi ni tatizo. Lakini likishaonekana kuwa limetibika na makipa wake wakaendelea kutunguliwa na mashuti ya mbali, mjadala utahamia kwake.

## MJADALA & BARUA

# Kituo hiki cha daladala Basihaya kitupiwe jicho

***Mhariri,***

*NINALIPONGEZA sana gazeti lenu kwa kuandika habari ambazo zinagusa sana maisha ya wananchi, husussan kero mbalimbali zinazotokea katika jamii yetu hii ya Kitanzania.*

*Baada ya pongezi hizi, ninawasilisha kwako kero kubwa inayotusumbua watumiaji wengi wa barabara ya Bagamoyo.*

*Katika siku za karibuni, eneo la Boko Basihaya limekuwa likisababisha foleni, kutokana na kituo cha daladala.*

*Hali hiyo imekuwa ikisababisha magari yanayotoka Tegeta kukumbwa na foleni kuanzia Namanga au Nyaishozi.*

*Kwa magari yanayotoka Bunju na Mbweni kwenda Tegeta yamekuwa yakikwama kuanzia Chama, hivyo abiria kutumia muda mrefu kutokana na usumbufu huo.*

*Kimsingi, foleni hiyo inasababishwa na kituo cha daladala cha Basihaya kuwa katika eneo lisilofaa kabisa.*

*Ninasema hivyo kwa sababu kimeingia kabisa ndani ya barabara na kusababisha magari mengine kushindwa kupishana.*

*Hali hiyo ilichangiwa zaidi baada ya kuongezeka kwa idadi ya magari hususan mabasi makubwa ya mikoani yalipoanza kutumia njia hiyo kwenda mikoa ya Kanda ya Kaskazini.*

*Pia kituo hicho ni njia panda, kwa kuwa kuna barabara inayotokea Ununio na maeneo mengine ya Tegeta na nyingine inaingia eneo la chuo binafsi.*

*Ninaziomba mamlaka husika zifuatilie kero hii na kuitafutia ufumbuzi ili kuwapunguzia watumiaji wa barabara hiyo usumbufu wa kupoteza muda mrefu wa kukaa katika foleni.*

*Ushauri wangu ni kuwa kero hii inaweza kupatiwa ufumbuzi wa kudumu iwapo kituo cha daladala cha Basihaya kitaondolewa na kuwekwa eneo zuri ambalo ni rahisi magari kupishana bila ya usumbufu wowote.*

***Mkazi wa Basihaya,***
***Dar es Salaam***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Mpangilio wa michuano Ligi ya Mabingwa Afrika una walakini

**Na Michael Eneza**

**Kwa timu ambayo ilifika hatua ya robo fainali baada ya makundi mwaka jana, halafu ikajipanga kikamilifu na uwekezaji wa maana ukawekwa, ingepaswa wapenzi wa soka nchini waendelee kufuatilia inafanya vipi katika hatua nyingine, ila mpangilio wa mashindano hauko hivyo.**

HISTORIA iliandikwa kwa njia mbili tofauti jijini Dar es Salaam hivi majuzi wakati klabu bingwa nchini, Simba ya jijini Dar es Salaam ilipotoka sare ya bao 1-1 na UD Songo, klabu bingwa ya Msumbiji halafu matokeo kwa jumla yakaamuliwa kwa bao la ugenini.

Simba ilitolewa katika michuano hiyo ambayo ni mchujo tu kabla ya timu kupangwa katika makundi na mashindano kamili sasa kuanza, au kufanyika. Ni historia kutolewa katika ngazi hiyo, na pia madhara yake kwa watazamaji na mashabiki kote nchini, kwani ilileta taharuki ya aina yake, kutolewa ghafla tu.

Kwa timu ambayo ilifika hatua ya robo fainali baada ya makundi mwaka jana, halafu ikajipanga kikamilifu na uwekezaji wa maana ukawekwa, ingepaswa wapenzi wa soka nchini waendelee kufuatilia inafanya vipi katika hatua nyingine, ila mpangilio wa mashindano hauko hivyo.

Ni kama kuna mtoano kwa timu ambazo hazikufikia daraja la kuingia katika mashindano hayo, ambako mara nyingine (yaani katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya) wanapangwa wawili wawili wachujane. Katika hali kama hiyo suala linaeleweka kwani timu haikuwa imefuzu kwa mashindano, ni kama kutupa karata, au shilingi.

Lakini pale ambapo timu imefuzu kwa mashindano tena kwa kuchukua ubingwa, wafuatiliaji wa timu hiyo wana haki ya kuiangalia kwa mapana, waridhike na ilipofika kwa maana ya mashindano yenye mechi kadhaa au tuseme mechi nyingi. Klabu itoke katika mashindano kwa mtiririko wa matokeo halafu izidiwe eneo fulani, au iwazidi wengine kwa vipengele kama hivyo - bao la ugenini kwa mfano, n.k. Tatizo ni huku kubisha hodi katika mashindano na kuchupa, kwa kujilinganisha na timu moja tu katika michezo miwili, bila kushindana na wengine, kwani wataanza mashindano kamili baada ya mchujo.

Hapo kimsingi ndiyo kuna tatizo, kuwa kwa kanuni za UEFA (tofauti na CAF, Shirikisho la Afrika) Klabu ya Simba iliingia kana kwamba ni 'rank outsiders,' timu ya mbali inayotafuta njia ya kupenya katika mashindano hayo. Timu inapokuwa ya tano au ya sita kwenye Ligi Kuu England inaweza kupewa mshindani wa aina hiyo kwa mfano mshindi wa tatu au wa nne wa ligi ndogo kama Ubelgiji apatikane wa kuingia katika mashindano yenyewe.

Kwa utafutaji huo wa nafasi kwa kutupa karata na siyo kwamba ni timu ambayo tayari iko kwenye mashindano, ikishindwa matokeo ya jumla ya mechi hizo mbili ni sawa tu.

Ina maana kuwa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hadi timu ambayo ni bingwa au imefaulu moja kwa moja kuingia kwenye mashindano hayo, mpaka itoke kuna jasho linatoka, inacheza mechi nyingi tu. Inabidi kuanza na makundi halafu wapatikane washindi wawili (kulingana na idadi ya makundi na idadi ya timu zinazoingia robo fainali), na hapo chochote kinaweza kutokea. Mara nyingi baada ya makundi ni hatua ya mtoano, ambao kisaikolojia ni mechi moja na marudio yake (kama ilivyokuwa katika mechi hii ya mzunguko wa awali). Hata ikitolewa katika ngazi hiyo mashabiki wanaridhika, walishaiona kwa undani, uwezo wake hadi makundi yakaisha, halafu hatua inayofuata ni kama kutupa karata, bahati.

Inavyoonekana ni kuwa CAF kwa uzembe wa kimkakati wanafanya kinyume cha mpangilio huo, kuwa wanafanya kwanza mchujo, halafu makundi, halafu waingie hatua ya mwisho. Kwa vile robo fainali huwa ni timu nane, ndizo zinatakiwa zipatikane katika makundi, na kama ni 16 bado kuna hatua ya mtoano ili zibaki nane ziingie katika hatua za mwisho. Mchujo awali hufanya timu iwepo mashindano kwa mdomo tu; katika hali halisi ni kuondolewa kabla mashindano halisi hayajaanza.

Ndiyo maana CAF wanatakiwa wabadili mtindo wa mashindano hayo ili timu zote zenye haki ya kucheza mashindano na siyo kwa mchujo maalum ili kuingia (kama upo) zicheze mechi na mizunguko ya mechi ya kuridhisha, kabla ya kuaga mashindano. Ina maana hatua ya makundi ndiyo ije mwanzoni, kwa mfano makundi ya kanda au makundi yoyote kama CAF ilivyozoea. Halafu kuwe na mzunguko mwingine wa kupata timu za kukamilisha fainali zenyewe, kwa mfano kati ya timu 70 za mzunguko wa kwanza zibaki 24, au pungufu. Hata ingekuwa mchuano ni makundi ya kanda kupunguza umbali wa safari siyo taabu, yakamilishe ushindani zitoke timu nane kati ya 20 kwa mfano, na hapo hapatakuwa na taharuki tena. Ni njia ya kuheshimu kila nchi inayoshiriki, ione uwezo wa timu yake bingwa, siyo dhi-

**KABWELA** NA FADHIL MOHAMMED



# Rais Museveni kuzindua kongamano la biashara Dar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amemwalika Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, kuzindua kongamano la kwanza la biashara kati ya Tanzania na Uganda linalotarajiwa kufanyika Septemba 6-7 mwaka huu katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari na kuwaeleza kuwa Rais Museveni ataambatana na wafanayabiashara kutoka nchini kwake ili kukutana na wafanyabiashara wa Tanzania.

Bashungwa alieleza kuwa lengo la kongamano hilo ni kutangaza fursa na kuhamasisha biashara na uwekezaji zilizoko Tanzania na Uganda. Pia Serikali itapata fursa ya kuzungumza na wafanyabiashara hao ili kuangalia changamoto za kufanya biashara katika nchi hizo mbili.

Alisema vilevile nchi hizo zitashirikiana kuzitatua, kuangalia fursa zilizopo, kuongeza biashara na kuhamasisha uwekezaji.

"Sisi Tanzania tumekuwa tunawauzia chakula na vifaa vya viwandani, kwa kuwa tunajenga uchumi wa viwanda ni fursa kwa Watanzania kushiriki kwenye kongamano hilo, ambalo litakuwa na tija kubwa kwetu kama nchi. Rais wetu analeta wakuu wa nchi mbalimbali ikiwamo Uganda ili kuwaonyesha fursa tulizonazo pamoja na kujenga mtandao mpana wa biashara," alisema Bashungwa.

Aliongeza kuwa kutakuwa na maonyesho ya bidhaa za Tanzania ambapo Watanzania watapata fursa ya kuonyesha bidhaa za kilimo na za viwandani, taasisi za umma na sekta binafsi zinazosaidia katika mnyororo wa thamani za biashara.

Ujio wa Rais Museveni pamoja na wafanyabiashara toka nchini humo itakuwa ni fursa ya kuunganisha wafanyabiashara wetu na wafanyabiashara wa Uganda kukuza wigo wa biashara, kupata masoko mapya pamoja na kutatua changamoto na kujenga mazingira mazuri zaidi ya kufanya biashara, kwa mujibu wa Bashungwa. Aliwahamasisha wazalishaji wa bidhaa za kilimo, wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda kutoka mikoa yote ya nchini kujitokeza kushiriki.



Wafanyakazi wa usafi wa mazingira katika Halmashauri ya Mji wa Masasi, mkoani Mtwara, wakizoa takataka na kupakia kwenye trekta kwenye dampo la eneo la Coca-Cola, stendi kuu ya mabasi wilayani Masasi, wikiendi. Dampo hilo, linalalamikiwa na wafanyabiashara walio jirani kwa mrundikano mkubwa wa takataka zinazotelekezwa kwa muda mrefu bila ya kuzolewa. **PICHA HAMISI NASIRI**

# Moro yasuasua utekelezaji REA

**Na Idda Mushi, MALINYI**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medark Kalemani, amesema mradi wa Umeme Vijijini (REA) kwa mkoa wa Morogoro umetekelezwa kwa asilimia 56.6, huku mikoa mingine ikiwa imetekelezwa kwa asilimia 70, hivyo kumtaka mkandarasi wake kutoa taarifa ya maandishi kwa kutotimiza ahadi ya asilimia 80.

Waziri Kalemani alisema hayo wakati akizungumza na wananchi wa vijiji vya Makanga na Idunda wilayani Ulanga mkoani Morogoro wakati akikagua na kufuatilia kazi za mradi wa REA.

Alisema serikali imetenga kiasi cha Sh. bilioni 42 kwa mkoa wa Morogoro ili kutekeleza Mradi wa REA, ambapo kwa mujibu wa mkataba kati ya serikali na mkandarasi aliyepewa kazi kwa mkoa wa Morogoro, anatakiwa hadi kufikia Desemba mwaka huu 2019 awe amemaliza kazi.

Aidha, alisema Wilaya ya Ulanga yenye vijiji 59 hadi kufikia Desemba watakuwa wamefikiwa na umeme na akatoa siku 20 kwa mkandarasi wa kampuni ya State Grid and Technical Works Limited inayosambaza umeme kuhakikisha inakamilisha umeme kwa vitongoji vya vijiji viwili vya Makanga na Idunda na kama atashindwa Mkuu wa Wilaya amkamate na kumpa taarifa.

Aidha, akawataka makandarasi wa mikoa yote nchini kuwatumia vijana wa maeneo inakopita miradi kwa kazi zinazojitokeza badala ya kuwatumia watu toka maeneo mengine nia ikiwa ni kuwapatia vijana ajira na kuondoa ulalamishi unaojitokeza maeneo mengi.

Aidha, Waziri Kalemani akamwagiza mkurugenzi wa miradi wa REA Taifa kumwondoa kwenye nafasi ya umeneja wa mkoa wa Morogoro, Seif Abdalah, kwa madai ya kushindwa kusimamia mradi huo kikamilifu.

## Shule zashauriwa kuweka vifaa vya zimamoto

**Na Mwandishi Wetu**

WAMILIKI wa shule nchini wameshauriwa kuweka mikakati ya kukabili majanga kwa kuweka vifaa vya kisasa vya kuzimia moto kwenye shule zao ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi wakati wote.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Shule ya St. Anne Marie Academy, Gladius Ndyetabura, kwenye mahafali ya wanafunzi 143 wa kidato cha nne, yaliyofanyika shuleni hapo.

Alisema shule yake imeweka vifaa maalum na vya kisasa kwa ajili ya kujilinda na majanga ya moto.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa shule hiyo iliyoko Mbezi kwa Msuguri jijini Dar es Salaam, Jasson Rweikiza, aliwashukuru na kuwapongeza wazazi wa wanafunzi wa shule hiyo.

Alisema ushirikiano mzuri wanaotoa umeisababishia shule hiyo kuendelea kufanya vizuri kitaaluma.

Aidha, aliwahakikishia wazazi hao kuwa wanaohitimu kidato cha nne mwaka huu watafanya vizuri kwenye mtihani yao kwani timu ya walimu wa shule hiyo wamefanyakazi ya kutosha kuwaandaa.

"Namshukuru mwalimu mkuu na timu yake kwa umahiri wanaoonyesha kuwaandaa vijana hawa," alisema.

## Kampuni zisizopeleka fedha ushirika kukiona

**Na Happy Severine, BARIADI**

MKUU wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, ametoa siku nne kwa kampuni zote zilizokopeshwa fedha benki kwa ajili ya kununua pamba ya wakulima zihakikishe zinapeleka fedha hizo kwenye vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) na iwapo zitashindwa kufanya hivyo atazianika hadharani kupitia vyombo vya habari.

Kiswaga alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kuongeza kuwa baadhi ya wanunuzi wamekuwa na tabia kuchelewa kupeleka fedha hizo licha ya kuwa wamekopeshwa na benki kwa ajili ya shughuli hiyo.

Alisema kampuni zinatakiwa kupeleka fedha hizo kwa wakati ili kuwanufaisha wakulima, hivyo ni vyema zikaacha tabia ya ucheleweshaji wa fedha kwani serikali imeamua kuwadhamini kwenye benki waweze kupata fedha kwa ajili ya kununulia pamba na si kwa ajili ya matumizi mengine.

"Natoa siku nne kwa kampuni ambazo zimekopeshwa fedha kupeleka fedha hizo haraka kwenye Amcos na iwapo zitashindwa kufanya hivyo, nitazianika hadharani na kuyachukulia hatua stahiki," aliongeza.

HABARI MIKOANI

# DC asisitiza mshikamano wa madiwani, watendaji

**Na Futuna Seleman,** RUFIJI

MKUU wa Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, Juma Njwayo, amelitaka Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya hiyo kuongeza mshikamano na ushirikiano kwa watendaji wa halmashauri hiyo, ili kuongeza mapato na kuijengea heshima wilaya hiyo.

"Sisi binadamu kila mtu ana mawazo yake unaweza kufikiri kama unapingwa kumbe ni mtazamo wako wewe... tunatofautiana kimtazamo tuvumiliane, rai yangu kwa pamoja na watendaji wetu tufanye kazi kwa bidii tuongeze mapato zaidi," alisema.

Hata hivyo, alipongeza ushirikiano uliopo na kusisitiza kuwa kwa vile halmashai hiyo imemaliza changamoto ya uwapo wa wakuu wa idara, sasa kazi ifanyike kwa pamoja ili kuleta matokeo chanya katika kusaidia maendeleo ya wananchi na kukuza uchumi wa wilaya, na vitengo vilivyobakia ambavyo havina wataalamu wanaotakiwa suala hilo linaendelea kufanyiwa kazi.

"Endelezeni mshikamano na mimi kama sehemu ya serikali nitaendeleza mshikamano na umoja ndio nguzo ya mafanikio, kuna wakati mwenyekiti huyo anaomba msaada tunafanyaje halmashauri isife tukajitahidi," alisema na kuendelea:

"Tumesonga mbele na itawezekaje tu, kama hakuna ushirikiano changamoto haziwezi kutatuka, ushirikiano ni kati ya mambo yanayoweza kutufelisha...ushirikiano muhimu."

"Msiwekeane vinyongo kusameheana ndio ubinadamu, kipindi hiki cha fedha kilichoanza fanyeni kazi kwa pamoja," aliongeza Njwayo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Saidina Malenda, akifungua mkutano huo alisema katika kipindi cha Julai 2018/2019 Rufiji imetekeleza majukumu mbalimbali ikiwamo uboreshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya kikiwamo cha Nyaminywili kwa kujenga wodi ya kinamama.

"Kwa upande wa Hospitali ya Wilaya, uboreshaji umefanyika kwa kukarabati jengo kwa ajili ya duka la nje la dawa, na ujenzi huo unaendelea," alisema Malenda.

Kuhusu uboreshaji wa elimu ya msingi na sekondari ambapo wilaya hiyo ilipokea Sh. 243,753,461.67 kwa ajili ya shule 45 za msingi na Sh. 288,496,596 kwa shule tisa za sekondari, hivyo Sh. 532,250,057 kutumika katika gharama za matumizi ya shuleni ikiwamo kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum upande wa sekondari na ukarabati wa miundombinu ya shule.

Katika hatua nyingine baraza hilo lilimchagua Ali Mbwana Ndungutu kuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo kwa tiketi ya CCM baada ya kupata kura 10 na kumbwaga mwenzake, Hassan Mpota aliyepata kura sita dhidi ya kura 16 zilizopigwa na wajumbe wa baraza hilo.



Mchuuzi wa matikitimaji akikokota baiskeli iliyosheheni matunda hayo, wakati akisaka wateja katika eneo la Gerezani, Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam jana. Tikiti moja liliuzwa kwa bei ya 2,000/- hadi 5,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: JOHN BADI**

# Walimu watakiwa kupata elimu ya mikopo

**Na Mwandishi Wetu**

WALIMU wametakiwa kujifunza elimu ya kibenki ikiwamo mikopo, amana na huduma zingine zinazotolewa na benki mbalimbali ili iwasaidie kupania uwezo wao kiuchumi na kujenga tabia ya kujiwekea akiba.

Rai hiyo ilitolewa jana na Kaimu Katibu wa Chama cha walimu (CWT) mkoa wa Rukwa, Aurelia Mwanakulya, ambaye alikuwa mgeni rasmi alipokuwa akifungua warsha ya Siku ya Walimu ilioandaliwa na Benki ya NMB katika Mji wa Sumbawanga, mkoa wa Rukwa nakuhudhuriwa walimu wapatao 300.

"Mkijijengea tabia ya kujiwekea akiba na kutumia mikopo kwa busara hakika mtaweza kukidhi mahitaji yenu mbalimbali pindi yanapojitokeza," alisisitiza.

Kwa upande wa Benki ya NMB aliitaka taasisi hiyo ya kibenki kuzidi kubuni bidhaa zaidi, lakini pia kuhakikisha kuwa huduma hizo zinapatikana kwa unafuu, uharaka na ufanisi mkubwa.

"Ni lazima NMB ijue kuwa ushindani ni mkubwa katika sekta ya kifedha na ni wale tu watakaoweza kushindana na ubora unafuu na ufanisi ndio watakaodumu kwenye soko," alibainisha.

Kwa upande wake Meneja Mwandamizi NMB wa Amana za Wateja na Bima, Issac Mgawasa, alisema kwa sasa taasisi hiyo ya kifedha ina wateja zaidi ya milioni 3.2 kati ya hao milioni 2.5 wanatumia simu za mikononi kufanya miamala mbalimbali.

"Tuna imani kuwa miaka michache ijayo tutakuwa tunakuwa na jamii isiyotegemea matumizi ya fedha halisi," alisisitiza.

Nae Meneja NMB wa Biashara Kanda za Nyanda za Juu Kusini, Humphrey Kaaya, alisema kuwa taasisi hiyo itaanzisha programu ya matumizi bora ya mikopo kwa wateja wake.

Akifafanua, alisema kuwa programu hiyo itawanufaisha wateja wa NMB katika mikoa ya Rukwa, Mbeya, Iringa na Katavi.

Meneja wa NMB Tawi la Sumbawanga, Happiness Pimma, alisema kuwa benki hiyo ni ya pekee inayotoa mikopo mingi kwa watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ambapo wengi wao ni walimu wakiwa pia wamefaidika na mikopo .

Wakichangia walimu kwa nyakati tofauti waliishukuru kutoa mikopo bila urasimu, huku wakiitaka ianze kutoa elimu ya ujasiriamali ili waweze kunufaika na mikopo hiyo, huku wakisisitiza kuwa wengi wao hawana elimu hiyo.

# Jukumu la chakula shule kwa machifu

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

SERIKALI wilayani Kalambo mkoani Rukwa, imewataka watemi wa makabila ya Wafipa kuisimamia jamii mkoani humo, ili kuchangia chakula shuleni kuwawezesha wanafunzi waweze kula wanapokuwa shuleni.

Hatua hiyo pia itasaidia kuboresha afya zao, hivyo kukabiliana na tatizo la udumavu linalo ukabili mkoa huo.

Ushauri huo ulitolewa na Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Frank Sichalwe, alipomwakilisha Mkuu wa Wilaya hiyo, Julieth Binyura, katika sherehe za kumsimika mtemi wa himaya ya Mambwe Nkoswe, Sapwe Nkongasimfukwe, zilizofanyika katika kijiji cha Kalembe.

Alisema wakazi wa wilaya hiyo ni wazalishaji wakubwa wa vyakula vya aina mbalimbali, lakini wazazi wamekuwa ni wagumu kuchangia vyakula kwa ajili ya watoto wao ili wawe wanakula shule badala ya athiri masomo ya wanafunzi na afya zao.

Sichalwe alisema machifu ni miongoni mwa makundi muhimu yanayosikilizwa na jamii mkoani Rukwa, hivyo wana jukumu la kuhakikisha wanalichukua suala hilo kama ajenda kwao ili liweze kupata mafanikio kwa kuwa utafiti umeonyesha kuwa kitendo cha wanafunzi kula chakula shuleni kinachangia kupunguza utoro pamoja na kukabiliana na udumavu.

Kwa upande wake mwenyekiti wa kamati ya ufundi wa baraza la machifu wa makabila ya Wafipa inayoshughulika na kusimika machifu, Mtemi Malema Sinyangwe wa himaya ya Ilwa-Nkansi, alisema wao wana jukumu kubwa la kuisaidia serikali kukabiliana na changamoto zinazoikabili jamii.

Alisema suala la maadili kwa jamii limekuwa ni changamoto, na kwamba si kuachiwa serikali na viongozi wa madhehebu.

Alisema kwa kuwa serikali inawatambua na kufanya kazi nao, watahakikisha wanarejesha maadili mema kwa jamii ili ustaarabu na kuheshimiana kuimalike ili viongozi wa serikali wabaki na jukumu la kutekeleza miradi ya maendeleo kama inavyoonekana katika serikali ya awamu ya tano.

Naye Katibu wa baraza la machifu mkoani humo, Chelenganya Sikulumbwe, alisema kuwa mkoa wa Rukwa uliamua kuanzisha kituo cha utamaduni cha makabila ya Wafipa kilichopo Kijiji cha Milanzi, ambacho kitakuwa na jukumu la kuratibu zoezi la kusimika machifu hao ambao wataisaidia serikali kutatua changamoto zinazo ikabili jamii.

# Tuico yaita wafanyakazi kuwatetea

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara na Taasisi za Kifedha ( TUICO) kimewataka wadau kutoka taasisi hizo kujiunga na chama hicho, ili kujenga umoja na mshikamano wa wafanyakazi kutoka taasisi hizo katika kutetea maslahi ya wafanyakazi hao.

Mbali na kutetea maslahi, pia kinawawezesha kufunga mikataba bora sehemu za kazi ili kuboresha maisha ya wafanyakazi.

Akizungumza katika mkutano na wafanyakazi wa benki ya NMB Katibu Mkuu msaidizi wa chama hicho, Tamim Salehe, alisema ni muhimu kwa wanachama ndani ya chama hicho kuimarisha umoja na mshikamano na kulinda maslahi ya kila mfanyakazi sambamba na kuhamasisha utekelezaji wa wajibu wao wanapokuwa kazini.

"Chama hiki kimekuwa mtetezi mkubwa na wa kweli kwa wafanyakazi katika taasisi nyingi za viwanda, biashara na kifedha, tutawezesha mazungumzo na mwajiri ili kuboresha maslahi ya wafanyakazi wote," Salehe alisema.

Katibu huyo alisema chama hicho kinatarajia kurudi katika meza ya mazungumzo na mwajiri wa wafanyakazi hao (NMB ) ili kudumisha mahusiano bora kati ya wafanyakazi, mwajiri wao na serikali ili kuongeza ufanisi kwa wafanyakazi hao.

Akitaja malengo makuu ya chama hicho Katibu huyo alisema ni kumtetea mwanachama dhidi ya dhuluma, uonevu, ubaguzi na migogoro mbalimbali kati ya mwajiri na wafanyakazi.

Pia kushirikiana na mwajiri kuhakikisha kuwa makundi maalum ya wafanyakazi kama vile wajawazito, walemavu wa aina mbalimbali wanapata haki sawa katika mazingira salama.

"Kuna baadhi ya taasisi tumewezesha mfano wajawazito kuongezewa likizo kutoka siku 84 hadi siku 120 sasa hili si jambo dogo," Salehe alisema.

Kwa mujibu wa Katibu huyo, chama hicho kilianza tangu mwaka 1995 na kwa sasa kina wanachama wapatao 103,000 nchi nzima kutoka taasisi mbalimbali za kifedha, mifuko ya hifadhi ya jamii na viwandani.



Mlulu Khalfan Said (kulia), akipokea cheti cha darasa la VII, baada ya kuhitimu elimu ya msingi kutoka kwa Padri Jiso Vincent, wakati wa sherehe za mahafali ya saba Shule ya Carmel Convent, iliyoko wilayani Mkuranga, mkoa wa Pwani juzi. **PICHA: MPIGAPICA WETU**

# Wananchi wajenga bweni la kisasa kwa nguvu zao

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

WAKAZI wa Kata ya Nangoo wilayani Masasi mkoani Mtwara wamekubaliana kuanza kujenga bweni la kisasa katika shule ya sekondari ya kata kwa nguvu zao wenyewe, ili kuiunga mkono serikali katika kutatua changamoto ya uhaba wa mabweni.

Aidha, wakazi hao wamesema watafanya kazi usiku na mchana hadi pale jengo hilo litakapokamilika kwa sababu hivi sasa wana uchungu na watoto wao kukosa bweni la kusomea.

Walifikia makubaliano hayo juzi wakati wa mkutano wa uzinduzi wa bweni hilo na kupokea mifuko 50 ya saruji yenye thamani ya zaidi ya Sh. 600,000 kutoka kwa diwani wao, Mohamedi Chilumba ambaye aliamua kuchangia saruji hiyo kwa ajili ya uhamasishaji wa ujenzi huo.

Liliani Milanzi, mkazi wa Nangoo alisema wao kama wazazi na walezi hawana pingamizi la kujitoa nguvu kazi zao kujenga bweni la wanafunzi kwani litasaidia kuwafanya wanafunzi hao kufanya mambo ambayo sio rafiki kwao hasa nyakati za usiku.

Alisema kukosekana kwa mabweni katika shule hiyo imekuwa ni moja ya sababu ambayo inawafanya baadhi ya wanafunzi kushindwa kusoma katika mazingira rafiki.

Naye Angelina Godfrey alisema watajitoa kwa nguvu zote kuhakikisha mabweni katika shule hiyo yanapatikana kwa kuwa ukosefu wa mabweni ni kikwazo kinachochangia wanafunzi hasa wa kike kushindwa kuendelea na masomo, lakini wakiwa na bweni watasoma katika mazingira bora.

Godfrey alisema changamoto hiyo ya ukosefu wa mabweni inasababisha hata baadhi kupata ujauzito.

Hassan Mkole alisema wazazi na walezi ndio wenye watoto wanaosoma kwenye shule hiyo, hivyo wana wajibu wa kuwa na hali ya kujitolea katika kufanikisha ujenzi huo kwa gharama yeyote kwani uwapo wa bweni kutasaidia kupunguza chagamoto nyingi kwa wanafunzi.

Diwani Chilumba alisema ametoa mifuko hiyo kama sehemu ya mifuko 100 ambayo awali aliahidi kuitoa kwa ajili ya ujenzi wa bweni hilo na kutatua changamoto zingine katika sekta ya elimu kwenye kata hiyo.

Alisema ameamua kuunga mkono jitihada za serikali katika kuhakikisha changamoto zilizopo kwenye sekta ya elimu kwenye kata hiyo zinakwisha hasa changamoto ya mabweni katika Shule ya Sekondari ya Nangoo.

## Mkombozi yamsaidia mwenye saratani ngozi

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara ya Mkombozi, imeahidi kuendelea kushiriki shughuli mbalimbali za kijamii kwa kuchangia watu wenye mahitaji maalumu.

Ilitoa ahadi hiyo baada ya uongozi wake kutoa msaada kwa familia ya Salim Rashid, mkazi wa Tuangoma jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kutembelea familia hiyo, Nwaka Mwabulambo Mkurugenzi wa Hazina wa Benki hiyo, alisema katika kuelekea miaka kumi ya benki hiyo, imeamua kushiriki na familia hiyo kwa kutoa msaada wa kuwafungulia akaunti ili jamii iweze kuwasaidia.

Alisema baada ya kupata taarifa kutoka katika vyombo mbalimbali kuhusu uhitaji wa Rashid ambaye anasumbuliwa na saratani uongozi wa benki uliamua kushiriki kwa vitendo kwa kuisaidia familia hiyo kwa kutoa mchango wa Sh. milioni moja sambamba na kufungua akaunti ya pamoja ili kuirahisishia familia hiyo kwenye zoezi la ukusanyaji wa fedha za msaada kutoka kwa jamii.

"Kama tunavyofahamu simu za mkononi zina ukomo wa utoaji fedha, hivyo benki kwa kuliona hilo tumeamua kuirahisishia jamii kazi hii kwa kufungua akaunti ya pamoja (Joint Akauti) ambayo itawezesha jamii na taasisi mbalimbali kuchangia kiasi chochote cha fedha ili kuirahisishia familia hii iweze kupata msaada wa fedha za matibabu," alisema Mwabulambo.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa kushiriki shughuli za kijamii, benki itaendelea kushirikiana na wadau wengine kuchangia shughuli mbalimbali za kijamii kama njia ya kutoa shukrani kwa kile wanachokipata kutoka kwa wateja wao ambao ndiyo wadau.

Aidha, aliongeza kuwa tayari uongozi wa benki umewashawishi watumishi wake kuona umuhimu wa kuchangia matibabu ya Rashidi huku ikiwataka Watanzania wengine kuona umuhimu wa kutoa michango kwa familia hii na zingine zenye mahitaji.

Aliitaja akaunti namba ambayo Watanzania wanaweza kutoa michango yao kwa familia hiyo kuwa ni 00420111912801 na kusema kuwa kufanya hivyo kutarahisisha matibabu ya Rashid ambaye tayari alishaanza matibabu hapa nchini na nje ya nchi.

# Tughe yawaangukia wakurugenzi

**Na Jaliwason Jasson, MANYARA**

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (Tughe) mkoani Manyara, kimemwomba Katibu Tawala wa Wilaya ya Babati, Halfan Matipula, kukisaidia kuzungumza na wakurugenzi wa halmashauri, kudhibiti vyama vingine kuchukua watumishi wanaostahili kuwa wanachama wao.

Wajumbe wa mkutano mkuu ambao walikutana kwenye kamati tendaji, walitoa ombi hilo kwa katibu tawala, ili kuwasaidia waepuke kukosa wanachama ambao ni wa kada ya afya.

Mwenyekiti wa Tughe mkoani Manyara, Honest Temba, alisema kumekuwapo na tabia ya chama cha watumishi wa Serikali za Mitaa (Talgw), kuwanyang'anya wanachama Tughe, kutokana na maofisa utumishi kuwa wao wako Talgw, lakini wana maslahi.

"Ila wanaosababisha sisi tugombanie wanachama ni wakurugenzi wa halmashauri na hiyo ni kwa kuwa wako Talgw, hivyo watumishi wapya wakija wanawalazimisha kujiunga huko maana wanakuwa hawajuwi," alisema Temba.

Alisema wafanyakazi hao wanapotezwa na vyama vyao ambavyo wanatakiwa kujiunga, ambapo wakipatwa na matatizo wanakimbilia Tughe na inakuwa vigumu kuwasaidia.

Mapema akisoma taarifa ya utekelezaji wa Tughe, Katibu wa chama hicho mkoani Manyara, Saburi Yakubu, alisema alipofika mkoani hapa, alikuta wanachama 1,110 ila mpaka sasa wameongezeka hadi kufika 1,800.

Yakubu alisema uhakiki wa vyeti vya wafanyakazi vimewapunguzia wanachama, suala la vifo vya watumishi na baadhi ya watumishi kujitoa uanachama.

Alisema kuna maombi 26 ya wanachama ambao wameomba kujiunga na chama hicho, ambacho kinawatetea watumishi wa umma huku akisema kuwa maofisa utumishi wengi, hawaelewi sheria na taratibu za vyama vya wafanyakazi.

Naye Katibu Tawala, Halfan Matipula, alisema kati ya vyama vya wafanyakazi ambavyo vimetulia ni Tughe, tofauti na vyama vingine, hivyo wa wasiogope changamoto na zisivuruge chama chao.

"Pamoja na kwamba chama kinafanya kazi ya kutetea watumishi, tufanye mambo yanayostaili na sisi ni vioo, hivyo tunapaswa kuishi kwa kujitambua na ndugu wa mtumishi ni mtumishi mwenyewe, kama kuna itilafu tuzimalize wenyewe," alieleza Matipula.

Vile vile ameridhia ombi lao la kuongea na wakurugenzi, ili wadhibiti kugombania wanachama ikitokea watumishi wapya waelekezwa mahali sahihi pa kujiunga na siyo kupendelea Talgw kwa kuwa wao wako huko.

"Tusitumie ugeni wa watumishi wapya kujinufaisha kupata mtaji wa wanachama, watumishi waachwe waende kwenye vyama sahihi na vyama hivi unapopata shida ndio unaona umuhimu wake, ila hamna haja ya kusubiri kupata shida," aliongeza.

Mwenyekiti wa Tughe wa Wilaya ya Simanjiro, Musa Mgogosi, aliwashauri wajumbe kutowategemea sana wakurugenzi katika kudhibiti suala la kupotosha watumishi vyama vya kujiunga vya wafanyakazi, maana wakurugenzi wako upande mwingine.

Mgogosi aliomba viongozi wa Tughe Taifa kuwatembelea wanachama wa mikoani ili wajue changamoto zao na kuzifanyia kazi, siyo kuwaachia viongozi wa mikoa na wilaya tu.



Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Arusha, Anastazia Tutuba (kulia), akipokea hotuba kutoka kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Odonyowas, Mwalimu Richard Mugabiso, baada ya kuisoma katika hafla ya kukabidhi majengo ya nyumba mbili za walimu na madarasa mawili na la utawala yaliyojengwa na Tasaf shuleni hapo, juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wazazi wachachamaa kisa wanafunzi kukosa chakula

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

WAZAZI wa watoto wa Shule ya Sekondari Oldonyowas Halmashauri ya Arusha, wameomba wazazi wenzao kutatua tatizo la ukosefu wa chakula cha mchana shuleni hapo, ili kuondoa changamoto ya baadhi ya wanafunzi kufeli sababu ya njaa.

Ombi hilo walitoa shuleni hapo wakati wa hafla fupi ya kukabidhiwa majengo ya shule hiyo na wadau waliofadhili ujenzi huo.

Mmoja wa wazazi hao, Anita Mushi, alisema utafiti unaoonyesha ukosefu wa mlo wa mchana shuleni kunachangia kwa kiasi kikubwa wanafunzi kutokuelewa walimu darasani, hali inayosababisha kufeli masomo.

"Naomba wazazi wenzangu tutafakari juu ya hili, kwani watoto wetu wanaposhinda njaa hata kumwelewa mwalimu ngumu na asipomwelewa, tusitegemee wafanye muujiza wa kufaulu masomo yao, tuchangie chakula ili wale shuleni," alisema.

Naye Kaimu Mkurugenzi, Halmashauri ya Arusha, Anastazia Tutuba, alishukuru wadau waliojenga baadhi ya majengo shuleni hapo na kuomba wazazi kujitafakari juu ya kuwapatia watoto wao chakula.

"Inasikitisha sana kusikia wanafunzi wanafika shuleni saa moja mpaka saa kumi jioni bila ya kula kitu chochote, huku wazazi wakipongezana kwa kuchanga fedha na kujenga shule, hili mliangalie ili watoto wetu waweze kuleta mageuzi katika masomo yao," alisema.

Alisema shule hiyo ni mpya, ina mandhari nzuri na mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia, endapo watoto hao watashinda njaa, wasitegemee ufaulu.

"Mtoto hawezi kufanya vizuri kwenye masomo akiwa na njaa, kwani mtu anaposoma ubongo unapoteza 'carolis' nyingi kuliko mtu anayelima, sasa ili nguvu mlizowekeza shuleni hapa ziweze kuzaa matunda bora kitaaluma, ni lazima muwape watoto hawa chakula cha mchana wawapo shuleni," alisema Kaimu mkurugenzi huyo.

Mkuu wa shule hiyo, Richard Mugabiso, akisoma risala fupi ya shule hiyo, iliyoanza Januari mwaka huu, alisema licha ya shule hiyo kujitosheleza kwa miundombinu na walimu, changamoto kubwa ni wanafunzi kutokupata chakula cha mchana wawapo shuleni, jambo linalotokana na wazazi kutokuchangia chakula hicho.

Alisema kutokana na hilo anakuwa na hofu na hali ya ufaulu wa wanafunzi hao wanaweza kushindwa kufanya vizuri kitaaluma, kutokana na wanafunzi hao kushinda njaa kutwa nzima na kuwataka wazazi kuliangalia na kulitafakari suala hilo upya.

Hata hivyo, mpango wa elimu bila malipo, unafafanua jukumu la wazazi ni kumpatia mtoto mahitaji yake binafisi ikiwamo chakula cha mchana kwa shule za kutwa, madaftari, nauli ya kwenda na kurudi shuleni.

Mwenyekiti wa kijiji cha Oldonyowas, Geofray Ayo, alisema, wazazi wanajitoa sana kuchangia maendeleo ya shule ikiwamo chakula cha watoto wao, lakini changamoto kubwa ni wazazi wa vijiji vya jirani, ambao hawachangii chakula jambo ambalo linasababisha kukosekana kwa chakula.

# Wajivunia mwanafunzi kushinda insha kitaifa

**Na Zanura Mollel, LONGIDO**

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Juma Mhina, amesema katika mashindano ya kuandika insha kitaifa, mshindi ni mwanafunzi wa kidato cha sita (CBN) Cynthia John Masuka kutoka Shule ya Sekondari Longido.

Alisema kuwa mwanafunzi huyo alipokea tuzo hiyo wakati wa mkutano wa wakuu wa nchi na serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

"Kwa zawadi zake, hakika Longido tupo vizuri," alieleza Mhina, na kupongeza jitihada za mwanafunzi huyo na walimu, kwa kuwa wanaipaisha Longido kujulikana zaidi.

Alisema hayo kwenye mahafali ya 15 ya Shule ya Msingi Sinya na kueleza kuwa hali ya elimu kwa sasa wilayani hapa ni nzuri tofauti na miaka ya nyuma.

Alisema matokeo ya mtihani wa darasa la saba kiwilaya ufaulu ni asilimia 83.6, huku kitaifa kiwango cha ufaulu ikiwa ni asilimia 80.

"Sisi tumevuka hadi malengo ya kitaifa na shule inayofanya vizuri na kuongoza kwa miaka 10 mfululuzi ni shule ya Sinya... yote haya ni juhudi za walimu na serikali kwa kujenga mazingira rafiki kati ya walimu na mwanafunzi," alisema Mhina.

Alifafanua kuwa Wilaya ya Longido ilikuwa na shule moja ya msingi iliyokuwa ikishika nafasi ya mwisho kitaifa ambayo ni Ilorienito, ila kwa sasa wamejitahidi na shule hiyo haipo tena katika nafasi 10 za mwisho, huku akieleza kuwa Shule ya Sinya ina wanafunzi wengi kutoka nje ya wilaya kutokana na ufaulu mzuri.

Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Sinya, Herman Minja, alisema wanafunzi waliosajiliwa kufanya mtihani wa darasa la saba ni 85, lakini watakoafanya mtihani huo ni 84, kutokana na mmoja wao kufariki dunia.

Mwalimu wa Shule ya Sinya, Indiaeli Nanyaro, alisema, katika risala kuwa changamoto kubwa inayowakabili ni ukosefu wa uzio, kwani shule hiyo ni ya bweni na ipo katikati ya pori, hivyo wanaiomba serikali kuweza kuwasaidia kutatua changamoto hiyo.

"Changamoto zingine ni upungufu wa vyumba vya madarasa na ofisi, jiko, nyumba za walimu, tunakuomba Mkurugenzi Mhina utusaidie upatikanaji wa mashine ya kuchapisha mitihani shuleni hapa," alisema Nanyaro.

Naye Ofisa Elimu Msingi Wilaya, Natang'adwaki Mollel, alikemea suala la utoro na kueleza kuwa endapo atabainika mzazi anayemkataza mtoto kwenda shule, hatua kali za kisheria dhidi yake zitachukuliwa.

# Mvua zakwamisha matumaini ya mazao

**Na Godfrey Mushi, HAI**

WANANCHI wa Hai, mkoani Kilimanjaro, wameingia hofu kutokana na kuwapo kwa mavuno kidogo ya mazao ya chakula msimu huu.

Mazao hayo ni mahindi na maharage ambayo kutokana na kukosekana na mvua za kutosha katika msimu wa 2018/19 hayakupatikana kwa wingi kama ilivyotarajiwa.

Kwa nyakati tofauti, wakulima wa vijiji vya Kware, Kwa Sadala, Msufini, Lambo Estates na Kijiji cha Mnadani, wameeleza hofu hiyo kwamba inatokana na kupatikana kwa mvua kidogo za masika hali iliyosababisha mahindi na maharage kupatikana tofauti na malengo yao.

Mkazi wa Kijiji cha Mnadani, Isaac Urio, alisema hawana matumaini ya kutosha na mavuno yaliyopatikana msimu huu, na kwa hali hiyo huenda bei ya vyakula sokoni ikapanda kuanzia mwishoni mwa mwaka huu au mwanzoni mwa mwezi Januari mwaka ujao.

Naye, Hellena Mwacha, mkazi wa Kijiji cha Kwa Sadala alisema mpaka sasa wakulima wengi hawana uhakika wa kuvuna mazao yao kwa sababu ya uhaba wa mvua katika baadhi ya vijiji hasa ukanda wa chini wa tambarare wa Wilaya ya Hai.

Kutokana na hofu hiyo, juzi Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Helga Mchomvu (Chadema) pia alieleza hofu hiyo akisema hali sio nzuri kimavuno na kwamba iko haja ya wananchi wa Hai kuchukua tahadhari.

"Kwa ujumla hali ya chakula katika maeneo yetu mengi ni changamoto na sababu ni kwamba mvua za masika zilizonyesha msimu huu wa 2018/2019 ni chache, hivyo malengo ya upatikanaji wa chakula tuliyojiwekea yatashuka sana," alisema Helga.

Diwani wa Kata ya Machame Magharibi (CCM), Martin Munisi, alitahadharisha kutokea kwa njaa, kama wananchi wa Hai hawatatunza chakula kidogo kinachovunwa hivi sasa.

"Ni lazima wananchi wajiandae kwa kulima mazao ya muda mfupi na hasa wale wa milimani wanapaswa kutumia vizuri mvua za vuli zinazotarajiwa kuanza hivi karibuni, wakulima wa ukanda wa tambarare wao mazao yao katika msimu wa masika uliopita yamekataa kutokana na mvua kutokunyesha za kutosha na kusababisha mavuno kuwa hafifu," alieleza Munisi. Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Kia (CCM), Yohana Laizer, alishauri kabla ya kufikiria aina ya mazao ya muda mfupi na yanayostahimili ukame kuhamasishwa kulimwa msimu ujao wa vuli, ni vizuri wananchi wa Hai wakafanya jitihada za kutumia mito na mifereji kujishughulisha pia na kilimo cha umwagiliaji.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Hai, David Lekey, alisema serikali iliweka malengo kwa msimu wa 2018/19 hasa mahindi kupanda hekta 21,060 na mavuno yangekuwa tani 52,650.

Mwezi Julai mwaka huu, Wizara ya Kilimo ilitoa tathmini ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa misimu miwili mfululizo inayoonyesha dalili za upungufu wa chakula katika mikoa 13 na halmashauri 46.

Tathmini hiyo ya mwaka 2018/19 na 2019/20 ilifanywa na Wizara ya Kilimo Mei na Juni, huku ikionyesha wilaya za Mwanga, Same, Siha na Hai (Kilimanjaro) kuwa miongoni mwa zitakazoathirika.

## Mhandisi afichua kutolipwa ujenzi hospitali

**Na Mwandishi Wetu, ROMBO**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, kimepokea taarifa kutoka Wilaya ya Rombo ya malalamiko ya mkandarasi anayejenga hospitali ya wilaya hiyo, kutolipwa fedha zake na kusababisha mradi kushindwa kukamilika kwa wakati.

Mradi huo wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Rombo, unahusisha majengo 22 yanayoigharimu serikali zaidi ya Sh. bilioni 7.5

Juzi, Mwenyekiti wa CCM mkoani Kilimanjaro, Patrick Boisafi na timu ya wataalamu waliotembelea mradi huo wa ujenzi, amekiri kuelezwa kuwa utekelezaji wake unasuasua kutokana na mkandarasi kukosa pesa za kununulia vifaa vya ujenzi pamoja na kuwalipa wafanyakazi.

Akizungumza baada ya kutembelea mradi huo unaotekelezwa na serikali ikiwa ni ukaguzi wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya Mwaka 2015/2020, Boisafi ameitaka Halmashauri ya Wilaya ya Rombo kuhakikisha inamlipa mkandarasi huyo kwa wakati ili aweze kukamilisha mradi huo.

Hata hivyo, Msimamizi mkuu wa mradi huo, Mhandisi Boniface Vedasto, alifichua siri hiyo, wakati akisoma taarifa ya mradi huo kwa Mwenyekiti huyo, alipoutembelea akiambatana na baadhi ya wataalamu na uongozi wa chama wa mkoa na wa Wilaya ya Rombo.

Hospitali ya wilaya hiyo inajengwa kwa fedha za serikali katika Kijiji cha Kiwanda, Kata ya Kirongo Samanga.

"Kimsingi ujenzi wenyewe ulianza Januari na ulitarajiwa ukamilike Julai 26, mwaka huu, kwa hiyo hatujaweza kufikia lengo," alisema Vedasto.

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, ilishapokea Sh. bilioni 1.5 ili kuanza utekelezaji wa ujenzi wa majengo sita, kati ya 22.

Majengo hayo na miundombinu yake ni pamoja na jengo la utawala, jengo la kufulia, stoo ya dawa, jengo la wagonjwa wa nje, maabara na mionzi na jengo la wazazi.



Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini nchini (Femata), John Bina, akizungumza kwenye mkutano wa sita wa Femata, uliofanyika jijini Tanga juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# DC Siha ataka wazazi kuchangia chakula shuleni

**Na Mwandishi Wetu, SIHA**

MKUU wa Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Onesmo Buswelu, ametoa wito kwa wazazi ambao hawataki kuchanga fedha au chakula shuleni, kwenda katika shule wanazosoma watoto wao nyakati za mchana kushuhudia wanavyopata madhila ya njaa.

Buswelu alitoa wito huo mwishoni mwa wiki akiwa katika Shule ya Sekondari Nuru, baada ya kuelezwa kwamba kuna mwanafunzi (jina limehifadhiwa), alizimia shuleni kutokana na njaa.

"Mimi nadhani kama ikiwezekana, wazazi au walezi waje kutembelea shuleni wakati wa chakula cha mchana ili kujionea adha wanayokumbana nao wanafunzi ambao wazazi wao hawajalipa michango ya chakula. Kumnyima mwanafunzi chakula ni kinyume na haki za binadamu, watu wameweka mbele kipaumbele cha kuchangia harusi au sherehe, badala ya kuwekeza katika elimu. "Hatutakubaliana na jambo hili hata kidogo, ni wajibu wa mzazi kumpatia mwanawe chakula ili kupunguza utoro na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi," alisisitiza Buswelu.

Mkuu huyo wa wilaya, alipewa taarifa kuhusu tukio hilo na Mwenyekiti wa shule hiyo, Wiliam Mollel.

Alielezwa kuwa mwalimu alihisi mwanafunzi huyo hajala kitu na aliposhauri apewe chakula kilaini alizinduka na kupata nguvu na kugundua sio ugonjwa kama walivyodhani.

Changamoto ya kutokula kwa wanafunzi shuleni wakati wa mchana kunaathari kiwango cha ufaulu kwa kuwa wanafunzi wanashindwa kufuatilia masomo kutokana na njaa.

Pamoja na mambo mengine akiwa shuleni hapo, Mkuu huyo wa wilaya alifungua vyumba vipya viwili vya madarasa na kupokea wanafunzi 62 wa kidato cha tano kwa mwaka 2019.

NIPASHE JUMATATU SEPTEMBA 2, 2019
Nipashe

# Spotika



WACHEZAJI WALIOCHEZA NA RONALDO MIAKA 10 WALIPO UK.16&17



## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Man City, Sergio Aguero, amefunga mabao 99 kwenye Ligi Kuu England hadi sasa kwenye Uwanja wa Etihad. Ni Thierry Henry pekee katika Uwanja wa Highbury (mabao 114) na Wayne Rooney kwenye Uwanja wa Old Trafford (mabao 101) waliofunga mabao mengi zaidi yake kwenye uwanja mmoja katika historia ya Ligi Kuu England.

## NGUVU YA MANE...

Mshambuliaji wa Liverpool, Sadio Mane, akimiliki mpira dhidi ya beki wa Burnley kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Turf Moor na Liver kushinda 3-0 juzi. **HABARI UK. 29**




# VAN DIJK ALIVYOWAPIKU CR7, MESSI UEFA

**MONACO,** Ufaransa

ZAMA za Cristiano Ronaldo na Lionel Messi za kutawala tuzo za soka zinaendelea kusukumwa ukingoni.

**Mwaka huu, beki wa Liverpool na Uholanzi, Virgil van Dijk amewaangusha kwa kuinyakua tuzo ya mwanasoka bora wa mwaka wa kiume wa Ulaya.**

Van Dijk amenyakua tuzo ya mchezaji bora wa Bara la Ulaya kwa mwaka 2018/19 baada ya kuiongoza safu ya ulinzi ya Liverpool kuchukua Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Kama Luka Modric alivyofanikiwa kuwaoondoa Ronaldo na Messi katika udhibiti wa tuzo hiyo mwaka jana - Van Dijk amekuwa mtu wa pili kuwapiku nyota hao ambao wametamba kwa zaidi ya muongo mmoja uliopita.

Van Dijk amekuwa baraka kwa Liverpool tangu alipojiunga na klabu hiyo kutoka Southampton na amekuwa kiungo muhimu kuisaidia kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na pia kuisaidia kuwania taji la Ligi Kuu ya England dhidi ya Manchester City hadi mwisho.

Kabla, alikuwa hajawahi kutwaa tuzo kubwa yoyote. Lakini usiku wa Alhamisi alilala na tuzo mbili; mchezaji bora wa Ulaya na beki bora wa Ulaya.

Takwimu za michezo ya mwaka 2018-19 zinaonyesha kuwa Van Dijk aliiwakilisha klabu na taifa lake katika mechi 59. Alifunga mabao tisa na kusaidia ufungaji wa mabao manne. Pia alichezea Liverpool kwa dakika nyingi zaidi ya mchezaji mwingine yeyote (dakika 4,465).

Katika mashindano yote ameonyesha kwa zaidi ya asilimia 70 umuhimu wake kama beki.

Liverpool ilifungwa mabao machache (mabao 22) ikilinganishwa na klabu nyingine za Ligi Kuu ya England msimu uliopita na Van Dijk alichangia ufanisi huo kwa asilimia 76.3.

Ukimlinganisha Van Dijk na mabeki wengine wa ligi tano kubwa Ulaya, England, Hispania, Italia, Ujerumani na Ufaransa, mchezaji huyo aliongoza katika msimu wa 2018-19 kwa kuokoa na kukaba.

Na pia alikuwa beki ambaye ni ngumu mno kumpiga chenga ukiwa naye sambamba ikilinganishwa na mabeki wengine. Rekodi hizo ndizo zikamfanya kuwabwaga kirahisi zaidi Messi na Ronaldo, ambapo alishinda kura mara tatu yao zaidi.


Messi msimu uliopita aliifikisha Barcelona nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa na akaisaidia kubeba taji la Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, na pia kuibuka mfungaji bora wa ligi zote tano za Ulaya na mfungaji bora wa ligi hiyo. Pia alichaguliwa kuwa mshambuliaji bora wa michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu uliopita.

Kwa upande wake Ronaldo yeye aliwaongoza Ureno kutwaa taji la Ligi ya Mataifa ya Uefa, na pia kuiwezesha Juventus kutwaa taji la nane mfululizo la Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Mabao yake 21 kwenye ligi hiyo, yalimsaidia kuibuka kuwa mchezaji bora wa mwaka wa Serie A.

Pamoja na yote hayo Messi na Ronaldo hawakuweza kufua dafu mbele ya Van Dijk ambaye aliibeba tuzo hiyo mbele yao.

**JE, WAJUA?**



Kurt Zouma ni mchezaji wa kwanza Chelsea kujifunga katika Uwanja wa Stamford Bridge kwenye mechi ya Ligi Kuu England tangu John Terry alipofanya hivyo Januari mwaka 2016 dhidi ya Everton.

# MICHEZO



Straika wa Yanga raia wa Namibia Sadney Ukhrob, akijaribu kutaka kuitoka ngome ya Ruvu Shooting kwenye mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania iliyopigwa Uwanja wa Uhuru wiki iliyopita.

# SABABU 5 YANGA KUPAPASWA NA RUVU SHOOTING

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza baada ya mechi 18 kupita, Yanga inapoteza mechi dhidi ya Ruvu Shooting ni baada ya Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Uhuru, historia kuandikwa kufuatia kuchapwa bao 1-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Ilikuwa ni mechi ya kwanza ya msimu kwa timu zote mbili, huku ikiwa ni ya 19 kwa timu hizo, Yanga ikiwa imeshinda mara 15, sare tatu, huku Ruvu Shooting ikishinda mara moja.**

Timu hiyo yenye maskani yake Mlandizi mkoani Pwani, imekuwa mteja mzuri wa Yanga kwa misimu mingi, lakini msimu huu imekataa katakata, hivyo kuzua hofu kwa wanachama na mashabiki wao.

Kuna sababu mbalimbali zilizosababishwa Yanga kufungwa na kibonde wake wa kudumu kwenye mechi hiyo. Hizi ni sababu tano kwa mujibu wa mwandishi wa makala haya...

**1. KUCHEZESHWA WAGENI WENGI**

Katika mechi hiyo, Yanga ilichezesha wachezaji wengi wageni kitu ambacho kilisababisha wao wenyewe kutokuwa na maelewano. Yanga ilianza na wachezaji watatu tu ambao walikuwamo kwenye kikosi msimu uliopita, lakini waliobaki walikuwa wapya kwenye kikosi hicho.

Wachezaji wa zamani ni Feisal Salum, Kelvin Yondani na Papy Tshishimbi. Pamoja na baadhi ya wachezaji wa zamani kuingizwa kipindi cha pili, akiwamo Mrisho Ngassa, lakini idadi kubwa ya wachezaji ilikuwa wapya kuanzia kipa Farouk Shikalo, David Molinga, Patrick Sibomana, Ally Mtoni.

**2. KUCHEZA STAILI YA AINA MOJA**

Kwa kiasi fulani Yanga imebadilisha aina ya uchezaji wake na hii inaweza kuwapa tabu mbele ya safari. Asili ya soka la Yanga ni mipira mirefu, lakini pia kutumia zaidi mawinga wenye kasi, wajanja na wepesi wa kupiga krosi.

Kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting, Yanga ilikuwa ikitumia zaidi mipira mirefu ili ianguke nyuma ya mabeki wa timu pinzani na mastraika wake wakafunge. Hata hivyo, mbinu hiyo ilionekana imeng'amuliwa na benchi la ufundi la Ruvu, kwani mabeki wa kati walikuwa wanahakikisha wanapiga vichwa mipira yote ya juu na kuwatibulia mahesabu mastraika wa Yanga.

Pamoja na kuonekana kuna ugumu, bado mabeki wa Yanga waliendelea kupiga mipira ya aina hiyo hiyo licha ya mpango namba moja kufeli.

**3. PENGO LA MAKAMBO HALIJAZIBWA**

Kama kuna mchezaji ambaye Yanga inamkosa ni Heritier Makambo, Mkongomani aliyeisaidia sana msimu uliopita, hasa kwa uwezo wake wa kupachika mabao.

Nimesema kuwa staili wanayotumia Yanga ya mabeki kupiga mipira mirefu, imekuwa si hatari tena kwa sababu Makambo alijua vema jinsi ya kuipokea na kuwahadaa mabeki ili kufanya makosa.

Wakati ikipigwa, Makambo alikuwa na uwezo wa kuwalazimisha mabeki kufanya makosa na yeye kuchomoka na kwenda kufunga, tofauti na mastraika wa sasa wa Yanga ambao wamekuwa hawawasumbui mabeki, badala yake wanaachia huru na kupiga vichwa kirahisi.

**4. KIUNGO WA KUPIGA PASI ZA MWISHO**

Pamoja na kusajili viungo wengi washambuliaji akiwamo Mapinduzi Balama kutoka Alliance, mastraika wa Yanga wanaonekana kuhaha sana kutokana na kutopata huduma sahihi kutoka kwa viungo hao.

Staili ya mastraika wa sasa wa Yanga si kama ile ya Makambo. Hawa wanaonekana kutengeneza nafasi na kuwekewa mpira kwenye nafasi za kufunga.


Kama Mapinduzi akipata uzoefu anaweza kuifanya kazi hii vizuri kutokana na uwezo wake mkubwa wa kuchezea mpira, lakini mastraika wa Yanga wanaonekana ni wale ambao wanatakiwa watengenezewe ili wafunge. Hakuna kiungo yeyote wa Yanga ambaye amejitahidi kufanya hivyo.

**5. WACHEZAJI HAWAJAWA FITI KIMWILI**

Hata Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera amekiri kuwa wachezaji wake hawajawa fiti kimwili na hawana pumzi. Wamekuwa wakichoka kadri muda unavyozidi kusonga mbele ndiyo wanavyozidi kuchoka.

Soka la Yanga mara nyingi ni la kutumia zaidi nguvu, hivyo wachezaji wanahitaji wawe vizuri kwenye fiziki, lakini kwa sasa wachezaji hawajawa hivyo kwa asilimia mia moja.

NJE YA UWANJA



## Danso yamkuta ya Pogba

BEKI wa Southampton, Kevin Danso ni mchezaji wa kwanza kuweza kutoa pasi ya mwisho na kisha kutolewa nje kwa kadi nyekundu kwenye Ligi Kuu England tangu Paul Pogba alipokutwa na balaa kama hilo, Desemba mwaka 2017, katika mechi ya Man United dhidi ya Arsenal.

# WACHEZAJI WALIOCHEZA NA RONALDO MIAKA 10 WALIPO

**MADRID,** Hispania

CRISTIANO Ronaldo alianza kuichezea mechi ya mashindano Real Madrid miaka 10 iliyopita wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-2 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, dhidi ya Deportivo La Coruna.

**Mshambuliaji huyo wa Ureno alifikia hatua ya kuwa mchezaji ghali zaidi duniani wakati akijiunga na Madrid akitokea Manchester United kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 94.**

Akaenda kuwa mfungaji bora wa wakati wote wa klabu hiyo akishinda mataji 15, yakiwamo manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na mawili ya Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, kabla ya kuondoka kwenda Juventus mwaka 2018.

Kufikia kipindi hicho cha muongo mmoja tangu Ronaldo alipoanza kucheza hapo Real Madrid, tunaiangalia timu ya wachezaji aliocheza nao kwa kipindi cha miaka 10 walipo hivi sasa...

### GOLIKIPA: IKER CASILLAS

Alikuwa chaguo la kwanza kwenye jezi za Real Madrid na anachukuliwa kama mmoja wa makipa bora wa wakati wote, Casillas alimaliza kipindi chake cha miaka 25 kucheza hapo Santiago Bernabeu mwaka 2015 kwa kujiunga na Porto ya Ureno. Mkongwe huyo alikumbwa na matatizo ya mshtuko wa moyo wakati wa mazoezi Mei, mwaka huu na kulikuwa na shaka kama ataweza kurudi tena uwanjani.

### BEKI WA KULIA: ALVARO ARBELOA

Arbeloa alirudi Madrid kwa mara ya pili mwezi mmoja baada ya Ronaldo kujiunga nayo na kuwa beki aliyekuwa akicheza mara kwa mara kabla ya kujiunga na West Ham mwaka 2016. Beki huyo mshindi wa Kombe la Dunia alistaafu baada ya kucheza msimu mmoja pale West Ham. Kwa muda mfupi alikuwa kocha wa timu ya Mambo FC mwaka 2018.

### BEKI WA KATI: EZEQUIEL GARAY

Maisha ya Garay pale Real Madrid yalionekana yangeishia hapo na kwamba asingeondoka, lakini aliuzwa kwenda Benfica mwaka 2011. Alihamia Zenit St Petersburg miaka mitatu baadaye na sasa amerudi kwenye soka la Hispania akiichezea Valencia, ambako amekuwa kwenye kikosi cha kwanza kwa misimu yote mitatu iliyopita.

### BEKI WA KATI: RAUL ALBIOL

Mchezaji mwingine aliyesajiliwa mwaka ambao Ronaldo alipowasili, Albiol alicheza mechi 43 katika mashindano yote wakati wa msimu wake wa kwanza. Aliondoka kwenda Napoli mwaka 2013 baada ya kukosa nafasi ya kucheza mara kwa mara, akicheza kwa misimu sita kabla ya kurudi tena Hispania kujiunga na Villarreal Julai mwaka huu.

### BEKI WA KUSHOTO: MARCELO

Mmoja kati ya wachezaji wawili tu ambao bado wanacheza Madrid ambao walicheza na Ronaldo, Marcelo sasa anaingia msimu wake wa 14 na klabu hiyo na amekuwa akicheza mara kwa mara. Licha ya kuhusishwa na mpango wa kutakiwa Juve mapema mwaka huu, Marcelo amebabakia Santiago Bernabeu na ameanza katika mechi zote msimu huu.

### KIUNGO WA KATI: LASSANA DIARRA

Diarra alianza vizuri zaidi hapo Los Blancos na baadaye alicheza mechi 17 wakati wakishinda taji msimu wa 2011-12, lakini Mfaransa huyo alihamia Anzhi Makhachkala mwaka 2012 baada ya kukosa namba. Baadaye akacheza pale Lokomotiv Moscow, Marseille na Al Jazira, kabla ya kuhamia Paris Saint-Germain Januari 2018. Alistaafu Februari, ingawa aliwahi kujiunga na klabu ya Ubelgiji, Sporting Charleroi ambako hakucheza mchezo hata mmoja.

### KIUNGO WA KATI: XABI ALONSO

Alonso alisajiliwa akitokea Liverpool na alikuwa mhimili wa kiungo wa Madrid kwa kipindi cha miaka mitano, akishinda mataji matano, likiwamo taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2014. Baadaye alichukuliwa na Pep Guardiola pale Bayern Munich. Kwa sasa amegeukia ukocha akifundisha klabu yake ya utoto ya Real Sociedad B.

### KIUNGO MSHAMBULIAJI: KAKA

Kaka aliwasili hapo Madrid Juni 2009 akiwa ameshinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'] mara moja na alikuwa mchezaji ghali zaidi kwa mwezi mmoja, kabla ya rekodi hiyo kuvunjwa na Ronaldo. Nyota huyo wa Brazil hakuwa na wakati mzuri chini ya Jose Mourinho na akarudi AC Milan miaka minne baadaye, huku ujio wa Gareth Bale ndio uliomlazimu aondoke. Alishindwa kufikia kiwango alichokuwa nacho kule San Siro na alikwenda kucheza kwenye Ligi Kuu ya Marekani, MLS, akiwa na Orlando City.

### MSHAMBULIAJI: CRISTIANO RONALDO

Ronaldo alianza kuichezea Madrid kwa kufunga penalti. Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or halafu akaongeza mabao mengine 450, na kuibuka kuwa mfungaji wa wakati wote wa Madrid. Kama kuondoka kwake kwenda Juve lilikuwa jambo la kushangaza, lakini kiwango chake kule kwa 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin kilikuwa bora. Alitwaa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Serie A katika msimu wake wa kwanza na kuiwezesha Juve kushinda taji lake la nane mfululizo la Ligi Kuu na yeye akifumania nyavu mara 21.

### MSHAMBULIAJI: RAUL

Alikuwa alama ya klabu Real Madrid wakati Ronaldo akiwasili hapo, akicheza naye kwa msimu mmoja. Ronaldo alipewa namba saba ya Raul wakati nyota huyo wa zamani wa Hispania alipohamia Schalke 04 mwaka 2010 na rekodi yake ya upachikaji mabao klabuni hapo ilizimwa na Ronaldo. Raul alitumia miaka mitano akicheza klabu tofauti za Schalke, Al Sadd na New York Cosmos kabla kuingia kwenye ukocha.

### MSHAMBULIAJI: KARIM BENZEMA

Mchezaji mwingine ambaye bado anacheza hapo Santiago Bernabeu akiwa amecheza na Ronaldo, Benzema ambaye amebakia hapo 'Los Blancos' kama mshambuliaji tegemeo. Mfaransa huyo alijiunga katika klabu hiyo mwaka mmoja na Ronaldo na walitengeneza upatina mzuri kwenye safu ya ushambuliaji. Anashika nafasi ya sita katika orodha ya wachezaji wanaongoza kwenye kufunga mabao wa wakati wote klabuni hapo, akiwa ametikisa nyavu mara 224, lakini bado ana safari ndefu ya kufikia rekodi ya Ronaldo.

### BENCHI: ESTEBAN GRANERO

Granero alikuwa na wakati mzuri Madrid na alirudi mwaka 2009 baada ya kucheza kwa majirani wao Getafe. Hakuwahi kuwa chaguo la kwanza na sasa anacheza pale Espanyol, akiwa pia amewahi kucheza QPR na Real Sociedad.

### BENCHI: GONZALO HIGUAIN

Mshambuliaji wa Argentina alicheza vizuri Madrid na Napoli kati ya mwaka 2007 na 2016, kabla ya kuhamia Napoli na Juventus. Baada ya kutokuwa na msimu mzuri kule AC Milan na Chelsea alikocheza kwa mkopo, amerudi tena Juve chini ya kocha Maurizio Sarri.

### BENCHI: GUTI

Guti alitumia miaka 15 akiwa hapo Madrid na alitajwa kama mmoja wa wachezaji wenye vipaji vya ukweli kutoka kwenye akademi ya Real Madrid. Aliondoka mwaka 2010 na alicheza mwaka wake wa mwisho pale Besiktas na sasa yupo kwenye benchi la ukocha.



CASILLAS

## Nukuu

"Uingereza kwa sasa ipo imara. Tuna matumaini timu za Uingereza zitaendelea kutawala, lakini kwa upande wa Chelsea kuna tatizo kidogo na itakuwa changamoto kubwa zaidi kwetu. Tunajua kwamba changamoto ya kufungiwa ni ngumu kwetu na hatuna cha kufanya, maana usajili tumeshindwa kufanya, hivyo, tunaweza tusiwe imara zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa, maana changamoto ni kubwa zaidi kwa upande wetu," **Kocha wa Chelsea, Frank Lampard akizungumzia michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya droo ya makundi kufanyika.**



"Mara zote nasema kamwe usiseme kamwe. Pengine mwezi mmoja au miwili nitakuwa na hisia za ajabu kwamba nimekikosa kitu nilichokuwa nakipenda na nitaamua kurudi tena, lakini bila shaka haiwezi kuwa rahisi hivyo kwa sababu umri unakufanya uchoke, ila siwezi kusema kwamba, sitakuwa na uwezekano wa kurudi uwanjani," **Arjen Robben alipoulizwa kuhusu uwezekano wa kurudi uwanjani baada ya kutangaza kutandika daluga.**



"Inaonekana hivyo. Nani anaweza kusema naweza kuendelea na miaka yote mitatu? Kama nikiamua mwenyewe, sitaweza kuendelea, nitachukua likizo na ninataka kuchukua maamuzi mazuri. Nina nguvu, lakini nina tatizo moja: Siwezi kuendelea kufanya kazi wakati nikitaka kupumzika, naamini baada ya mapumziko nitakuwa na nguvu zaidi na hapo nitaweza kufanya kazi nipendavyo," **Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, alipoulizwa kama atachukua mapumziko baada ya kumaliza mkataba wake.**



## Michezo




KAGERE

# USIYOYAJUA RAUNDI YA KWANZA LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20 umeanza kwenye viwanja mbalimbali nchini kwa ajili ya kusaka mfalme mpya wa soka.

**Matokeo ya raundi ya kwanza yalikuwa ni Mbao kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Alliance, Mbeya City na Prisons kutoshana nguvu kwa kumaliza dakika 90 bila kufungana, huku Namungo ikiikandamiza Ndanda FC mabao 2-1.**

Matokeo ya mechi zingine ni kwamba Polisi Tanzania iliifunga Coastal Union bao 1-0, Biashara United kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar, Mwadui kuidungua Singida United bao 1-0, Azam ikaichapa KMC bao 1-0, huku Lipuli ikitoa kipigo cha mabao 3-1 dhidi ya Mtibwa Sugar.

Wakati Yanga ikila kibano cha bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting, Simba ikaitandika JKT Tanzania mabao 3-1.

Mambo mbalimbali yamejitokeza kwenye mechi hizo, baadhi ya timu na wachezaji wakiweka rekodi mbalimbali kwenye mechi hizo za kwanza.

### 1. KAGERE AJA NA REKODI KIBAO

Straika hatari kwa sasa nchini Meddie Kagere ameweka rekodi mbalimbali kwenye Ligi Kuu siku ya kwanza tu akicheza mechi ya kwanza kwa timu yao dhidi ya JKT Tanzania.

Ameweka rekodi ya kufunga bao la mapema zaidi kwenye Ligi Kuu, akifunga dakika ya kwanza, Simba ikiifunga JKT Tanzania mabao 3-1.

Mabao mawili aliyofunga kwenye mechi hiyo iliyochezwa Alhamisi, yamemfanya kufikisha jumla ya mabao 25 ya Ligi Kuu, tangu ajiunge na klabu hiyo akitokea Gor Mahia msimu uliopita.

Ameweka rekodi nyingine ya kufunga mabao kwenye mechi za kwanza kwa misimu miwili mfululizo.

Msimu uliopita alifunga bao pekee kwenye mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Agosti 22, mwaka jana dhidi ya Prisons, Simba ikishinda bao 1-0.

Ndiye mchezaji pekee aliyefunga bao kwenye raundi ya kwanza msimu huu, kati ya wale waliofunga mechi za raundi ya kwanza msimu uliopita.

Wachezaji waliofunga mabao kwenye mechi za ufunguzi msimu uliopita na hawajarudia kufanya hivyo zaidi ya Kagere ni Vitalis Mayanga, Evergetus Mujahuki, Zawadi Mauya, George William, Omari Mponda, Salum Ayee, Erick Mbilizi, Heritier Makambo ambaye hayupo kwenye Ligi Kuu kwa sasa, Kelvin Yondani, Haruna Chanongo, Joseph Mahundi na Danny Lianga.

### 2. YANGA YACHAPWA BAADA YA MISIMU MINNE

Yanga imechapwa kwa mara ya kwanza kwenye mechi ya raundi ya kwanza baada ya msimu minne.

Kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting kimeifanya timu hiyo kupoteza mechi kwenye raundi ya kwanza tangu Ligi Kuu msimu wa 2014/15.

Mara ya mwisho kufungwa kwenye mechi yake ya kwanza kwenye Ligi Kuu ilikuwa ni Septemba 20, mwaka 2014 ilipochapwa mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro. Mabao hayo yalifungwa na Mussa Hassan Mgosi na Ame Ally.

Baada ya hapo Yanga haikuwahi kupoteza mechi kwenye raundi ya kwanza hadi ilipoteka Jumatano iliyopita.

### 3. RUVU YAIFUNGA YANGA BAADA YA MECHI 18

Kwa mara ya kwanza Ruvu Shooting imefanikiwa kuifunga Yanga baada ya michezo 18.

Katika michezo hiyo yote, Yanga imeshinda mara 15, sare tatu, na hii sasa ni mara ya 19 timu hizo zinapambana na hatimaye Ruvu inafanikiwa kupata ushindi wake wa kwanza Jumatano iliyopita kwa bao la dakika ya 20 lililofungwa na Sadat Mohamed.

### 4. MCHEZAJI MBAO AFUNGA BAO LA MSIMU

Paschal Liponda wa Mbao amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao kali msimu huu. Alifunga bao dakika ya 11 kwenye mechi dhidi ya Alliance na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1.

Mechi hiyo ilichezwa Agosti 24, siku ya ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mabao mengine ya mechi zote tano zilizochezwa siku hiyo, yalifungwa baada ya dakika 11, hivyo kuingia kwenye rekodi hiyo msimu huu. Hata yaliyofungwa nyuma ya dakika hizo ni mechi ambazo zilichezwa siku zilizofuata.

Msimu uliopita, Salum Aiyee wa Mwadui (kwa sasa KMC FC) alikuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao, akifanya hivyo dakika ya tisa kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar, ingawa timu yake ilipoteza mechi hiyo kwa kufunga mabao 2-1.

### 5. MAGOLI 19 YAVUNJA REKODI

Mabao 19 yaliyofungwa raundi ya kwanza ya Ligi Kuu yamevunja rekodi ya msimu uliopita wa 2018/19. Msimu uliopita yalifungwa mabao 15, hivyo msimu huu kuna ongezeko la mabao matatu zaidi ya msimu uliopita.

Hata hivyo, kwa misimu yote miwili, kumekuwa na sare mbili tena zinazofanana mabao kwenye mechi za raundi ya kwanza.

Msimu huu sare ilikuwa ni ya bao 1-1 kati ya Mbao dhidi ya Alliance, na Mbeya City dhidi ya Prisons zikatoa sare ya bila mabao, wakati msimu uliopita Coastal Union ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Lipuli FC, na JKT Tanzania ilitoka suluhu dhidi ya KMC.

### 6. ZILIZOPANDA LIGI KUU ZOTE ZASHINDA

Namungo FC na Polisi Tanzania, timu ambazo zimepanda daraja na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu huu zimeshinda mechi zao za kwanza.

Namungo, ikiwa nyumbani Uwanja wa Majaliwa iliichapa Ndanda mabao 2-1, na JKT Tanzania ikashinda bao 1-0 dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

Msimu uliopita, kati ya timu nne ambazo zilipanda Ligi Kuu ni moja tu ambayo ilishinda kwenye mechi yao ya kwanza za Ligi Kuu.

Biashara ya Mara ndiyo ilikuwa timu pekee kushinda, ilipoichapa Singida tena ikiwa ugenini bao 1-0.

Timu zingine ambazo ni Alliance na African Lyon zilifungwa, huku KMC ikitoka sare.

**NAJUA WAJUA**



LIVERPOOL haijawahi kupoteza katika mechi yoyote kati ya 33 zilizopita za Ligi Kuu England ambazo Sadio Mane alicheka na nyavu (W29 D4 L0).




# MAKUNDI 7 YA KIFO MABINGWA ULAYA

Mabingwa wa Ulaya msimu uliopita, Liverpool.

**MONACO,** Ufaransa

KILA shabiki wa mpira wa miguu anapenda kuangalia wachezaji bora zaidi wakipambana dimbani. Lakini kwa klabu husika zinakuwa kwenye wakati mgumu zinapojikuta zimepangwa kwenye makundi yenye timu bora tupu katika mashindano mbalimbali.

**Na hivyo ndivyo inavyotokea kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, mashindano makubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani humo.**

Makundi kwa ajili ya michuano hiyo tayari yamepangwa, sasa hapa tunaangalia makundi ya kifo yaliyowahi kushuhudiwa katika historia ya mashindano hayo.

Makala haya yanachambua makundi saba ya kifo katika historia ya michuano hiyo tangu kuanzishwa kwake.

### 7. REAL MADRID, MILAN, AJAX NA AUXERRE (2010/11)

Cristiano Ronaldo, Kaka, Ronaldinho, Zlatan Ibrahimovic, Clarence Seedorf, Andrea Pirlo - kundi hili lilikuwa na magwiji hawa.

Zote Real Madrid - ambao walikuwa washindi wa kundi na Milan wana historia bora zaidi ya mashindano hayo ya Ulaya. Kwani klabu zote mbili kwa pamoja zimetwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara 20. Real ikitwaa mara 13 na Milan mara saba.

Milan walishinda taji la Ligi Kuu ya Italia mwaka 2011, Ajax wakazalisha nyota wa baadaye. Christian Eriksen ndio aliibuliwa akiwa na Ajax pamoja na Toby Alderweireld na Jan Vertonghen. Auxerre walifanikiwa kutinga hatua ya 16-bora. Barcelona ndio walitwaa ubingwa huo.

### 6. LIVERPOOL, CHELSEA, REAL BETIS NA ANDERLECHT (2005/06)

Sio Anderlecht wala Real Betis ambao walikuwa mabingwa wa ligi za nyumbani kwako, lakini Chelsea alikuwa bingwa wa EPL. Blues hao walitwaa ubingwa kwenye Ligi Kuu ya England wakipoteza mchezo mmoja tu.

Kikosi cha Jose Mourinho kiliingia kwenye michuano hiyo kikionekana kuwa na nguvu ya kuweza kuwanyang'anya ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Liverpool. Wekundu hao walitoka sare mchezo wa mwisho wa kundi pale Stamford Bridge na kuwawezesha kumaliza wakiwa washindi wa kundi. Barcelona walitwaa taji hilo.

### 5. BAYERN MUNICH, NAPOLI, MANCHESTER CITY NA VILLARREAL (2011/12)

Ulikuwa ni ubatizo wa moto kwa Manchester City na Napoli kwani walikuwa wanaanza kucheza mashindano hayo. Hakuna kati yao aliyekuwa anapenda kukutana na Bayern Munich na waliiona Villarreal kama ndio timu ya kuionea.

Napoli ilipambana na kuwa nafasi ya pili kwenye kundi baada ya mchezo wa mwisho kuifunga Man City mabao 2-1, yote yakifungwa na Edinson Cavani. Man City iliyokuwa chini ya kocha, Roberto Mancini ilifanikiwa kutwaa taji la ligi msimu huo. Chelsea waliibuka mabingwa.

### 4. BORUSSIA DORTMUND, ARSENAL, NAPOLI NA MARSEILLE 2013/14

Napoli hawajawahi kuwa na bahati ya kupangwa kundi rahisi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ikiwa ni mara yake ya tatu kucheza michuano hiyo, miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wakajikuta tena kwenye kundi gumu.

Pengine haikuwa mshangao wakati walipomaliza wakiwa na pointi 12 sawa na Arsenal na Borussia Dortmund. Lakini ilishindwa kufuzu hatua ya mtoano. Real Madrid walitwaa kombe.

### 3. TOTTENHAM, REAL MADRID, BORUSSIA DORTMUND NA APOEL NICOSIA (2017/18)

APOEL lazima walishangaa kwamba watakwenda kufanya nini kwenye soka baada ya kujikuta wamepangwa kundi moja na Dortmund, Real na Tottenham Hotspur.

Timu hiyo ilikuwa na wakati mgumu kukutana na timu kama Spurs iliyokuwa kwenye kiwango cha juu chini ya kocha, Mauricio Pochettino na Real Madrid bila shaba yoyote ilikuwa inajulikana kwamba ina kikosi bora.

Waliwashangaza wengi, baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 nyumbani kwa Real na pia kuwafunga Dortmund. Lakini Madrid wakalitwaa taji hilo kwa mara ya tatu mfululizo Mei 2018.

### 2. BORUSSIA DORTMUND, REAL MADRID, AJAX NA MANCHESTER CITY (2012/13)

Kundi hili lilishuhudia watawala wa soka la England, Uholanzi, Ujerumani na Hispania wakipangwa pamoja.

Jurgen Klopp akiwa na Dortmund alikuwa akitoka kushinda taji la Bundesliga mara mbili mfululizo, na hakuna aliyeshangaa ilipoibuka kuwa kinara wa kundi.

City walimaliza mkiani mwa kundi, huku Dortmund wakakutana na Real Madrid kwenye nusu fainali. Roberto Lewandowski alifunga mabao manne kwenye mchezo wa kwanza na kutinga fainali. Lakini walifungwa na Bayern Munich kwenye fainali kwa bao la Arjen Robben pale katika dimba Wembley.

### 1. BARCELONA, INTER, TOTTENHAM NA PSV EINDHOVEN (2018/19)

Baada ya kuwa na mbio za kufa au kupona kwenye Ligi Kuu ya England, Spurs wakajikuta wamefuzu tena kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. Lakini mwisho wa siku wakajikuta wakitinga fainali na kukutana na Liverpool ambao waliwashinda kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya England. Pamoja na kuwa na matumaini makubwa ya kulibeba taji hilo kwa mara ya kwanza, wakajikuta wakichezea kichapo kutoka kwa Liverpool kwenye fainali na kulitwaa taji hilo.

NDANI YA 18



Tammy Abraham ni Muingereza wa kwanza kufunga takriban mabao mawili mfululizo katika mechi za Ligi Kuu England alizoichezea Chelsea tangu Frank Lampard alipofanya hivyo Januari 2010.

Nipashe
# Spotika



CRISTIANO Ronaldo alianza kuichezea mechi ya mashindano Real Madrid miaka 10 iliyopita wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-2 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, dhidi ya Deportivo La Coruna.

Uk. 16&17

# NYAKATI TAMU ZA PIQUE AKITIMIZA YA 500 BARCA



Pique na mchumba wake, Shakira

**BARCELONA,** Hispania

GERARD Pique alifikisha mechi yake ya 500 kuichezea Barcelona wakati mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, walipocheza na Real Betis Jumapili ya Agosti 25, mwaka huu na kujikuta akiingia katika historia ya kuwa mmoja wa mabeki bora zaidi kuwahi kutokea katika historia ya klabu hiyo.

Beki bora wa wakati wote wa Barcelona, Pique anaburuzwa na Lionel Messi na Andres Iniesta wakati linapokuja suala la tuzo binafsi walizoshinda, na kumbukumbu inaonyesha kwamba ametwaa zaidi ya mataji 29 kwa kipindi chake chote cha uchezaji hadi sasa.

Lakini kumekuwa na mengi kwa Pique katika kipindi cha miaka 11 aliyokaa hapo kwenye dimba la Camp Nou ukiacha kubeba mataji, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, anafahamika kuwa ni mtu asiyependa kuzungumza na mwenye haiba ya utulivu.

Akiwa anasherehekea kipindi chake hicho, hapa tunaangalia nyakati bora zaidi kwake hapo Barcelona.

### KUANZA BILA KUFUNGWA

Pique aliongeza ukuta wa chuma kwenye safu ya ulinzi ya Barcelona wakati alipotua hapo akitokea Manchester United, huku mchezo wake wa kwanza kuichezea wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Wisla Krakow kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alianza kucheza mechi ya Ligi Kuu ya La Liga wakati Barca ikitoka sare ya 1-1 na Racing Santander kwenye dimba la Camp Nou Septemba 13, na 'Blaugrana' hao walianza kwa msimu bora wa kukumbukwa zaidi wa 2008-09.

### KUFUNGA ULAYA

Pique amefunga mabao katika kila msimu kati ya misimu 11 aliyoichezea Barcelona, na bao lake la kwanza alifunga dhidi ya Sporting Lisbon kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Baada ya Lionel Messi kuwaweka mbele Barcelona ugenini katika Uwanja wa Jose Alvalade, Pique alifunga bao la pili kwa Barca kwenye mchezo huo.

### BAO KWENYE CLASICO

Real Madrid walikuwa kwenye ubora wa juu wakati Barcelona ilipowasili kwenye Uwanja wa Bernabeu Mei mwaka 2009, huku miamba hao wa mji mkuu wa Hispania wakiwa wameshinda mechi 17 kati ya 18 zilizopita.

Lakini Blaugrana hao waliwaadabisha kwa kuwachapa mabao 6-2, huku Pique akifunga bao la mwisho. Hilo lilikuwa bao la kwanza la Pique la ligi kwa Barcelona.

### KULIPA KISASI

Pique aliachwa kwenye kikosi cha Manchester United wakati 'Mashetani Wekundu' hao wakishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2008, lakini mwaka mmoja baadaye akalipiza kisasi cha kuachwa.

Barcelona ilicheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya United mwaka 2009 kwenye Uwanja wa Olimpico na Pique alikuwa moyo wa safu ya ulinzi ya kocha, Pep Guardiola, huku mabao ya Lionel Messi na Samuel Eto'o yakiipa ubingwa miamba hao wa Camp Nou.

### SALUTI YA VIDOLE VITANO

Mashabiki wa Real Madrid bado wana hasira na Pique baada ya kuwaonyesha ishara ya vidole vitano (maarufu kama mkono) katika Uwanja wa Camp Nou Novemba mwaka 2010.

Baada ya Barcelona kuwafumua wapinzani wao hao mabao 5-0, Pique alionyesha ishara ya vidole vitano kwa mashabiki wa Real waliokuwa kwenye Uwanja wa Camp Nou, ishara ambayo ilipewa jina la 'manita' (ikiwa na maana mkono mdogo), na hadi leo mashabiki wa Madrid hawajawahi kumsamehe.

### MATAJI MATATU MARA MBILI

Baada ya msimu wa kwanza pale Barcelona kushuhudia akitwaa mataji matatu ya La Liga, Kombe la Mfalme [Copa del Rey] na Ligi ya Mabingwa Ulaya, Pique pengine alihofia kwamba asingefikia tena rekodi hiyo.

Lakini msimu wa 2014-15 Pique alijikuta akiiongoza Barcelona wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Juventus kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mjini Berlin nchini Ujerumani na kubeba kwa mara ya pili mataji matatu kwa msimu mmoja, La Liga, Copa del Rey na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### KURUDI OLD TRAFFORD

Pique alielezea kwamba dimba la Old Trafford kama "nyumba yake ya pili" wakati Barcelona ilipopangwa na Manchester United kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na alibainisha hisia zake za kurudi tena kwenye uwanja huo.

Pique aliisaidia Barca kuibuka na ushindi wa 1-0 na wakashinda mabao 3-0 kwenye mchezo wa pili katika dimba la Camp Nou, na United walijikuta wakijuta kumuachia aondoke kwa euro milioni tano Agosti mwaka 2008.

### URAIS BARCA

Januari 2018, Pique alisaini mkataba wa kuendelea kumuweka hapo Camp Nou hadi mwaka 2022, huku kukiwa na kipengele cha kumuuza kwa euro milioni 500.

Mkataba huo unatarajiwa kuwa wa mwisho kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 na Rais wa Barca, Josep Maria Bartomeu akitarajia kusimama tena kuwania nafasi ya kuiongoza klabu hiyo mwaka 2021, pengine hakuna mgombea mwingine maarufu zaidi ya Pique, ambaye ameshabainisha wazi mpango wake wa kugombe nafasi hiyo siku za usoni klabuni hapo.

### USILOLIJUA

MANCHESTER United imevuna pointi tano katika mechi nne za mwanzo wa Ligi Kuu England msimu huu (W1 D2 L1), mara ya mwisho kuvuna pointi chache kama hizo kwenye mechi zake nne za mwanzo katika ligi hiyo ilikuwa msimu wa 1992-93 (ilipovuna pointi nne).





# Watoto 6,200 wana utapiamlo

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

ZAIDI ya wototo 6,200 wenye umri wa chini ya miaka mitano mkoani Mbeya wanakabiliwa na utapiamlo mkali kutokana na lishe duni liche ya mkoa huo, kuwa miongoni mwa mikoa inayozalisha chakula kwa wingi.

Hayo yalisemwa na Mratibu wa Lishe wa Mkoa wa Mbeya, Benson Sanga, wakati wa kikao maalumu cha kutiliana saini mikataba ya kupambana na lishe duni kwa watoto kati ya madiwani na maofisa watendaji wa Kata zote za Jiji la Mbeya na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Sanga alisema Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ndiyo inayoongoza kwa kuwa na watoto wengi wenye tatizo hilo hali ambayo inatishia ustawi wa maisha yao ya sasa na ya baadaye na hivyo akawataka wataalamu kuhakikisha wanatoa elimu.

Alisema katika halmashauri hiyo watoto waliobainika kukabiliwa na utapiamlo huo mkali ni 2,266 idadi ambayo alisema ni kubwa na inahitaji juhudi kubwa na ushirikiano wa wazazi na serikali kukabili tatizo hilo.

"Sababu kubwa ya tatizo hili ni wazazi kushindwa kutambua chakula bora kwa ajili ya watoto, mtu anajikuta anamlisha mtoto chakula cha aina moja kila siku na wengine wanazalisha mazao mengi, lakini wanauza yote, mtu ana maziwa lakini watoto wanakosa lishe hii ni aibu," alisema Sanga.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila kwenye kikao hicho, aliwataka wataalamu kutoa elimu kwa wanannchi hasa katika ngazi za vijiji.

Alisema Mkoa wa Mbeya una kila kitu hivyo ni aibu watoto kukabiliwa na utapiamlo na kwamba maofisa watendaji pamoja na madiwani wanatakiwa kusaidia kuwaelimisha wananchi kila wanapokutana nao. "Ajenda ya lishe inatakiwa ipewe kipaumbele kwenye kila kikao kuanzia ngazi ya kijiji na ninyi madiwani pamoja na watendaji ndio mnatakiwa kuhimiza hili kwa sababu muda mwingi mpo na wananchi," alisema Ntinika.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salumu Manyatta, alisema hali hiyo ni hatari katika sekta ya afya kwenye mkoa huo na kwamba njia pekee ya kumaliza tatizo hilo ni kutoa elimu ya lishe bora kwa wananchi.

# Wazee washtukia mpango kumega chuo

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

UMOJA wa wazee ambao ni wadau wa maendeleo katika Mkoa wa Mbeya (Wamambe), umeishauri Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuachana na mpango wa kumega eneo la Chuo cha Kilimo Uyole kwa ajili ya makazi na badala yake ikisaidie kuimarisha miundombinu ya barabara ili kuondoa kero ya usafiri.

Wazee hao walitoa ushauri huo juzi walipokuwa wanazungumza na waandishi wa habari kuhusu mchango wao kuhusu mpango kabambe wa maendeleo ulioandaliwa na Jiji la Mbeya ikiwamo masuala ya mpangilio wa makazi.

Mwenyekiti wa Wamambe, Mwaiseje Polisya. alisema mawazo ya watendaji wa Jiji la Mbeya kutamani kumega eneo la chuo hicho kwa ajili ya matumizi mengine ikiwamo makazi sio mawazo mema kwa maelezo kuwa vyuo vitakuwapo ndani ya miji milele na hivyo kuhitaji maeneo makubwa kadri iwezekanavyo.

Alisema wazee wanatamani chuo hicho kiwe Chuo Kikuu cha Kilimo ambacho kitakuwa kinazalisha wataalamu wa kilimo wa ngazi mbalimbali kama ilivyo kwa Chuo Kikuu cha Kilomo cha Sokoine (Sua) kilichopo mkoani Morogoro.

"Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na kuanzishwa zaidi ya miaka 50 iliyopita na kuwa na majengo mengi kama baadhi ya miji mikuu ya wilaya nchini, lakini bado hadi leo kina misitu ndani yake na hakijajaa, Chuo Kikuu cha Sokoine kina majengo mengi na mashamba makubwa, hivyo tunatamani hata chuo chetu kije kiwe kama hivyo," alisema Polisya.

Aliwaomba viongozi wa serikali kuhakikisha wanazima mawazo ya baadhi ya wanaotamani kumega eneo hilo na badala yake lisimamiwe ipasavyo, ili kuhakikisha mipaka yake haiingiliwi na wenye tamaa.

Katibu wa Wamambe, Henry Mwakasala, alisema kwa sasa barabara ambazo zinapita katika eneo la chuo hicho ni mbovu na zinakifanya chuo hicho kutofikika kiurahisi.

Aliiomba Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) kuboresha barabara hizo ili zipitike katika kipindi cha mwaka mzima tofauti na ilivyo sasa ambapo zinapitika kwa shida utadhani chuo hicho hakipo ndani ya Jiji.

Katika hatua nyingine, Polisya alisema wazee wanaiomba serikali isibadili matumizi ya uwanja wa ndege wa zamani wa mkoa huo badala ya kuwa na mawazo ya kubadili matumizi na kutaka kuweka vitu vingine.

Alisema wazee wanaiomba serikali kuuboresha uwanja huo, ili utumiwe na ndege ndogo zinazoingia jijini Mbeya, kutumika kwa dharura endapo itatokea, na kwamba katika Mji wowote maeneo ya wazi kama uwanja huo yanatakiwa kuwapo.

Alisema wazee hao wanaunga mkono nia ya serikali iliyowahi kutamkwa kuwa uwanjani hapo pataanzishwa chuo cha wataalamu wa anga na sio vinginevyo.



Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari Iyunga, Dk. Stephen Mwakajumilo (kushoto), akipokea msaada wa printa kwa niaba ya uongozi wa shule hiyo, kutoka kwa Meneja wa Kiwanda cha Bia cha TBL Mbeya, Godwin Fabian, katika hafla iliyofanyika jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. Kiwanda hicho kilitoa msaada wa printa 12 zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 50 kwa shule 12 za msingi na sekondari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi kuzalisha miche miparachichi milioni 1.5

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (Tari) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, inakusudia kuzalisha miche milioni 1.5 ya maparachichi ya kisasa kwa ajili ya kuyasambaza kwa wakulima ili kuongeza tija katika uzalishaji wa zao hilo.

Idadi hiyo inatarajiwa kugawiwa kwa wananchi na kupandwa kwenye mashamba yenye ukubwa wa hekta 8000 nchi nzima kwa lengo la kumuinua mkulima kupitia zao hilo ambalo linatajwa kuwa na soko zuri duniani kote.

Hayo yalisemwa na mtafiti wa matunda kutoka katika taasisi hiyo, Daudi Mbogo, alipokuwa anazungumza na baadhi ya wakulima waliojiunga kwenye vikundi kwa ajili ya kupata mafunzo ya kilimo bora cha maparachichi kutoka katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema wanakusudia kuzalisha mbegu hizo katika taasisi hiyo pamoja na kwenye vikundi vya wakulima waliofundishwa ili kuhakikisha mbegu bora za zao hilo zinapatikana na kusambazwa kwa wananchi na kuinua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Elimu ya uzalishaji wa mbegu bora tumekuwa tukiitoa kwa wakulima kwa muda mrefu, lakini kwa sasa tumeamua kuwashirikisha katika kuzalisha mbegu kwa ajili ya wengine, hapa kituoni tunakusudia kuzalisha miche 25,000, kupitia vikundi, tunatarajia kuzalisha miche 600,000 na mingine itazalishwa na taasisi zingine tunazoshirikiana nazo," alisema Mbago.

Alisema pamoja na miche kuzalishwa na taasisi hiyo pamoja na vikundi, lakini pia wapo wakulima ambao walishapatiwa mafunzo na wamezalisha miche ya kutosha ambayo wanaendelea kuisambaza katika maeneo mbalimbali.


Mratibu wa Utafiti na Ubunifu wa Tari-Uyole, Dk. Ndabhemeye Mlengera, alisema wameamua kulipa kipaumbele zao la maparachichi baada ya kubaini kuwa zao hilo lina soko kubwa na la uhakika ndani na nje ya nchi.

Alisema zao hilo linaweza likasaidia kuinua uchumi wa taifa kwa kuliingizia fedha nyingi za kigeni kwa madai kuwa ni miongoni mwa mazao yanayouzwa zaidi nje ya nchi. Alisema zao hilo halihitaji rasilimali fedha nyingi katika uwekezaji na hivyo kuwa rahisi kuzalisha na mkulima kupata kipato kizuri ambacho kitasaidia kuinua uchumi.

"Zao hili ni zao ambalo halimpi presha mkulima, akishapanda anaanza kusubiri kuanza kuvuna na huduma zake ni ndogo ila akianza kuvuna muda wote atakuwa anapata faida maana mtaji ni mdogo ila mavuno ni makubwa," alisema Dk. Mlengera.

Baadhi ya wakulima wa zao la parachichi ambao wameungana kwenye vikundi na kupewa elimu ya kilimo bora cha zao hilo, wamesema tayari wameanza kupata manufaa makubwa kwa kulima zao la parachichi ikiwa ni pamoja na kuwa na uhakika wa kipato.

Mmoja wa wakulima hao, Raphael Bukuku, kutoka katika Halmashauri ya Rungwe mkoani Mbeya, alisema kabla ya kuanza kujishughulisha na kilimo hicho alikuwa hana kazi maalumu ya kufanya, lakini baada ya kupata mafunzo hayo amejiajiri mwenyewe na kuwa na kipato cha uhakika. Alisema kilimo cha maparachichi ni ajira ambayo inamwezesha kujilipa mshahara mzuri kuliko hata baadhi ya watumishi wakubwa wa serikalini na hivyo akawataka wananchi wengine kuchangamkia fursa hiyo.





# Mashirika ya msaada wa kisheria yaaswa

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

MASHIRIKA yanayotoa msaada wa kisheria nchini yametakiwa kuzitumia vizuri fedha zinazotolewa na wafadhili kwa malengo yaliyokusudiwa ya kuwahudumia wananchi ili waweze kupata haki zao.

Hayo yalielezwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Kitaifa la Msaada wa Kisheria (LSF), Lulu Ng'wanakilala, wakati wa kufunga mafunzo ya siku tano kwa wawakilishi wa mashirika ya kutoa msaada wa kisheria kwa mikoa yote iliyofanyika jijini hapa.

Ng'wanakilala aliwataka mashirika hayo yanayopokea msaada fedha kutoka ufadhili wa LSF kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa na kuwasaidia wananchi kupata haki zao kwenye vyombo husika.

"Fedha hizi tunazitoa kwenu kwa lengo la kuwahudumia wananchi kupata haki zao, hivyo hatutalivumilia shiriki ambalo litashindwa kuonyesha thamani ya fedha iliyotolewa kwa malengo yalivyokusudiwa," alisema.

Mtendaji huyo alisema LSF inakabidhi misaada hiyo kutoka kwa ufadhili wa mashirika ya Kimataifa ya Danida na UKAID kwa lengo la kuyawezesha mashirika ya msaada wa kisheria hapa nchini.

Alisema mradi huo umeonyesha mafanikio tangu kuanza utekelezaji wake wa miaka mitano na ulianza mwaka 2017 na kuishia 2020 na zaidi ya wananchi milioni tano wamefikiwa na watoa huduma wa kisheria.

Naye Veroni Olomi kutoka shirika la kutoa huduma ya msaada wa kisheria Mkoa wa Kilimanjaro, alisema changamoto kubwa wanayokutana nayo ni rasilimali fedha za kuwawezesha kuwafikia wananchi wengi zaidi maeneo ya vijijini.

Olomi alisema kesi nyingi wanazokutana nazo katika maeneo ya kiutendaji ni migogoro ya ardhi hasa kutokana na mila na desturi za kuwanyima haki ya ardhi wanawake wanapofiwa na mume pamoja na kesi za ndoa na mirathi.

Alibainisha kuwa zaidi ya watoa huduma 170 wa msaada wa kisheria wamewezeshwa na shirika hilo katika mkoa huo kwa lengo la kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Kwa upande wake, mtoa huduma msaada wa kisheria Mkoa wa Simiyu, Marius Isavika, alisema uwapo wa watoa huduma hao umesaidia kupunguza vifo vya vikongwe na wenye ualbino kutokana na elimu waliyotoa maeneo ya vijijini.

"Mlikuwa mnasikia mauaji ya vikongwe yaliyokuwa yakitokea mikoa ya Kanda ya Ziwa, lakini kwa sasa matukio hayo hayasikiki sana ni kutokana na watoa huduma wa msaada wa kisheria kutoa elimu hiyo kwa wananchi hasa walioko vijijini," alisema.

Hata hivyo, alisema shirika lao limekuwa likitoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wananchi wengi wa maeneo ya vijijini kutokana na mkoa huo kuwa na asilimia 93 watu wake kuishi kwenye maeneo hayo.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Kitaifa la Msaada wa Kisheria (LSF), Lulu Ng'wanakilala (kulia), akimkabidhi cheti Eugen Philip Mawele kutoka Wilaya ya Kondoa cha kutambua kushiriki mafunzo ya wiki moja ya mashirika ya watoa msaada wa kisheria nchini yaliyofanyika jijini Dodoma wikiendi. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Jamii yaonywa kuwatenga wenye ulemavu

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, ameitaka jamii kuacha kuwatenga watu wenye ulemavu na badala yake washirikiane nao katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Katambi aliyasema hayo jijini hapa wakati wa tamasha la pamoja baina ya kituo cha watoto wenye ulemavu cha Miyuji Cheshire Home na Antonio Day Care, lililoandaliwa na taasisi ya Endless Succes.

Alisema serikali ya awamu ya tano inatoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu na imetenga asilimia mbili kati ya kumi zilizotengwa na halmashauri kwa ajili ya mikopo, hivyo hakuna sababu ya watu hao kuachwa nyuma kwenye shughuli za kijamii.

Pia, alisema taasisi inapaswa kupongezwa kwa kuandaa tamasha hilo kwa kuwakumbuka watu wa aina hiyo kwa kuwa nao wanahitaji haki ambazo jamii nyingine inapata.

Alisema uamuzi waliochukua taasisi hiyo kufurahi pamoja na watoto hao na kuwapelekea zawadi mbalimbali inachangia kuwajenga watoto hao kutambua wanapendwa na jamii.

Alisema wakichangamana na wenzao inawasaidia katika makuzi kutokana na kwamba wanafanya vile wanavyoona wenzao wanafanya.

"Watoto hawa wakikutana na wenzao kufurahi pamoja kunawasaidia kuendelea kujua vitu mbalimbali kutoka kwa wenzao ikiwamo kuongeza upeo wa kujitambua," alisema Katambi.

Awali, akisoma taarifa ya kituo hicho, Mwalimu Leochrister Gibore, alisema moja ya changamoto zinazowakabili ni pamoja na uhaba wa walimu, posho za wahudumu ikiwamo dawa ambazo zinahitajika kwa ajili ya watoto hao.

Alisema vitu hivyo ni muhimu kwa watu wa aina hiyo kwa sababu vinasaidia kuwaweka katika hali nzuri.

Naye Mkurugenzi wa Endless Success Foundation, Amina Feruz, alisema watoto hao wakionyeshwa upendo linawasaidia kuona na wao ni sawa na jamii nyingine inayowazunguka.

Alitoa wito kwa wazazi wenye watoto wenye ulemavu wasiwafiche majumbani na badala yake wawapeleke shule ili nao wapate haki ya msingi ya kupata elimu.

Alisema wakijumuika pamoja na wenzao pia kunawasaidia kupata uwelewa wa vitu mbalimbali ambavyo wenzao wanajifunza.

## Waonywa rushwa ya vitenge na pombe

**Na Peter Mkwavila, CHAMWINO**

WAKAZI wa Wilaya ya Chamwino wametakiwa kutopokea rushwa ya pombe na vitenge kutoka kwa watu wanaowania nafasi za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) wilayani humo, Idda Siriwa, alipokuwa akitoa elimu kwa vikundi mbalimbali vya ngoma za asili vilivyokuwa vimeshiriki katika tamasha la utamaduni wa mila na desturi.

Alisema kupokea vitu hivyo ni rahisi kwao kuuza haki yao ya kimsingi ya kuchagua kiongozi bora ambaye hatokani na rushwa.

"Hakikisheni mnachagua viongozi wa serikali za mitaa kwa sera na ubora wa vyama vyao vya kisiasa msipofanya hivyo mnaweza kujikuta mkikosa maendeleo," alisema.

Aliwaomba wakazi hao kutumia haki yao kwa kuwachagua viongozi watakaoleta maendeleo kwa ajili ya Watanzania wote bila kujali itikadi yoyote ya chama, dini au siasa.

Alisema wakiwachagua viongozi watoa rushwa wanaweza kujikuta wakinyanyaswa na kuwa watumwa kwa kuwa tayari walishatoa rushwa ili waweze kuchaguliwa kwenye nafasi walizoziomba.

"Ninawaomba wananchi msikubali kunyweshwa pombe wala kupokea vitenge ili muwachague, bali tumieni haki yenu ya kimsingi ya kuchagua viongozi watakaoleta maendeleo kwa ajili ya Chamwino na taifa kwa ujumla," alisema.

Kadhalika, alivitaka vikundi hivyo vilivyoshiriki tamasha hilo kuhakikisha wanatunga nyimbo zao za kutoa elimu dhidi ya ubaya wa kutoa na kupokea rushwa.

Akizungumza kwa niaba ya waandaaji wa tamasha hilo, Diwani wa Kata ya Buigiri, Keneth Yindi, alisema lengo la tamasha hilo ni kuibua vipaji ikiwa na pamoja kutoa elimu itakayofanikisha wananchi kuchukia vitendo vya rushwa.

Alisema pia kupitia tamasha hilo watahamasisha umuhimu wa kujiunga bima ya afya iliyoboreshwa ili wananchi wengi waweze kupata matibabu.





Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (katikati), akizungumza jambo wakati wa kikao cha Kamati ya Marekebisho ya Sheria ya Chama cha Mabunge Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika, mjini Zanzibar jana. **PICHA: BUNGE**

# Vijana watakiwa kuchangamkia fursa za kiuchumi visiwani

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Wilaya ya Kusini Unguja, Idrissa Mustafa Kitwana, amewataka vijana nchini kuchangamkia fursa za kiuchumi zilizopo visiwani hapo ili kujitengenezea ajira na kuacha kusubiri kuajiriwa serikalini.

Aliysema hayo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, wakati akifungua kongamano la vijana kuhusu fursa za kiuchumi zilizopo visiwani Zanzibar.

Alisema vijana ndio nguvu kazi ya taifa katika kuinua uchumi nchini hivyo ni vyema wajitume wenyewe ili waweze kujipatia kipato halali.

Aliwataka vijana kizitumia fursa ili waweze kujiajiri kwa kufanya kazi mbalimbali zenye kuwapatia riziki na kuacha kusubiri ajira kutoka serikalini.

Alisema ili vijana wawe na mustakabali mzuri wa kukuza uchumi ndani ya nchi na kujiendeleza maisha yao, lazima wawe na elimu, wajiepushe na dawa za kulevya na taifa liwe na vijana wenye afya bora na kufanya kazi zao kwa ufanisi.

"Elimu ndio ufunguo wa maisha hivyo itumieni elimu kwa kuifanyia kazi ikiwamo ujasiriamali, kilimo badala ya kuweka vyeti ndani na kusubiri ajira wakati unakupiteni," aliwatahadharisha.

Aliwataka vijana kuacha kufikiria utalii ni kutembeza wageni pekee kwa kuwa kuna kazi nyingi ambazo ni za utamaduni na ujasiriamali, hivyo wakizifanya watalii watavutiwa nazo na pato litaingia nchini.

Naye Dk. Miraji Ussi, Mkurugenzi Masoko Kamisheni ya Utalii, alisema Zanzibar utalii unakuwa na miradi mingi ipo ya kuvutia watalii vikiwamo viungo na kusuka mikeka.

Alisema miradi mingine ni sekta ya malazi na michezo ya ngoma za kiasili ambayo watalii huvutiwa nayo na kuwaomba vijana wachangamkie fursa hizo.

Washiriki wa kongamano hilo waliomba Kamisheni ya Utalii kuwapangia sera maalum watalii wanapoingia nchini kuhusu suala la kivazi ili utamaduni wa Zanzibar uweze kuimarika.

Mada nne ziliwasilishwa katika kongamano hilo ikiwamo ujasiriamali, uchumi, sekta ya utalii, uchumi wa visiwani na uchumi wa mafuta na gesi na kaulimbiu ya kongamano hilo ni 'Tumia elimu kuwa fursa ya maendeleo ya kiuchumi'.

# Comoro, Z'bar kushirikiana kibiashara

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

COMORO inatarajia kuanzisha uhusiano na kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na elimu na Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja ikiwa hatua moja wapo ya kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Hayo yameelezwa na ujumbe maalum kutoka Comoro ukiongozwa na Waziri wa Ushirikiano wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo, Said Abdallah, uliofika Zanzibar kwa ziara ya siku nne katika mkoa huo, walipokuwa wakizungumza na Mkuu wa Mkoa huo Ayoub Mohammed Mahmoud, ofisini kwake.

Akizungumza kwa niaba ya ujumbe huo, Waziri Said alisema ujio wao katika Mkoa wa Mjini Magharibi ni kuomba ushirikiano wa kubadilishana uzoefu kwa shughuli mbalimbali za maendeleo kati ya mikoa ya Comoro na Mjini Magharibi ukiwamo Mkoa wa Ngazija ambao anatoka kiongozi huyo.

"Tumekuja kuomba ushirikiano wa kiutendaji kwa mikoa yetu na manispaa zake na mkoa huu wa Mjini na manispaa zenu katika masuala ya kijamii kwa kuanzia tuanze na sekta ya elimu na biashara maana tumeona mwingiliano uliopo kwa wananchi wetu wa Comoro wanakuja Zanzibar kwa shughuli mbalimbali na Wazanzibar wapo Comoro kwa shughuli za biashara," alisema Said.

Alisema uzoefu unaonyesha viongozi wengi wa visiwa wanajishughulisha zaidi na siasa na kusahau wajibu wao wa msingi wa kuwaletea maendeleo wananchi wao hatua ambayo inadumaza ukuaji wa uchumi.

"Uzoefu tulionao sisi viongozi wa visiwa wengi wetu tunapopata nafasi za kuwatumikia wananchi tunajisahau na kujishughulisha zaidi katika siasa na kusahau kuwatumikia wananchi, sasa mimi nimeamua kwa nafasi niliyonayo kuwashawishi wenzangu kuja kwenu kujifunza na kuomba ushirikiano wa kuwaletea maendeleo wananchi wetu," alisema.

Alisema wananchi wa Comoro wanajishughulisha zaidi na biashara na hawana uwezo wa kuzalisha bidhaa zao wenyewe, hivyo watatumia uwezo na fursa ziliopo katika Mkoa wa Mjini Magharibi kuleta mabadiliko ya kiuchumi kwenye mikoa na manispaa zao wanazotoka.

**"Nchi zetu hizi zina ushirikiano wa muda mrefu, wananchi wetu wamekuwa wakiishi pamoja, lakini hapo pia upo umoja wa watu wa Comoro ambao una ushirikiano wa karibu na serikali, visiwa hivi vinaunganishwa moja kwa moja na usafiri wa baharini kuna meli zetu zinafanya safari zake nchini Comoro," alisema Ayoub.**

Naye Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema visiwa vya Zanzibar na Comoro vina uhusiano wa kindugu kwa kipindi kirefu na kuunganishwa moja kwa moja na usafiri wa baharini.

"Nchi zetu hizi zina ushirikiano wa muda mrefu, wananchi wetu wamekuwa wakiishi pamoja, lakini hapo pia upo umoja wa watu wa Comoro ambao una ushirikiano wa karibu na serikali, visiwa hivi vinaunganishwa moja kwa moja na usafiri wa baharini kuna meli zetu zinafanya safari zake nchini Comoro," alisema Ayoub.

Aliahidi kuendeleza ushirikiano na udugu uliopo kwa wananchi wa visiwa hivyo na kwamba serikali ya mkoa wake itafanya kazi kwa karibu na baadhi ya mikoa ya kisiwa hicho waliofika kutaka ushirikiano.

# Wanaume wakumbushwa jukumu la malezi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WANAUME wametakiwa kushughulikia majukumu yao hasa ya kifamilia na kuacha kuwatupia lawama kinamama.

Wakitoa michango yao wakati wa mafunzo ya ushirikishaji jamii katika kuboresha utoaji na upatikanaji wa elimu ya jinsia, afya ya uzazi na maadili kwa vijana, katika ukumbi wa Kituo cha Walimu TC Bububu Wilaya ya Magharibi A Unguja, walisema kumekuwapo na tabia kwa baadhi ya kinababa kuwabebesha mzigo wa majukumu kinamama wa familia hali ambayo haitakiwi kwa mujibu wa sheria za dini.

Wamesema kinamama wengi hasa katika maisha ya sasa wanahangaika kujitafutia riziki wapate mahitaji yao na watoto jambo ambalo linatakiwa kutekelezwa na kina baba.

Juma Khamis miongoni mwa washiriki hao, alisema muda mwingi wamekuwa wakiupoteza kuhangaika badala ya kukaa nyumbani na kuwashughulikia masuala mengine ya msingi hasa ya ndoa zao.

Alisema imezoeleka kuwa familia hasa mtoto anapoharibika kitabia lawama zote hupewa mama kutokana na kinababa kutokuwa na muda wa uangalizi wa watoto wake.

Akiwasilisha mada mratibu wa mradi kutoka Unesco Kanda ya Tanzania, Matheas Herman, alisema watoto wanapata maudhi tofauti katika mizunguko yao ya kimaisha kutokana na kutokuwa na ukaribu zaidi na wazazi wao na hivyo kuwafanya wapate vishawishi na kusababisha kuharibikiwa katika maisha yao, kwa kupata ujauzito na wengine kujiingiza katika makundi maovu na uasherati.

Aliwaomba wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao na kuwaelimisha zaidi kuhusu hali halisi ya maisha pamoja na athari za kujihusisha na makundi maovu na uasherati.

# ‘Saratani yoyote kwa watoto inatibika’

**Na Frank Monyo**

IMEELEZWA kuwa ugonjwa wa saratani yoyote kwa watoto unatibika kwa zaidi ya asilimia 80, endapo wenye dalili za awali za ugojwa huo wakiwahishwa hospitali kwa ajili ya uchunguzi na kuanza matibabu ya mapema.

Watoto zaidi ya 600 waliopatiwa matibabu kwa mwaka 2011 hadi 2018, asilimia 50 hadi 60 wamepona ikiwa ni asilimia 20 ya watoto zaidi ya 2,000 ambao hawajafika hospitali kwa ajili ya matibabu.

Hayo yameelezwa jijini Dar es Salaam jana na Mratibu wa Mipango kutoka Taasisi ya Tumaini la Maisha (TLM), Lilian Ndyetabula, wakati wa tamasha la uchagiaji wa huduma za matibabu na elimu kwa umma juu ya magojwa ya saratani kwa watoto.

Alisema kuwa TLM ni taasisi isiyo ya serikali inayofanya kazi kwa karibu na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kitengo cha saratani kwa watoto na

ilianzisha mwaka 2011 na wazazi wa watoto wenye saratani, madaktari, na wafanyabiashara lengo likiwa ni kutatua changamoto ya watoto wanasumbuliwa na ugonjwa huo kuchelewa kufika hospitali kupatiwa matibabu na kuokoa maisha yao.

“Tulivyokuwa tunaanza tuliwafikia watoto zaidi ya 600 na kati yao asilimia 50 hadi 60 wamepona na kwa hao wanaofika hospitali ni asilimia 20, hivyo tunakadiria watoto zaidi 2,000 hawajafika hii inamaanisha bado kuna kazi kubwa baadaye,” alisema Ndyetabula.

Aliongeza kuwa kwa kipindi hicho watoto wengi walikuwa wanafikishwa hospitali wakiwa wamechelewa na wamepita kiwango cha matibabu na hivyo hupelekea wengi wao kupoteza maisha.

Alisema katika kupunguza changamoto hiyo, wameanzisha mpango mkakati kwa mwaka 2019-2025 wa kuwafikia watoto popote walipo na kuhakikisha hata kama mtoto anasafirishwa kutoka mkoani kwenda Muhimbili afike kwa wakati na kuanza matibabu.

“Katika mpango huu tumeanza kushirikiana na Hospitali kama Bugando, KCMC, Mnazi Mmoja Zanzibar, Mbeya na Dodoma kwa kuweka vituo ambapo wazazi wanaweza kuwapeleka watoto katika hospitali hizo kuanza matibabu ya awali, lakini tunataka tufike hata chini zaidi hadi kwenye zahanati, ambapo huko ndio wanawaona watoto kwa mapema, kwani mzazi wa kijiji sehemu ya kwanza atakayompeleka mtoto ni zahanati,” alisema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya TLM na mwanzilishi wa taasisi hiyo, Gerald Mongella, alisema saratani kwa watoto inatibika, hivyo wazazi wasikimbilie njia ambazo sio rasmi katika kutafuta matibabu ya watoto wao badala yake wawapeleke hospitali kwa uchunguzi zaidi.

Kwa upande wa Fatuma Heri, ambaye amepona saratani ya shingo, alisema kuwa alipata ugonjwa huo mwaka 2009 na baada ya kufanyiwa vipimo katika hospitali ya CCBRT aligundulika kuwa na saratani ya uvimbe shingoni.

“Namshukuru Mungu kwa kuniponya saratani kwani nakumbuka 2009 nilitokewa na uvimbe kwenye shingo, wazazi wangu walinipeleka CCBRT na nikatolewa nyama kwa ajali ya kufanyiwa kipimo na baada ya majibu nikagundulika kuwa na saratani ya uvimbe shingoni,” alisema Fatuma na kuongeza kuwa;

“Baada ya kugundulika nilianza matibabu, dawa nilizokuwa natumia zilikuwa zinasababisha nanyonyoka nywele na kutapika nawashukuru TLM na Dk. Kaijage kwani niliambiwa mambo mengi sana kuwa ukutumia mionzi hutozaa mara utakufa lakini mimi mpaka leo nipo hai na nimepona,” alisema.



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Hifadhi Eneo la Ngorongoro, Prof. Abiud Kaswamila (kulia), akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Santos Silayo (kushoto), kabla ya kufunga mkutano wa tano wa kisayansi jijini Arusha mwishoni wa wiki. Katikati ni Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Prof.Esnati Chaggu. **MPIGAPICHA WETU**

# Wanasayansi, watafiti wataka kipaumbele uhifadhi mazingira

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

MATOKEO ya utafiti mbalimbali uliowasilishwa na kujadiliwa katika Mkutano wa Tano wa Kisayansi juu ya utafiti wa mazingira utaleta manufaa kwa taifa ikiwa serikali itayapokea na kuyafanyia kazi kama watunga sera ili utekelezaji wake ufanyike kwa lengo la kuhifadhi na kutunza mazingira.

Akizungumza baada ya kufunga mkutano wa siku tatu uliofanyika jijini hapa mwishoni mwa wiki na mada ikiwa Binadamu na Utunzaji wa Viumbe hai kwa Maendeleo endelevu ya Mazingira, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Uhifadhi wa Ngorongoro, Prof. Abiud Kaswamila, alisema mkutano umekuwa wa mafanikio makubwa kutokana na ushiriki na mawasilisho ya utafiti.

“Mengi yaliyojadiliwa katika mkutano yamelenga katika kutunza maeneo yaliyohifadhiwa ili yaendelee kuwa katika hali yake asili na kuifanya nchi kutoingia katika hatari kuwa jangwa,” alisema Prof. Kaswamila.

Alisisitiza kuwa mkutano kama huo ni muhimu ukafanyika kila wakati hali itakayosaidia kujadili utafiti pamoja na hatimaye kuja na mapendekezo yatakayosaidia nchini katika suala zima la utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

“Umuhimu wa kuhifadhi na kutunza mazingira ni jukumu la kila Mtanzania hivyo kwa wasimamizi wa Sheria za Mazingira wanawajibu wa kuendelea kutoa elimu ili kuwajengea uelewa wananchi juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira,” alisema Prof. Kaswamila.

Alisema ushirikiano ulioonyeshwa na wajumbe wote zaidi ya 150 kuwapo katika mkutano huo ni uthibitisho kuwa uhifadhi na utunzaji wa mazingira ni muhimu kwa faida ya taifa na kwa kizazi cha sasa na baadaye.

Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ambao ndiyo waratibu wa mkutano huo, Prof. Esnati Chaggu, alisema baraza limeandaa mkutano huo kama Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 inavyowaelekeza kuwa na mikutano ambayo itasaidia kuleta mawazo katika utunzaji wa mazingira.

“Maeneo yaliyohifadhiwa kama Ziwa Manyara ni lazima yaendelee kubaki katika hali ya usalama kimazingira ili uhasilia wa eneo uwe endelevu hata kwa vivazi vijavyo,” alisema Prof. Chaggu.

Alisema kuwa kuna maeneo matano nchini ambayo yametengwa kuwa hifadhi ya binadamu na viumbe hai kama vile Serengeti -Ngorongoro, Ziwa Manyara, Hifadhi ya Usambara Mashariki, Gobe- Masito- Ugala na Jozani Chwaka bay ni muhimu yakaendelea kulindwa kutokana na ekolojia iliyopo katika maeneo hayo.

Mmoja wa wajumbe wa mkutano huo na pia Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Santos Silayo, alisema TFS ni miongoni mwa wadau wakubwa wa mazingira na walishiriki ili kutoa mchango kuhusu suala nzima la uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

“Tumeshiriki kuonyesha uzoefu wetu katika kusimamia utunzaji wa mazingira hasa misitu na ekolojia zake ambazo ni hazina kwa taifa na namna jamii inavyofaidika na mazingira,” alisema na kuongeza kuwa mkutano ulikuwa wa mafanikio makubwa.

## Mazao ya misitu yaingiza mil. 1.9/- kwa siku mbili

**Na Dege Masoli, MUHEZA**

ZAIDI ya Sh. milioni 1.9 zimekusanywa na serikali kwa siku mbili kutokana na mauzo ya mazao ya misitu yaliyofanyika kwa njia ya mnada katika wilaya za Kilosa mkoani Morogoro na Muheza mkoani Tanga.

Akizungumza baada ya mnada kwenye shamba la Longuza, Mkurugenzi wa Mipango na Matumizi ya Misiti, Mohamed Kilongo, alisema kisasi hicho kimekusanywa kwenye misiti ya Mtibwa Wilaya ya Kilosa Mkoa wa Morogoro na Longuza lililopo Wilaya ya Muheza mkoani Tanga.

Kilongo alifafanua kuwa zaidi ya Sh. milioni 453 zilikusanywa katika mnada wa shamba la Mtibwa na zaidi ya Sh. milioni 1.5 zilipatikana kwenye uuzwaji wa miti ya shamba la Longuza baada ya kuuzwa ujazo wa 2,100 kati ya elfu 12 zilizopangwa kuuzwa.

Alisema serikali imepanga kuuza miti ya eneo la ujazo wa milioni 1.62.8 katika misiti yake 13 iliyopo nchini, na kwamba miti iliyouzwa Longuza ni ya aina ya misaji yenye umri wa miaka 48.

Alieleza kuwa mpango wa uuzwaji wa mazao ya misitu ulianza mwaka 2012 baada ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Misitu (TFS) ambapo aina tatu za kuuzwa mazao hayo zinatumika ikiwamo utumaji maombi yaani mnunuzi, kutangazwa kwa mnada na mali zitakazouzwa na ule wa mazungumzo na mnunuzi husika.

Naye Ofisa Misitu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Misitu na Nyuki, Dk. Cellina Mongo, alisema minada hiyo inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Misitu sura 323, kanuni za misitu za mwaka 2004 na Tangazo la Serikali Namba 255/2017.

## HABARI KIMATAIFA



Rais wa Ujeruman, Frank-Walter Steinmeier (kushoto) na mwenzake wa Poland, Andrzej Duda, wakiwa katika maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 80 ya vita vya pili vya dunia katika mji wa Wielun, Poland. **PICHA: ALLIANCE**

# Watu milioni mbili wafutiwa uraia India

**NEW DELHI,** India

INDIA imechapisha orodha ya mwisho ya watu wapatao milioni 1.9 iliyowafuta uraia waliokuwa wakiishi Kaskazini Mashariki mwa nchi hiyo.

Usajili wa kitaifa wa raia (NRC) ni orodha ya watu ambao wanaweza kuthibitisha kuwa waliinga nchini humo hadi Machi 24, 1871, kabla ya Bangladesh kupata uhuru wake kutoka kwa Pakistan.

Watu ambao hawajajumuishwa katika usajili huo wamepewa siku 120 kukata rufani dhidi ya hatua ya kufutiwa uraia wa nchi hiyo.

Hata hivyo, bado haijabainika nini kitafuata baada ya hatua hiyo kutekelezwa. Serikali ya India imesema mpango huo ni muhimu katika mchakato wa kuwabaini wahamiaji haramu kutoka Bangladesh.

Idadi kubwa ya watu waliokamatwa wanazuiliwa katika kambi ya muda kwa kushukiwa kuwa raia wa kigeni, lakini kuna hofu endapo watakubalika walikotoka.

Mpango huo umezua gumzo kali huku baadhi ya watu wakidai ni hujuma dhidi ya jamii ya Assam walio wachache nchini India.

Rasimu ya usajili iliyochapishwa mwaka jana iliwatenga watu milioni nne.

Usajili wa NRC ilibuniwa mwaka 1951 ambayo ililenga kutofautisha mzaliwa wa Assam ambaye ni raia halisi na mhamiaji kutoka taifa jirani la Bangladesh. Usajili huo umefanyiwa mabadiliko kwa mara ya kwanza.

Familia katika Jimbo la Assam wamekuwa wakitakiwa kuwasilisha stakabadhi zinazothibitisha kuwa ni wazawa wa nchi hiyo, huku wale wanaoshindwa kufanya hivyo wakichukuliwa kuwa wahamiaji haramu.

Chama cha Bharatiya Janata (BJP) cha Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi, kwa muda mrefu kimekuwa kikipinga uhamiaji haramu nchini humo, lakini miaka ya hivi karibuni kimeiunga mkono usajili wa kitaifa wa raia.

**Mahakama maalumu za kusikiliza kesi za uraia nchini India zilibuniwa mara ya kwanza mwaka 1964 na tangu wakati huo mahakama hiyo imeamua kuwa zaidi ya wananchi 100,000 ni raia wa**

Kwa kuhofia huenda wakavuliwa uraia na baadaye kufungwa jela maelfu ya Wahindu wa Bengali na Waislamu wamejiua tangu mpango wa usajili wa uraia ulipoanza mwaka 2015.

Baadhi ya watu waliozuiliwa wanalalamikia hali mbaya ya maisha katika vituo vya kuwashikilia wale wanaodaiwa kuwa wahamiaji haramu ambavyo vimejaa kupita kiasi.

Mahakama maalumu za kusikiliza kesi za uraia nchini India zilibuniwa mara ya kwanza mwaka 1964 na tangu wakati huo mahakama hiyo imeamua kuwa zaidi ya wananchi 100,000 ni raia wa kigeni.

Lakini uamuzi wa mahakama hizo zimekumbwa na utata kutokana na jinsi zinavyoendeshwa.

Suala la kubaini ikiwa mtu ni mzawa wa India au mhamiaji haramu limekuwa likizua utata kwa kuwa familia nyingi hazina stakabadhi hali inayotokana na ukosefu elimu, huku wengi wao hawatilii maanani umuhimu wa kutunza nyaraka.

Wengine hawana fedha za kuwasilisha madai hayo kesi mahakamani ili wapate ufumbuzi wa kisheria Assam ni moja ya majimbo ya India inayokaliwa na watu kutoka jamii tofauti na suala la uraia wao limekuwa likitiliwa shaka kwa muda mrefu.

Miongoni mwa watu hao ni jamii ya Bengali na Assamese-wanaozungumza kihindi.

Theluthi tatu ya watu milioni 32 wanaoishi katika jimbo hilo ni Waislamu, idadi ambayo ni ya pili kwa ukubwa baada ya wale wanaoishi Kashmir.

Wengi wao wametokana na kizazi cha wahamiaji walikaa katika eneo hilo wakati wa utawala wa Uingereza.

Lakini wahamiaji haramu kutoka taifa jirani la Bangladesh, ni kilomita 4,000 kutoka mpaka wa India, wamekuwa wakiishi kwa hofu kwa miongo kadhaa sasa.

Mwaka 2016 serikali ilitangaza kuwa karibu watu milioni 20 wanaoishi India ni wahamiaji haramu.

Watu wengi wanasema mpango huo hauna uhusiano wowote na masuala ya kidini, lakini wanaharakati wa kutetea haki wanadai kuwa jamii ya Bengali ambao wengi wao ni waumini wa dini ya Kiislamu, ndio wanaolengwa.

Pia wanahofia hali ya Waislamu wa jamii ya Rohingya walio wachache katika taifa jirani la Bangladesh.

Hata hivyo, Wahindi kadhaa wanaozungumza Kibengali-hawajahusishwa katika zoezi hilo hali ambayo imezua taharuki katika Jimbo la Assam.

"Moja ya jamii iliyoathiriwa zaidi na mpango huu ni Wahidu wa Bengali. Wengi wao wamekamatwa na kuzuiliwa kambini. Hii ndio sababu siku chache kabla ya NRC kuchapishwa BJP ilibadili mkondo wa mchakato huo ikisema kuwa inakiri kosa lilifanyika katika uchapishaji wa orodha hiyo ya mwisho. Hii ni kwasababu Wahidu wa Bengali ni wafuasi sugu wa BJP," alisema Barooah Pisharoty.

Watu zaidi ya 1,000 waliothibitishwa kuwa raia wa kigeni wamekuwa wakizuiliwa kwa miezi sita sasa katika jela za India.

Serikali ya India pia inajenga jela mpya itakayoweza kuwa na uwezo wa kuchukua watu 3000. **BBC**

# Papa Francis akwama kwenye lifti dakika 25

**VATICAN,** Italy

KIONGOZI wa Kanisa la Katoliki duniani, Papa Francis, ameomba radhi waumini kwa kuchelewa misa katika Kanisa la Mtakatifu Petro na kusema kuwa alikwama kwenye lifti akiwa anaelekea kanisani.

Kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 82 alikwama kwenye lifti kwa dakika 25 baada ya umeme kukatika na kuweza kutoka kabla ya kikosi cha wazima moto hakijawasili.

"Ninapaswa kuomba radhi kwa kuchelewa," alisema Papa Francis (pichani chini) wakati akiwaeleza waumini wake huku akitabasamu.

Aidha, aliwataka waumini wote kuwapongeza wazima moto kwa kazi kubwa waliofanya.

Ahutubia umati wa waumini, Papa Francis alisema kulikuwa na hitilafu ya umeme hivyo lifti ilisimama.

Alisema: "Namshukuru Mungu na kikosi cha zimamoto kifika kwa wakati."

Televisheni inayorusha matangazo ya moja kwa moja ya sala hiyo walihisi papa huyo amechelewa kufika katika misa kutokana na sababu za kiafya.

Papa Francis alitangaza pia kuwa mwezi ujao, atatangaza makadinari 10 wapya wa Kanisa Katoliki. **BBC**



# Mkutano wa huduma za ndege waanza nchini

Na Beatrice Shayo

MKUTANO wa Kimataifa wa Shirikisho la Taasisi zinazotoa huduma za anga na kuongoza ndege (CANSO) unaanza leo nchi na utajadili mambo mbalimbali ikiwamo teknolojia ya pamoja katika anga barani Afrika.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Hamza Johari, ambaye pia ni Mwenyekiti wa CANSO alisema, mkutano huo, huo unatarajiwa kumalizika Septemba 6, na utahudhuriwa na wajumbe zaidi ya 200 kutoka barani Afrika.

"Tunataka ndege inapoingia Bara la Afrika inakutana na huduma zote ambazo ni sawa kwa sasa kuna changamoto ya teknolojia zinatofautiana baina ya nchi na nchi, hivyo rubani inamlazimu abadilike kutokana na nchi anayokwenda kutua," alisema.

Johari alisema wanachokitaka ni upatikanaji wa mfumo mmoja ambao unatoa huduma bora na sio kila nchi kuwa na teknolojia yake katika masuala ya usafiri wa anga.

Alisema moja ya vitu watakavyovijadili ni mfumo wa pamoja ili kumsaidia rubani kuendesha ndege kwa uhakika bila vikwazo kutoka nchi moja kwenda nyingine ili kuwa na anga linalofanana kama kaulimbiu inavyotaka.

Alisema kaulimbiu ya mkutano huo ni; 'Kuelekea anga isiyo na mipaka barani Afrika na mchango wake katika kizazi kijacho cha wataalamu wa usafiri wa anga'.

Pia alisema pamoja na mambo mengine wajumbe wa mkutano huo watajadili na kutoa suluhu kwenye masuala ya namna ya kuwa na anga lisilo na vikwazo barani Afrika, kutokana na kuwa na mitambo ya kuongoza ndege inayoweza kuwasiliana na taratibu zinazofanana ambazo zitasaidia kuimarisha usalama wa anga.

"Wajumbe watapata fursa ya kujadili jinsi nchi wanachama wa Kanda ya Afrika watakavyoboresha ushirikiano na kujadili changamoto ya kuepusha uwezekano wa ajali kati ya ndege zisizo na rubani (drons)," alisema Johari.

Alisema kwa mujibu wa takwimu sekta ya anga barani Afrika inakuwa kwa haraka na idadi ya safari za ndege inatarajiwa kuongezeka mara mbili ya sasa katika kipindi cha miaka kumi ijayo.

Johari alisema kuna ongezeko kubwa la ndege zisizo na rubani na vyombo vingine vinavyotumika anga.

Alisema ukuaji wa sekta pamoja na maendeleo ya teknolojia vinahitaji kuwekwa kwa taratibu mpya za usimamizi na udhibiti wa sekta ili kusiwapo madhara.

Alisema katika mkutano huo siku ya kwanza wajumbe wa Afrika watakutana ambapo kutakuwa na wataalamu mbalimbali wataotengeneza mikakati ya kufungua fursa ikiwamo uboreshaji mifumo ya ndege na usimamizi wa vyombo hivyo.

Alisema mikakati watakayojiwekea itasaidia katika Mkutano wa CANSO unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu nchini Marekani.



Wanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya St Anne Marie Academy ya Mbezi kwa Msuguri, jijini Dar es Salaam, wakiwa kwenye mahafali yao yaliyofanyika kwenye viwanja vya shule hiyo, mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Pemba, Unguja wafurahia kasi ya 4G

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya Vodacom Tanzania Plc imezindua huduma ya intaneti yenye kasi ya 4G visiwani Zanzibar (Pemba na Unguja) na wakazi wake watapata fursa ya mtandao wenye kasi zaidi nchini.

Katika visiwa hivyo Vodacom ina minara zaidi ya 53 yenye kasi ya 4G, 3G na 2G ambayo inawezesha wakazi hao kufurahia huduma kutokana na uwezo wa vifaa vyao.

Akizungumza kuhusu maendeleo hayo, Mkurugenzi wa Kitengo cha Network wa Vodacom, Alec Mulonga, alisisitiza kwamba, kampuni hiyo imejikita kuipeleka Tanzania kwenye zama za kidijitali na kuhakikisha kwamba kila mtu anaunganishwa.

"Vodacom Tanzania inaamini katika nguvu ya teknolojia kwenye kuleta maendeleo na kutoa fursa mpya. Kuunganisha ngome hii ya utalii - Zanzibar na huduma yetu ya 4G kutaleta fursa mpya za maendeleo kwa kuwa tutakuwa tumeifungua katika soko la dunia na huduma nyingine za kimtandao kama elimu, afya, kilimo na usalama pamoja na kukuza uchumi wa Wazanzibari," alisema Mulonga.

Alisema uwapo wa intaneti umebadilisha namna ya upatikanaji wa taarifa na ufanyaji biashara. Na kwa upande wa utalii, intaneti ina uwezo wa kuwafanya watalii kufurahia zaidi safari zao nchini Tanzania na vile vile kuwaongezea uwezo wa kupata huduma za malazi kwa gharama nafuu kupitia mtandao. Pia ni chombo cha kuwezesha utangazaji wa biashara na mawasiliano kati ya watoa huduma na watu wengine.

Alisema kwa zaidi ya miaka 20, Vodacom Tanzania imewekeza katika kuboresha mtandao wao ili uweze kuwafikia na kuwaunganisha mamilioni ya Watanzania. Upatikanaji huu wa mtandao wenye kasi utawezesha ufanisi wa utendaji kazi wa sekta ya utalii visiwani Zanzibar.

Kwa upande wake, Mwanakheri Abdulswamadu, mkazi wa Mchambawima Unguja alieleza furaha yake kuhusu upatikanaji wa mtandao huo wenye kasi zaidi.

"Tunachokiona leo ni matokeo ya uwekezaji mkubwa unaofanywa na Vodacom Tanzania kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa mtandao wetu, Mfano; mwaka uliopita tuliingia mkataba wa kukodisha Mkongo wa Taifa (NICTBB) na kuboresha vituo vyetu kote nchini. Tumedhamiria kuwekeza kwenye miundombinu ya mtandao ili kukidhi mahitaji ya wateja wetu upande mawasiliano na pia kupunguza utofauti wa kidijitali, pia kuimarisha uwezo wa ushindani kati ya mashirika ya mawasiliano hapa nchini," alisema Mulonga.

# Kibano watendaji ujenzi madarasa

Na Lilian Lugakingira, BUKOBA

MKUU wa Wilaya ya Muleba mkoani Kagera, Richard Ruyango, ameiagiza idara ya ujenzi ya wilaya hiyo kutoa ramani za majengo ya vyumba vya madarasa kwa watendaji wote wa vijiji na kata ili kuepuka baadhi ya miradi ya ujenzi huo kukwama kutokana na kutokuwapo kwa ramani, na kusababisha baadhi ya wanafunzi kujifunzia katika mazingira hatarishi.

Agizo hilo alilitoa wakati wa uzinduzi wa vyumba viwili vya madarasa katika shule za msingi Akanazi na Ichwandimi na matundu 16 ya vyoo katika shule za msingi Bushekya na Kishoju, vilivyojengwa na Shirika la World Vision kwa kushirikiana na wananchi wa kata za Bisheke na Mubunda, kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 100.2, kupitia mradi wa Mbuka AP.

Ruyango alisema kuwa serikali haiwezi kukubali ujenzi wa vyumba vya madarasa kukwama kutokana na uzembe wa baadhi ya watumishi, baada ya kufika Shule ya Msingi Akanazi na kukuta matofali yaliyofyatuliwa kwa nguvu za wananchi yakiwa yameanza kuharibika, huku ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule hiyo yenye wanafunzi 727 na vyumba vinne tu vya kudumu vya madarasa ukiwa umesimama, kutokana na utata wa ramani.

"Hatuwezi kuendelea kuwa na wahandisi wababaishaji wanaokwamisha miradi bila sababu za msingi, yeyote ambaye hatakuwa makini na kazi yake ataondolewa," alisema.

Aidha, aliwataka viongozi na watendaji wa vijiji na kata katika Wilaya ya Muleba kuhamasisha wananchi kuchangia nguvu zao kwa kukusanya vifaa vya ujenzi, ili kujenga madarasa imara na kuwaepusha watoto kusomea katika madarasa yasiyofaa, yakiwamo yaliyojengwa kwa udongo ambayo ni hatari kwa usalama wa wanafunzi hasa wakati wa mvua.

Baada ya kutembelea shule hizo nne kwa ajili ya kupokea vyoo na vyumba vya madarasa aligundua uwapo wa uhaba wa vyumba vya madarasa na matumizi ya madarasa yasiyofaa yaliyojengwa kwa udongo, na kusema k serikali na wadau wengine wa maendeleo wanafanya jitihada kubwa kuboresha mazingira ya kujifunzia, lakini bado nguvu za wananchi zinahitajika.

Mwakilishi wa Meneja wa World Vision Tanzania Kanda ya Kagera, Joseph Potino, alisema ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa na vyoo umezingatia mazingira rafiki kwa watu wenye mahitaji maalum.

Alisema vyumba viwili vya madarasa vimegharimu zaidi ya Sh. milioni 47.8 ambapo World Vision ilitoa zaidi ya Sh. milioni 46.7 na mchango wa wananchi ni zaidi ya Sh. milioni moja, na kuwa kwa upande wa matundu 16 ya vyoo yaliyogharimu zaidi ya Sh. milioni 52.4, shirika hilo limetoa zaidi ya Sh. milioni 51.6 na wananchi walichangia Sh. 820,000.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI**

Anahitajika - Mhasibu na sales Lady
Sifa – Awe Mwanamke
Elimu – Diploma

Ofisi yetu ipo Posta – Dar es Salaam
Kwa Mawasiliano :- 0715 – 885 533

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BARCELONA, PSG WASITISHA MAZUNGUMZO YA NEYMAR




**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imesitisha mazungumzo na Paris Saint-Germain kwa ajili ya kumsajili Neymar, lakini watatoa ofa nyingine kwa nyota huyo wa Brazil kipindi kijacho cha majira ya joto, kwa mujibu wa ESPN FC.

Vyanzo vilivyopo karibu na mabingwa hao wa Ligue 1 pia vimethibitisha Jumamosi kwamba mpango huo umesitishwa rasmi na Neymar ataendelea kubakia jijini Paris.

Baada ya wiki kadhaa za majadiliano ya makubaliano na Paris Saint-Germain, Barca imeshindwa kukamilisha mpango wa kumsajili Neymar ili atue tena kwenye dimba la Camp Nou.

Hata hivyo, hiyo haitakuwa mwisho wa Barca kumtaka mshambuliaji huyo, kwani watarudi tena kipindi kijacho cha majira ya joto.

Klabu hiyo inapanga kuhakikisha kwamba, itatoa ofa nyingine kwa Neymar katika kipindi kijacho cha majira ya joto ili kumrudisha mchezaji huyo hapo Camp Nou baada ya kuondoka mwaka 2007.

Akizungumza Ijumaa, mkurugenzi wa soka wa PSG, Leonardo alisema klabu hiyo bado imefungua milango ya kumuuza Neymar kwenda Barca, lakini ofa yao haikufikia ile waliyoitaka wao.

PSG inataka kiasi cha euro milioni 222, ambazo walimnunua Neymar kutoka Barca mwaka 2007.

# Koulibaly aizawadia ushindi Juventus Serie A

**TURIN,** Italia

BEKI wa Napoli, Kalidou Koulibaly alijifunga dakika za majeruhi na kuwapa Juventus ushindi wa mabao 4-3 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, mjini Turin juzi Jumamosi.

Napoli iliyokuwa nyuma kwa mabao 3-0 ilipigana na kukomboa mabao yote matatu, lakini bao la kujifunga na Koulibaly likawapa ushindi Juve.

Mabao kutoka kwa Danilo, Gonzalo Higuain na Cristiano Ronaldo yaliwapa mabingwa hao wa Italia uongozi wa 3-0.

Napoli hawakukata tamaa na Kostas Manolas na Hirving Lozano wakafunga kila mmoja bao moja kabla ya Giovanni Di Lorenzo kufunga bao la tatu la kusawazisha.

Lakini Koulibaly akiwa kwenye harakati za kuokoa mpira langoni kwake dakika za majeruhi akajikuta akisukumia mpira kwenye vyavu za goli lake na kumuacha kocha wa Napoli, Carlo Ancelotti akiondoka kichwa chini.

"Juventus wana kiwango kizuri, tunajua hilo na ndio maana tulicheza kwa tahadhari kubwa, lakini kosa moja likatugharimu," alisema Ancelotti akiiambia Sky Sport Italia baada ya mchezo huo.

"Tunaweza kushinda, lakini tulipoteza nafasi, ni jambo la kawaida kwenye soka na naamini tutakuwa na nafasi nyingine."




# Klopp: Mane hana hasira na Mo Salah




**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amethibitisha kwamba, Sadio Mane "alikwazika" baada ya kuonyesha ishara ya hasira wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Burnley, lakini "kila kitu kiko sawa."

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal alionyesha ghadhabu wakati akielekea benchi alipotolewa dakika ya 85, akionyesha kukasirishwa na maamuzi ya awali ya Mohamed Salah kutompasia mpira wakati akiwa eneo la penalti.

James Milner, Joe Gomez, Jordan Henderson na Roberto Firmino wote walijaribu kumtuliza wakati alipoonekana kubwatukiana na Andreas Kornmayer, kocha wa viungo wa Liverpool.

Klopp alibainisha Mane, ambaye alifunga bao la pili la Liverpool kwenye dimba la Turf Moor, kwamba alionekana kukwazika.

Kocha huyo alibainisha kwamba, alizungumza na mchezaji huyo kwenye vyumba vya kubadilishia nguo ili kulimaliza tatizo hilo.

"Alikasirika, hicho ni kitu cha kawaida," alisema Klopp. "Sadio hawezi kuficha hisia zake na napenda hilo. Ila kila kitu kimeshamalizika.

"Tulizungumza kuhusu hilo na kila kitu kipo sawa. Sisi ni binadamu na mambo kama hayo huwa yanatokea, si jambo la ajabu."

# Madrid kumsajili Fernandes

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Fiorentina kupitia kwa mkurugenzi wake, Daniele Prade imesema kwamba Real Madrid watamsajili kiungo na nahodha wa Sporting Lisbon, Bruno Fernandes kabla ya dirisha kufungwa leo Jumatatu saa sita usiku.

Mapema wiki hii, Real Madrid waliripotiwa kuwa kwenye mazungumzo na wakala wa kiungo Fernandes kujadili mpango wa kumsajili staa huyo kabla ya dirisha hili la uhamisho wa majira ya kiangazi huko Ulaya kufungwa.

Kwa mujibu wa Prade, timu yake ilishindwa kumsajili Raphinha kutoka Sporting kwa sababu klabu hiyo ya Ureno haitaki kuwa na pengo kubwa zaidi kwa kuwa mpango wao ni kumuuza nahodha wao kwenda Bernabeu kwa ada ya pauni milioni 63.

"Sporting wanaweza kuwa wameshamaliza mambo ya kuuza kwa sababu Bruno Fernandes atakwenda zake Real Madrid kwa ada ya euro milioni 70 (pauni milioni 63)," alisema Prade alipozungumza na Corriere dello Sport kwenye utambulisho wa mchezaji Dalbert, aliyetua kutoka Inter Milan.

Wakati wa Ligi Kuu England, Manchester United na Tottenham Hotspur walihusishwa sana na mpango wa kumsajili kiungo huyo mchezeshaji, lakini dili hilo lilikwama hadi dirisha la usajili huko England likafungwa.

Fernandes alifunga mabao 32 na kutoa pasi za mwisho 18 katika mechi 53 alizochezea Sporting msimu uliopita, wakati msimu huu tayari ameshafunga bao moja na kutoa pasi za mwisho nne.






# CHICHARITO AUZWA SEVILLA

**MADRID,** Hispania

MCHEZAJI wa kimataifa wa Mexico, Javier Hernandez 'Chicharito' amekubali dili la kumrudisha tena Hispania kwa mara ya pili, wakati Sevilla jana ilikuwa ikitarajia kukamilisha usajili wa euro milioni nane, kwa mujibu wa ESPN FC.

Hernandez jana Jumapili alisafiri kwenda nchini Hispania kwa ajili ya kufanyiwa vipimo vya afya na atakabidhiwa jezi namba 14.

Mchezaji huyo ambaye alikuwa akiwaniwa na klabu za Ligi Kuu ya Marekani na Flamengo pamoja na Fiorentina, aliamua kubakia jijini London pale West Ham licha ya klabu hiyo kumsajili mshambuliaji wa Uswisi, Albian Ajeti mwenye miaka 22 kutoka FC Basel.

Chicharito mwenye umri wa miaka 31, alifunga bao dhidi ya Brighton wakati West Ham ikitoka sare ya 1-1 mapema mwezi huu.

Kwa mara ya mwisho alicheza kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, akiwa na Real Madrid kwa mkopo kutoka Manchester United wakati wa msimu wa 2014-15 kabla ya kusajiliwa Bayer Leverkusen, ambako alikaa kwa misimu miwili.

Ataongeza nguvu kwa klabu hiyo ya Hispania ambayo inapambana kwenye ligi hiyo ya Hispania.

Alikuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka West Ham kipindi hiki cha majira ya joto baada ya kukosa nafasi ya kucheza mara kwa mara.

# *Guardiola amtetea Sanchez kuboronga*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amemtetea Alexis Sanchez akisema kwamba kuboronga kwa mchezaji huyo huko Manchester United halikuwa kosa lake.

Sanchez ameondokana na balaa la Man United baada ya kukamilisha uhamisho wake wa mkopo wa msimu mzima wa kujiunga na Inter Milan katika dirisha hili la majira ya kiangazi.

Wakati mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Chile akilalamikiwa kila kona kwa kukosolewa kwa kiwango chake kibovu kufuatia kucheza ovyo tangu alipotua Old Trafford akitokea Arsenal Januari mwaka jana, Guardiola ameibuka na kusema wanaopaswa kulaumiwa ni Man United. Guardiola alisema: "Namfahamu Sanchez. Tumefanya kazi pamoja Barcelona. Namkumbali sana kama mchezaji, lakini pia kama mwanadamu.


"Ni mtu safi, mtaratibu na mpambanaji. Na sasa ameamua kwenda Italia kujiunga na moja ya timu kubwa Ulaya kwa sasa, Inter Milan, akicheza chini ya kocha mkubwa Antonio Conte.

"Nina uhakika mkubwa anakwenda kufanya vizuri kwa sababu namna ambavyo Inter wanacheza, unaonekana na mchezo wake. Kucheza karibu na Romelu Lukaku kwenye ushambuliaji, naamini atakwenda kuwa na wakati mzuri huko Milan."

Guardiola alisema Sanchez hakupaswa hata chembe kubebeshwa lawama, kwa sababu soka ni mchezo wa timu na si mtu mmoja mmoja.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# GUARDIOLA: AGUERO ATAKUFA AKIFUNGA

Sergio alifunga mabao Argentina wakati akiwa na miaka 16, atakufa huku akifunga...

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amemsifia Sergio Aguero baada ya Manchester City kuibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Brighton and Hove Albion, akidai kwamba mshambuliaji wake huyo "atakufa huku akifunga mabao".

**Aguero alifunga mara mbili katika kila kipindi wakati City wakipata ushindi huo nyumbani kwenye mchezo wa Ligi Kuu England Jumamosi, na mshambuliaji huyo wa Argentina akipaa kileleni kwa kuwa na mabao sita katika mechi nne alizocheza na pia alitengeneza bao la Bernardo Silva.**

Bao la uongozi la Kevin De Bruyne katika sekunde ya 68 liliipeleka City kwenda kushinda mechi yao ya tatu kati ya nne.

"Sergio alifunga mabao Argentina wakati akiwa na umri wa miaka 16 na atakufa huku akifunga mabao," alisema Guardiola.

"Ana kipaji cha aina yake na napenda huwa anajaribu kila mara. Tangu siku ya kwanza tumebadilisha mambo, lakini nafurahishwa na kujituma kwake. "Bila shaka tunahitaji mabao, kila mmoja anajua. Anatusaidia na mabao yake, lakini hata siku ambayo hafungi, tunahitaji uwapo wake. Nina furaha kubwa juu yake.

"Mchezo ulikuwa mgumu, matokeo yalikuwa ni 4-0, lakini kiwango hakikuwa cha juu kwa sababu Brighton walicheza vizuri. Timu chache zinakuja hapa kucheza kwa hamasa kama hii.

"Wachezaji wangu wa mbele walicheza vizuri na walitengeneza tofauti nzuri. Makocha kama Graham Potter ni wazuri kwenye soka."

Aymeric Laporte aliondoka uwanjani akiwa kwenye machela baada ya kuumia goti kipindi cha kwanza na kumfanya Fernandinho achukue nafasi yake kama beki wa kati.

Kiungo huyo sasa atalazimika kuendelea kucheza katika nafasi hiyo, kwa kuwa Nicolas Otamendi ndio beki pekee wa kati aliyebakia hapo City, kwani John Stones bado hajapona majeraha yake ya nyama za paja, wakati timu hiyo ikielekea kwenye mechi za makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Guardiola alimzungumzia Fernandinho na kusema: "Yeye ni kiungo wa kati, kila mmoja anajua hilo, lakini nafikiri ana jukumu kwa sasa la kucheza kama beki wa kati.

"Tatizo tulilonalo ni namna atakavyoweza kuzoea haraka. Ana akili na yupo imara kwenye kupiga mipira ya kichwa.

"Anaweza kucheza nafasi zote. Lakini kucheza kama beki wa kati kwa kipindi chake chote cha uchezaji hilo sijui."

## ZISIKUPITE

### NEYMAR AKWAMA BARCA

NEYMAR kurudi Barcelona kumeshindikana na mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 27, sasa amekubali kubaki na mabingwa hao wa Ligue 1, Paris St-Germain. ***(Sun)***

### KAMKIMBIZA SANCHEZ

ALEXIS Sanchez, 30, amejiunga na Inter Milan kwa mkopo wa muda mrefu baada ya kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer kumwambia mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Chile kwamba atacheza tu kwenye michuano ya kombe la Europa League. ***(Sun)***

### ERIKSEN ANUKIA KUAMKIA JUVE

KIUNGO Mdenmark Christian Eriksen, 27 bado anaweza kuondoka Spurs, kufuatia Juventus kumpigia chapuo dakika hizi za mwisho kabla ya dirisha la usajili Ulaya kufungwa leo saa sita usiku. ***(Express)***

### POGBA KUIGOMEA UNITED

KIUNGO wa Ufaransa Paul Pogba, 27, atakataa Manchester United kumshawishi kutia saini mkataba mpya akilenga kufanikisha kujiunga na Real Madrid. ***(Mirror)***

### BAYERN BADO INAYE SANE

BAYERN Munich bado inahitaji kumsajili winga wa Manchester City, Leroy Sane - ingawa Mjerumani huyo mwenye umri wa miaka 23, anajiandaa kuwa nje kwa kipindi kirefu akiuguza majeraha. ***(Mirror)***

### NEYMAR AMZUIA ERIKSEN PSG

KITENDO cha Neymar kushindwa kujiunga na Barcelona, kimehitimisha mchakato wa kiungo Mdenmark, Christian Eriksen, 27, kutua PSG kwa dau la pauni milioni 72 akitokea Tottenham. ***(Football. London)***

### DE GEA ANUKIA SOKONI JANUARI

MANCHESTER United inaweza ikawa inatazama kumuuza kipa Mhispania David de Gea, 28, katika dirisha la usajili la Januari kufuatia wasaka vipaji wao kuwa mawindoni Ulaya wakisaka kipa mpya. ***(Sun)***

### ROMA YAMTAKA FODEN

RANGERS na Roma zimetoa maombi ya kuitaka huduma ya kiungo wa Manchester City na England U-21, Phil Foden, 19, kwa mkopo. ***(Mirror)***

### HERNANDEZ AOMBA KUSEPA

STRAIKA wa West Ham na Mexico, Javier Hernandez, 31, ameomba kuondoka wakati huu akikaribia kujiunga na Sevilla. ***(Mail)***

### GERRARD 'ASARENDA' KWA KENT


KOCHA wa Rangers, Steven Gerrard amenyosha mikono juu kuhusu uwezekano wa kuinasa saini ya winga Ryan Kent, 22, kutoka klabu yake ya zamani, Liverpool. ***(Express)***

### FERNANDES KUZUIWA SPURS

KIUNGO wa Ureno, Bruno Fernandes, 24, alikubali kujiunga na Tottenham kutoka Sporting Lisbon, lakini klabu hiyo ya Primeira Liga ikazima mpango huo. ***(GQ Portugal via Mirror)***

## HABARI MICHEZO

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Lipuli | 1 | 1 | 0 | 0 | 3 | 1 | 3 |
| 2. Simba | 1 | 1 | 0 | 0 | 3 | 1 | 3 |
| 3. Kagera Sugar | 1 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 3 |
| 4. Namungo | 1 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 3 |
| 5. Azam | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 |
| 6. Ruvu Shooting | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 |
| 7. Polisi Tanzania | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 |
| 8. Mwadui | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 |
| 9. Mbao | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 |
| 10. Alliance | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 |
| 11.Mbeya City | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 12.TZ Prisons | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 13.Ndanda | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 |
| 14.Yanga | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 15. Coastal Union | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 16. Singida United | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 17. Kinondoni MC | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 18. Mtibwa Sugar | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 0 |
| 19. JKT Tanzania | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 0 |
| 20. Biashara United | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 |

# AZAM FC YAITAFUTIA KASI TRIANGLE FC CAF

**Na Mwandishi Wetu**

AZAM FC, imeendelea kujiimarisha kuelekea mechi yao ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Triangle FC ya Zimbabwe baada ya jana kuichapa Transit Camp mabao 3-1 kwenye mchezo wa kirafiki uliochezwa Uwanja wa Uhuru.

**Septemba 13, mwaka huu Azam itaikaribisha Triangle FC kwenye mechi ya mkondo wa kwanza kabla ya kurudiana Septemba 27 nchini Zimbabwe na mshindi wa jumla atacheza mechi ya mchujo na timu atakayopangiwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf).**

Timu zitakazotolewa kwenye raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa ndizo zitakazopangwa kucheza mechi ya mchujo na timu zitakazopenya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho na mshindi atatinga moja kwa moja hatua ya makundi ya michuano hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Azam na Yanga inayoshiriki Ligi ya Mabingwa Afrika, ni timu pekee zilizobaki kwenye michuano ya kimataifa kwa upande wa Tanzania Bara baada ya Simba (Ligi ya Mabingwa) na KMC FC (Kombe la Shirikisho) kutolewa raundi ya awali.

Katika mechi hiyo ya jana, Azam FC ambayo imetinga raundi hiyo ya kwanza kufuatia kuitoa Fasil Kenema ya Ethiopia kwa jumla ya mabao 3-1, ilianza kupachika bao la kwanza kupitia kwa Daniel Amoah kabla ya Donald Ngoma aliyetupia mawili kuwafanya kuwa mbele kwa mabao matatu.

Bao la kufutia machozi kwa upande wa Transit Camp katika mechi hiyo iliyohudhuriwa na mashabiki wachache, lilizamishwa kimyani na Samson Mkwangwa.

Kocha Mkuu wa Transti Camp, Rajabu Bwamkuu, akizungumzia mechi hiyo alisema ni wakati wa kutumia makosa waliyoyafanya na kujipanga upya.

"Bado ninaijenga timu na wachezaji wanajua kazi yao kushindwa haiwezi kuwa mwisho wetu, tutaendelea kujiimarisha," alisema kocha huyo ambaye timu yake inashiriki Ligi Daraja la Kwanza inayorajiwa kuanza Septemba 14, mwaka huu.

# Waamuzi 21 wafeli mtihani Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

JUMLA ya waamuzi 14 na wasaidizi 10 wanatarajiwa kuchezesha Ligi Kuu Zanzibar msimu huu baada ya kufaulu masomo yao ya utimamu wa mwili na mtihani wa kuandika darasani.

Jumla ya waamuzi walioshiriki mtihani huo walikuwa 45 na kati yao 21 hawakufanya vizuri, hivyo watachezesha Ligi Daraja la Kwanza Kanda.

Akizungumza na gazeti hili Katibu wa Kamati ya Waamuzi, Muhsini Ali Kamara, alisema waamuzi hao watachezesha ligi hiyo katika viwanja tofauti vitakavyochezewa ligi hiyo ikiwamo kile cha Gombani Kisiwani Pemba na vilivyopo hapa kisiwani Unguja Mau na Amaan.

Alisema msimu huu kwa waamuzi utakuwa tofauti ikilinganishwa na misimu mingine ikiwamo waamuzi wa Unguja watachezesha michezo itakayochezwa Kisiwani Pemba na Wapemba watakuja Unguja, huku wakitegemea zaidi ratiba ya ligi hiyo.

"Waamuzi msimu huu watazunguka, watachezesha mechi za Pemba na za Unguja, watachanganyika wote kwa pamoja haitakuwa kama misimu iliyopita kama kwa waamuzi wa Pemba wachezeshe Pemba tu na Unguja wachezeshe Unguja tu, hapana wote watazunguka katika viwanja vilivyopangwa kuchezewa ligi," alisema.

Aidha, alisema msimu huu kamati hiyo imejipanga kuhakikisha waamuzi watachezesha kwa kufuata sheria 17 za soka na haitaacha kumchukulia hatua mwaamuzi atakayeharibu mchezo kwa makusudi.

Hata hivyo, amewaomba mashabiki wa soka visiwani Zanzibar kuacha tabia ya kutukana waamuzi pindi wawapo mchezoni na badala yake waongozwe na busara kwa kuzisoma na kuzitafsiri sheria za soka.




Abdallah Pazi 'Dulla Mbabe' (kushoto) akimwadhibu Mchina, Zulipikaer Maimaitiali, katika pambano lililofanyika China wiki iliyopita na kutwaa ubingwa wa WBO Asia Pacific uzito wa Middle baada ya kumpiga kwa Knockout (KO) raundi ya tatu. **PICHA: MTANDAO**

# *Dulla Mbabe kutua leo na ubingwa WBO*

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kufanya kweli kwa kuipeperusha vema bendera ya Tanzania nchini China kwa kumtwanga kwa Knockout (KO) raundi ya tatu mwenyeji, Zulipikaer Maimaitiali, bondia Mtanzania, Abdallah Shaaban Pazi 'Dulla Mbabe' anatarajiwa kuwasili nchini leo asubuhi akiwa na taji lake la ubingwa wa WBO Asia Pacific uzito wa Middle.

Katika pambano hilo lililopigwa juzi kwenye Ukumbi wa TSSG Center mjini Qingdao, China, Dulla Mbabe alilianza kwa kasi na kumpelekea makonde mfululizo Zulipikaer, ambaye ni bondia namba moja China na aliyekuwa akishikilia mkanda huo, kabla ya kumkalisha chini raundi ya tatu.

Akizungumza na Nipashe juzi akiwa nchini humo Dula Mbabe alisema ameshukuru kupata ubingwa huo aliokuwa anautamani kwa muda mrefu, alisema licha ya pambano hilo kuwa gumu na lenye ushindani mkubwa alijituma mpaka kuhakikisha anapata ushindi huo ugenini.

"Mpambano ulikuwa mgumu, lakini nashukuru nimejitahidi nimepata ubingwa ambao umetokana na dua za Watanzania," alisema Dulla.

Aliwataka Watanzania pamoja na mashabiki wa mchezo huo kujitokeza kwa wingi leo asubuhi katika Uwanja wa Ndege Julius Nyerere sasa tatu asubuhi kumpokea kufuatia kuipeperusha vema bendera ya nchi kwenye medali ya masumbwi.

Kwa upande wake promota wa Dulla Mbabe, Jay Msangi, alisema kijana wake ameliletea sifa taifa lake, Tanzania kwa ushindi huo.

"Ni heshima kubwa, wadau tujitokeze kwa wingi kwenye hafla ya kumpokea bingwa huyu siku ya Jumatatu saa tatu na nusu asubuhi pale Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere," alisema Jay Msangi.

Kwa ushindi huo, sasa Dulla Mbabe anashikilia mataji mawili makubwa, lingine ni la WBF Intercontinental uzito wa Super Middle baada ya kumpiga Mtanzania mwenzake, Francis Cheka kwa KO pia raundi ya sita Desemba 26, mwaka jana katika Ukumbi wa PTA, Sabasaba jijini Dar es Salaam.

# Michezo

Jumatatu Septemba 2, 2019

Nipashe



Guardiola: Aguero atakufa akifunga

UKURASA 30

TUMEUA...




Washambuliaji wa Juventus, Gonzalo Higuain (kulia) na Cristiano Ronaldo, wakipongezana baada ya mechi ya Serie A kumalizika, huku beki wa Napo, Kalidou Koulibaly akimwaga machozi chini baada ya kujifunga dakika za mejeruhi na kuwafanya wenyeji hao kushinda 4-3 juzi. **HABARI UK. 28**

## Neymar basi tena Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imesitisha mazungumzo na Paris Saint-Germain kwa ajili ya kumsajili Neymar, lakini watatoa ofa nyingine kwa nyota huyo...




HABARI UK 28

## Klopp: Mane hana hasira na Salah

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amethibitisha kwamba, Sadio Mane "alikwazika" baada ya kuonyesha ishara ya...




HABARI UK 28

# Simba yaja na mkakati mpya

## Mo amwaga sera, Kagere kuletewa wembe mpya unaomzidi kucheka na nyavu huku...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Klabu ya Simba, Mohammed 'Mo' Dewji amewataka wapenzi na wanachama wa klabu hiyo kuwa wavumilivu baada ya timu yao kutolewa mapema katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imefahamika miamba hiyo imeelekeza nguvu zake kusaka straika zaidi ya Meddie Kagere.

**Mabingwa hao wa Tanzania, Simba wametupwa nje mapema kwenye raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kufuatia kulazimishwa sare ya bao 1-1 na UD Songo ya Msumbiji katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, ikiwa ni baada ya mechi ya awali ugenini kulazimisha suluhu, hivyo kutolewa kwa faida ya bao la ugenini.**

Kwa kipindi chote tangu Simba kutolewa Jumapili ya Agosti 25, mwaka huu, uongozi wa klabu hiyo ulikuwa kimya huku mashabiki wa timu hiyo wakishindwa kuelewa kinachoendelea.

Lakini Jumamosi Mo, aliibuka na kuwataka Wanasimba kuwa wavumilivu baada ya timu yao kutolewa mapema kwenye Ligi ya Mabingwa, huku taarifa zaidi kutoka chanzo chetu ndani ya klabu hiyo zikieleza hasira yao sasa ni kutafuta straika zaidi ya Kagere.

"Wanasimba, mnisamehe kwa ukimya. Maumivu ya matokeo yametupata sote. Naomba tukumbushane, sisi ni Simba! Simba lazima anyanyuke! Hawezi kukata tamaa. Niwaombe tusivunjike moyo wala kukata tamaa. Hatutaogopa maneno ya watu na hatutaacha kupambana na kujipanga kwa ajili ya malengo yetu," alisema Mo kupitia ukurasa wake wa Instagram.

Alisema msimu huu watautumia kikamilifu kuhakikisha wanaboresha mipango yao ili msimu ujao warudishe furaha ya wapenzi wa klabu hiyo.

"Tumwombe Mwenyezi Mungu atutangulie katika safari yetu endelevu. Tukumbushane tena: Roma haikujengwa kwa siku moja. Tuwe wavumilivu, tutafika tu Insha'Allah," alisema.

Hata hivyo, chanzo chetu kilieleza: "Unajua kwa ujumla uongozi umeumia sana kutokana na matokeo hayo, na umeona kuna haja ya kutafuta straika mwenye uwezo kama ama zaidi ya Kagere kwa kuwa tatizo lilionekana katika safu ya ushambuliaji.

"Hata kocha Aussems [Patrick], alisema mara tu baada ya ligi ya msimu uliomalizika kuwa anahitaji straika zaidi ya Kagere, lakini uongozi haukulifanyika kazi ipasavyo, jambo ambalo limeonekana wazi kwenye mechi dhidi ya UD Songo.

"Shida ni pale mabeki wa upinzani wanapobaini straika pekee na wembe ni Kagere, ndiye anayepelekewa mipira, hivyo anapobanwa biashara inakuwa imekwisha, na ukitazama mechi iliyopita Bocco [John] alikuwa majeruhi," kilisema chanzo chetu.

Aidha, kilifafanua kuwa mchakato huo utafanywa kipindi cha dirisha dogo ili kutoa nafasi kwa straika huyo kuanza kuzoeana na wachezaji wenzake kabla ya msimu ujao kuanza.

"Lengo kwa sasa Simba inataka kujenga timu itakayokaa na wachezaji wake kwa muda mrefu, waweze kuzoeana tayari kwa msimu ujao, hilo ndilo unaolitaka uongozi kwa sasa," kilisema chanzo hicho.

Msimu uliopita Simba ilitinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa lakini moja ya makosa yanayoelezwa kufanya ni kuacha baadhi ya wachezaji wake nyota, kama kiungo James Kotei na beki Juuko Murshid kuondoka huku wachezaji wapya waliosajiliwa wakichelewa kuzoeana na wenzao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002